KWA AJILI YA WANAUME TU

SOMO LA WARUMI

NA: Gary A. Taylor

Orodha ya Yaliyomo

Utangulizi..... *7*
Sura ya 1: *Wewe ni mtumishi?*..... *11*
Sura ya 2: *Ni kwa Jinsi Gani unamtumikia Mungu?*..... *15*
Sura ya 3*: Kuishi kwa Imani*..... *21*
Sura ya 4: *Nguvu ya Mungu imeonekana katika uumbaji*..... *25*
Sura ya 5*: Kuchemsha chura*..... *31*
Sura ya 6: *hakuna nafasi ya kunyosheana vidole*..... *37*
Sura ya 7: *Si kwa kile unachokifikiri*..... *41*
Sura ya 8: *Tutasimama na Hatia mbele za Mungu*..... *43*
Sura ya 9: *Utii Ni Muhimu kuliko Mila*..... *47*
Sura ya 10: *Uaminifu wa Mungu*..... *51*
Sura ya 11: *Hakuna mwenye haki bila Kristo*..... *55*
Sura ya 12: *Haki kwa njia ya Imani*..... *59*
Sura ya 13: *Kuhesabiwa haki kwa njia ya imani*..... *63*
Sura ya 14: *Ibraham: alihesabiwa haki kwa Imani*..... *69*
Chapter 15: *Haki huja kwa Imani*..... *73*
Chapter 16: *Kaa ukimtazama Mungu*..... *77*
Chapter 17: *Amani na Furaha*..... *81*
Chapter 18: *Upendon wa Kristo usio na Masharti*..... *85*
Chapter 19: *Uzima Ndani ya Kristo*..... *89*
Chapter 20: *Hukumu Yaweza Kubadilishwa Kwa Msamaha*..... *93*
Chapter 21: *Kufa, Kuwa hai katika Kristo*..... *97*
Chapter 22: *Muumini haogopi Kifo*..... *103*
Chapter 23: *Dhambi Ina nguvu*..... *107*

Chapter 24: *Muumini si Mtumwa wa Dhambi* *111*
Chapter 25: *Ni Yesu tu anayeweza Kutuweka Huru*..... *115*
Chapter 26: *mapambano yetu ya dhambi*..... *119*
Chapter 27: *Mapambano Yetu Binafsi* *123*
Chapter 28: *Uzima kwa njia ya Roho*..... *127*
Chapter 29: *Utamtambuaje Mkristo*..... *131*
Chapter 30: *Ni lazima tuishi kwa Roho*..... *137*
Chapter 31: *Waumini wanashiriki katika utukufu wa Mungu*... *141*
Chapter 32: *Maisha yajayo* *145*
Chapter 33: *Roho Mtakatifu Huomba* *149*
Chapter 34: *Mungu anatenda Kazi wapi?*..... *155*
Chapter 35: *PredestinationKuchaguliwa Tangu Asili*..... *159*
Chapter 36: *Mbadala wa upatanisho wetu*..... *163*

Dibaji

Mungu alipowaita na kuwavuvia waandoishi wa agano jipya, hakuchagua watu ambao walikuwa wameacha mambo yao makubwa iliw aweze kujiandikia mambo yao wenyewe. Alisema na watu ambao miguu yao ilikuwa ni michafu kwa sbabu ya vumbi la Rumi na utawala mzima. Aliweka ujumbe wake kwa watu amabo mikono yao ilikuwa imezowea kushika samaki na hata mikono yao ilikuwa imechakaa kwa sababu ya kusuka nyavu kila mara. Alikamata akili za watu walikuwa wanajua kushindwa, kughadhibika na hata kupoteza. Alitumiwa watu waliokuwa tayari kupoteza vyote kwa ajili ya yesu na waliopigwa mawe kama malipo yao, mundu na mijeredi.

Alipowatenga watu wa hadhi kubwa katika dini na elimu kubwa alimfanya kuwa kipofu na hata kumvunjavunja Sauli. Alimnyenyekeza na hata kumfukisha katika kiwango cha kuitwa Paulo, Mtumishi aliyefunzwa na Mungu aliyesema, “Kitu cha kufaa mabacho watu hawa wanazunguka nacho, ninakiharibu na hata kukitupilia mbali—kwa ajili ya mambo yangu ninayoona yanafaa. Kwa nini? Kwa sababu Ya Kristo. Ndiyo mamabo yote nilyoyaona kuwa ni muhimu katika maisha yangu yamefika mwisho. Ukilinganisha na faida a kumjua Yesu kama Bwana, mzaliwa wa kwanza, kila kitu nilichowaza kwanza hakikuwa

kinafaa—Mavi ya mbwa. Nimeyatupilia yote ili nimkumbatie Kristo nay eye anikumbatie." (Wafilipi 3:7-9, Ujumbe)

Leo Mungu bado anatafuta watu kama hao. Anataka watu amabao anaweza kusema nao kwa uwazi na ujasiri. Hatafuti walio kamili bali waliojeruhika, wamesamehewa, na waliotengenezwa. Hatafuti wanojivuna au kujikweza. Anatafuta wale wanaojuwa kwamba wao ni wapokeaji wa wa upendo amabao hawakuhustahili; watu ambao kupitia wao wanaweza kuonesha huruma na shauku kwa wale wanaohangaika.

Kwa Gary Taylor, Mungu kaisha mpata Mtu kama huyo. Katika yeye Mungu kaisha jipatia mtu amabaye amesha kabiliana na mafanikio na hata hasara; Mtu aliye na nguvu za ziada na hata ufahamu ambaye kaamua kumtegemea Mungu kwa nia ya Bwana. Wakati wote, Gary yuko sokoni, akijadiliana katika meza ya mkutano nyuma yake kuna eneo la ujenzi. Anaingiza hasara katika mambo yake. Azungumzapo na watu anawaeleza juu ya mambo aliyokutana nayo aliyoyategemea na ahata akajikuta katika hatari ya kupoteza masiha yake. Anapoanzisha mazungumzo na watu wengine nasema yale aliyokutana nayo kabisa kama mfuasi wa Yesu. Anashauku kubwa ya kila mtu kukutana na ujuzi na utimilifu wa maisha katika Kristo.

Ni kutoka katika maisha yake na kutokana na macho haya na moyo huuu amabo Gary aliujua na kuifahamu akili ya Kristo katika barua ya Paulo kwa waumini wa Rumi. Juma baada ya juma amekuwa na kazi ngumu na hata katika mazingira ya nyumbani kwani kamruhusu Mungu kukamata usikivu wake na kuweka maisha ya somo la Warumi katika moyo wake. Na matokeo ni hii kazi ya kitabu cha toleo la 65 iliyoandikwa na mtu wa kawaida ambaye anashauku ya kuona Mungu anafanya vitu vikubwa zaidi. Haya yalifundishwa kila juma na mtu ambaye alikuwa ni mwepesi wa kuwaeleza watu wake kile alichowaeleza Paulo wafilipi, "Si kwamba ni,mekwisha kufika, au anumekwisha kuwa mkamilifu: la! Bali nakaza mwendo ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na kristo." (Wafilipi 3:12, NASB)

Mtu yeyote wa kike au wa kiume apate busara ya kusoma masomo haya. Maprofesa na wachungaji wamefaidika na kile Gari amekiandika. Hata hivyo kitabu hiki ni kwa ajili ya " wanaume haswa." Kimeandikwa ili wanaume waweze kugundua na kujengwa katika Kristo. Lakini kwa kujua moyo wa gari kimeandikwa pia ili wanaume wapate kuwa waaminifu katika kufundisha na kusaidia kuwajenga wanaume wengine; ili waweze kufaya ushauri wa Paulo kwa kijana wake Timotheo, "mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi , uyaweke haya kwa watu waaminifu ambao wataweza kuwafundisha na wengine pia."
(2 Timotheo 2:2,)

Wayne Bristow
Edmond, Oklahoma

Utangulizi

Tafadhali tambua sina elmu kubwa. Mafundiho yangu makubwa nimeyapata kwa bwana na kutoka kwa watu waliowekeza maisha yao ndani yangu. Watu hawa ni baba yangu, mama yangu, Dr. Wade Akins, Pioneer Missions missionary; Dr. Philip Jett, mchungaji wangu; Dr. David Dockery, Raisi wa Union University; Wayne Bristow, mwanzishi wa Huduma ya Total Life International Ministries; na wamisionari wengi waliofanya kazi name katika zaidi ya safari za kimisionari 75 katika karne mbili zilizopita katika mataifa manne tofauti.

Baada ya kongamano la Maximum Man conference lililofanyika Jackson, TN in 2004, niliombwa na walei wengi kufundisha masomo ya Biblia kwa juma kwa ajili ya wanaume tu. Kusudi la somo ilikuwa ni kuwafanya wanaume wa madhehebu yote, maadili yote, jamii na maswala ya kiuchumi kuwaleta pamoja kwa ajili ya kujifunza neno la Mungu. Kwa miaka miwili nilisema "hapana" kwa watu na hata Bwana kwasababu nilihisi kwamba sisitahili kufanya jukumu hili. Baada ya maombi mengi bwana alinipatia amani na mwongozi wazi mwezi wa February 2006. Masomo yalianza na kitabu cha Luka na ilituchukua miaka miwili tukijifunza maisha ya Kristo.

Tulianza na kundi dogo la wanaume kama 15-20 waliokuwa wakihudhulia kila juma. Tulikuwa kukichukua sura katika biblia na tunaiangaia kutoka katika historian a mtazamo wa kitheologia. Kwa ujumla nilikuwa najaribu kuweka kweli za Kiroho na kuweka katika matumizi ya mazingira ya leo.

Mwaka uliofuata tuliingia katika ktabu cha Matendo kwa muda wa mwaka mmoja na nusu. Katika mayendo, tulijifunza kanisa la kwanza, Roho Mtakatifu, na ujuzi wa Huduma ya Paulo.

Na baada ya kuamaliza kitabu cha warumi tuliingia kitabu cha Warumi, na kilichukua mwaka mmoja na Nusu kukikamilisha. Katika somo hili tulijifunza jinsi ya kusihi maisha ndani ya kristo. Kitabu cha warumi kina sura 65 fupi fupi ambazo ndizo zilitengeneza notsi zangu kwa ajili ya masono ya kila juma. Maombi yangu na matumaini yangu ni kwamba walei watayatumia haya kama njia ya kuwafundisha wanaume wengine misingi na mafunsisho ya msingi ya ukristo kwa mtazamo wa mtu mlei.

Maandiko mengi ya theologia yameandikwa katika Lugha mabayo ni ngumu kwa mtu wa kawaida. Kwa hiyo nimeandika kwa kueleza mamabo ya kiroho kwa lugha rahisi inayotumiwa na watu wa sasa kwa nyakati za sasa.

Mara nyingi wanaume wamezimishwa katika mambo ya kikanisa na hivyo kuwa watu wa dini tu na imeleta mchanganyiko na kuondoa uelewa. Yesu alitumia mifano rahisi kueleza theologia ya ndani. Hakusema maneno ambayo wengine hawakuyaelewa. Nimejaribu kutumia mifano ya siku hizi kueleza maana ya theologia ya wazo kuu amabalo halipaswi kupotea katika mafundisho ya biblia.

Kutokana na uzoefu wangu nimejifunza kwamba kila mtu anajambo linalomsumbua katika maisha yake. Miaka kadhaa iliyopita niliwaza, kama ningeweza kuwa “kama hivi” ningefaulu. Hadi nilipotambua kwamba kumbe kuwa kama Fulani tayari ni tatizo. Ukweli ni kwamba “Kila mtu” anajambo linalomsumbua

katika maisha yake. Kama sisi wanaume tutakuwa wawazi na kuwa wazi kati yetu juu ya kile kinachoendelea katika maisha yetu ninaamini Mungu angeanza kufanya jambo kubwa katika maisha yetu.

Hatua ya kwanza ya kukua katika Ukristo ni kutambua kwamba kuna tatizo ambalo huwezi kulirekebisha. Mtu anayekimbilia mlango wa kujikataa mara zote hujimaliza na ni muda gani mungu anaweza kumpatia nafasi ya kumrejesha kwake tena.

Kwa kuwa tunaona maisha si kwa ajili yetu bali kwa ajili ya uoendo wa mungu tutabadilika sana. Shauku zetu ziwe shauku za Mungu na kwa hatu ahiyo Mungu ataumba jambo jipya katika maisha yetu. Tunatambuliwa na Kristo. Tunahangaika kuendeleza uhusiano wa kweli na wa maana na Kristo kwasababu tumepungukiwa uelewa kwa kweli wa pendo lake lisilo na mashariti na la kina.

Kwa kuwa tunatak kujua yajayo ni vyema kujua kwamba Mungu ndiye kashikilia yajayo. Ni maombi yangu kwamba utapata muda wa kusoma sura zote 65 na kumuruhusu roho Mtakatifu kusema na roho yako. Maombi yangu ni kwamba Mungu katika roho yako atainua ujasiri kwa ajili yake na utukufu wake.

Mwisho wa siku, Biblia inamambo matatu ya msingi:

1) Kumjua Mungu na kumpenda kwa kina;
2) Kuwapenda watu kwa kina, hata wale wanaokuudhi;
3) Kufanya wanafunzi na kufundisha wanaume kua wafuasi wa kweli wa kristo.

Mungu anatafuta wanaume watakaoongoza na kusimama kwa ajili yake. Ni matumaini yangu kwa roho wa Mungu katika maisha yako Kitabu hiki kitakuwa ni msaada wa kukukuza na kukuendeleza katika uelewa wa kina wa kweli za Kiroho za Neno la Mungu .

SURA YA 1

WEWE NI MTUMISHI?

Warumi 1:1-7

"Paulo, Mtumwa wa Yesu Kristo, aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa aihubiri injili ya Kristo."- Warumi 1:1

Katika tamaduni zetu leo kuwa mtumishi siyo nafasi nzuri ya kufurahisha. Watumishi hawapigiwi kura kama tunavyofanya mashuleni. Katika mitazamo ya tamaduni zetu watumishi wanaonekana kama wadhaifu, hawana heshima na hawaendani na tamaduni. Utumishi wa Paulo unatuonesha kwamba mtu wa kweli, mfuasi wa kweli wa Kristo. Umesha wahi kufikiri ni jambo gani linamfanya mtu aonekane kuwa ni wa kweli mfuasi wa kweli wsa Kristo anayefanana naye. Umeshawahi kuwaza ni vitu gani vinavyopelekea kuwa mtu wa kweli? Kuwa mtu halisi au wa kweli ni lazima uwe mtumishi wa Kristo.

Paulo, mwandishi wa Warumi alikuwa na akili, mnyenyekevu, anayetambua, mwenye nguvu, jasiri na kiongozi shupavu na alikuwa kajitoa katika wito alikuwa kaitiwa maishani mwake. Maisha ya Paulo ni maisha ya kiongozi jasiri aliyekuwa kaharibiwa na dhambi lakini akaokolewa kwa Neema ya Mungu. Kwakuwa likuwa ni kiongozi wa Kirumi na apia alikuwa I

kamanda wa kuigwa. Hakuna kazi iliyokuwa ni kubwa kwa Paulo. Hata hivyo hakubaki kama alivyokuwa baada ya kukutana na Mungu akielekea Dameski ambapo Mungu alimkabili. Uzoefu wake wa maisha, ujasiri wake na mateso yake yote ni ushuhuda wa mahusiano ya ndani kabisa na Bwana Mwokozi wake. Shauku yake na kufuata Roho ya mungu huku akiwekeza katika maisha ya watu inatupatia njia ya kufuata kwa jisni gani tunapaswa kusafikiri katika njia hii inaypitwa "Maisha". Paulo alikuwa ni mtumishi wa kristo. Hakuwa na ugumu katika hilo. Aliona hii kama ni lalama ya heshima. Hakuna aibu kujishusha ili kwamba Kristo apate kuonekana.

Tunaposafiri katika kitabu cha warumi tutamuona Paulo kama mwanasheria maarufu amejiweka kwa ajili ya Injili kwa wazi na kwa nguvu. Paulo alikuwa na shauku na kanisa la Rumi japo hakuwa amefika huko. Kanisa la rumi lilianza kama matokeo ya Pentekoste (Matendo 2). Kama tunavypjua kwamba Pentekoste halikuwa ni tendo la kawaida ambalo lilitokea katika siku ya sikukuu ya mavuno ambapo wayahudi wote walikuwa wamekusanyika ili kuweza kusherekea sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu.

Kusudi la barua ya Paulo ilikuwa ni kujitambulisha na kuonesha kwa uwazi imani yake. Kitabu cha warmi ni kizuri sana kwa ajili ya imani ya kikristo. Umeshawahi kujiuliza, " hivi misingi ya Ukristo inatoka wapi?" Kwa sehemu kubwa mafundisho haya yanatoka katika Kitabu cha Warumi.

Warumi inaweza kugawanywa katika makundi mawili: Sura ya 1-11 – "Nini cha Kuamini" na sura ya 12-16 – "Kwa jinsi gani tuamini." Lengo langu katika kitabu hiki ni kumruhusu roho Mtakatifu atuoneshe kwa njia ya Neno la Mungu kweli za Kiroho juu ya nini tuamini kulingana na Ytesu kristo. Inamaanisha kuwa wawakilishi sahihi wa Imani ya Kikristo.

Hebu tuanze na Mstari wa kwanza wa Warumi 1:1: *"Paulo, Mtumwa wa Kristo Yesu aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu."* Paulo anajumuisha mitazamo yake juu yake mwenyewe kwa maneno matano : "Ni mtumwa wa Kristo

Yesu." Haya maneno yanamaanisha nini? Kwa mtumishi unapaswa kuwa mnyenyekevu. Kwa Paulo kama raia wa Rumi kuchagua kuwa mtumishi lilikuwa ni swala ambalo halifikiriki. Hebu chukua mtu tajiri, mmarekani wa maisha ya kati kuwa mtumishi? Kuwa mtumishi inamaanisha mambo mengi:

1) **Kutii**: Bwana mkubwa anapokuwa ameagiza mtumishi anafanya nini? Hutii kwa mtazamo safi.

2) **Kutumika**: Kusudi la Mtumishi ni kutumika. Katika imani ya Kikiristo wewe si mfalme– huwezi kufanya mabo yako na wakati huo utumike.

3) **Kutegemea**: mtumishi humtegemea Bwana wake kwa ajili ya mabo yake mbalimbali.

Mstari wa kwanza unatueleza kutii, kutumika na kutegemea. Hafi tutakapokuwa na moyo wa kutumika vinginevyo hatuwezi kuyafanya haya. Nini mtazamo wako kuhusu Yesu? Mtazamo wako kuhusu kristo unatoa mwelekeo wa maisha yako. Sisi sote tunakuwa katika maisha tukiwa na mizigo mingi. Tunaendeshwa na dhambi za majivuno, wivu na hata ubinafsi kiasi kwamba tunafikia hatua ya kuwa vipofu. Kuna jawabu moja tu kwa ajili ya huu ilimwengu aliochanganikiwa na si jingine bali ni upendo wa Kristo.

Msatri wa 2: *"ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu."* Injili iliahidiwa (Mwanzo 2:3; Isaya 11:1; Zaburi 6:10). Moja ya vitu inayoifanya Injili iwe na nguvu ni kwamba katika matukio mengi miaka mamia iliyopita Mungu alitumia manabii kutangaza uijio wa Kristo. Si kwamba Kristo alijitokeza tu ahalafu watu wakaanza kueleza jinsi alivyo. Hapana ni zaidi ya hapo. Mungu alieleza kile anachokwenda kukifanya na alikitimiza. Ni eleze dini yeyote ambayo Mungu wake alitabiriwa kabla na ikatokea. Hii ni wazi juu ya asili ya uungu wake na nguvu zake za kiungu.

Mstari wa 3: *"Yaani habari za mwanawe aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya Mwili?"* Paulo anaeleza kwamba Yesu

ni mwana wa Mungu, alimwahidi masihi bwana aliyefufuka, “Ukoo wa Daudi.” Paulo anakaza kwamba yesu kwa kweli katimiza Agano la kale kwamba masihi atatoka ukoo wa Daudi. Kwa maelezo haya ya Imani anatambua nafasi yake na anatangaza kwamba anakubaliana na mafundisho ya maandisko na mitume. Paulo anaichanganua injili kwa njia ifuatayo :

1) Yesu alikuja Duniani kama mwanadamu kwa sili ya kawaida kabisa .

2) Yesu alikuwa sehemu ya ukuhani wa kiyahudi kwa jia ya ukoo wa daudi.

3) Yesu alikufa na akafufuka toka wafu.

4) Yesu alifungua mlango kwa ajili ya neema ya Mungu na wema upate kuachiliwa kwetu.

Kitabu cha warumi kinakuza mkazo huuna kutupatia maelekezo wazi ya jinsi gani ya kuishi maisha katika Kristo.

Mstari wa 5*: “ambaye katika yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani kwa ajili ya jina lake.”* Paulo anaamini kwamba msamaha wa dhambi zetu ni “neema .” Ni kitu ambacho hatukustahili. Neema imetolewa – hatukuifanyia kazi. Huwezi kufanya kazi ili upate neema. Neema inatoka kwa mtu aliye ni mkibwa katika madalaka kama vile Bwana kwa mtumwa wake. Katika asili yetu ya dhambi sisi hatustahili. Nje na Kristo tunahasira, hatutambuliki, watu tusio haki lakini kwa neema ya Mungu tumestahilishwa mahusiano na Yesu Kristo.

Unaweza kufikiri kufanya mabadiliko ambayo Paulo aliyafanya katika maisha yake? Utumishi siyo kitu cha asili. Iko kinyume na mbegu iliyo ndani yetu yaani DNA kama wanadamu. Kristo ni mbadilishaji wa mchezo. Upendo wake unasababisha kubadili namna yetu ya kuishi. Je uko tayari kuingia katika gharama za kuwa mtumishi mwaminifu na mfuasi ya Kristo?

SURA YA 2

NI KWA JINSI GANI UNAMTUMIKIA MUNGU?

Warumi 1:8-13

"Kwa Maana Mungu nimwabuduye kwa Roho yangu katika Injili ya mwana wake ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma."- Warumi 1:9

Kitu gani kinachokuvutia sana? Watu wengine wanavutiwa sana na familia zao, kazi, viburudisho, n.k. Paulo alikuwa anavutiwa na kumtumikia Kristo. Kabla hajaanza theologia yake ya ndani kuhusu injili Paulo anajiweka wazi na kuwaomba warumi waangalie yeye ni nani kama mwanadamu.

Watu walimtumikia Bwana kwa makusudi mengi. Paulo alielewa kuwa shauku ya mtu ndiyo inayomuongoza katika maisha yake. Wengine wanamtumikia Mungu kwa mambo yao. Wengine wanataka waonekane kuwa namaadili hata tofauti na jinsi walivyo. Wengine wanamtumikia Mungu kwa hofu kwamba wasipofanya Mungu atawaadhibu. Wengine wanamtumikia Mungu kwasbabau wameamuriwa na kuhamasihwa na kanisa. Wengine wanatumika ili waweze kulingana na matakwa ya kanisa kwasbabau kunakanuni fulani. Vijana wengi wanatumika kwasbabau wanaogopa karaha za wazazi maana wanawafokea na wanajisikia vibaya. Wengine wanatumika kwasbabau wanataka kupata pesa kanisani. Wengine wanaona kwamba huduma inaweza kuwawezesha kujulikana na watu wengine kibiashara. Swali ni kwamba, "Ni sababu ipi inakufanya umtumikie Mungu?"

Kujibu swali hili kwanza tunapaswa kuelewa kwamba yote haya hayana ukweli. Bila kujali ni huduma gani tunaifanya, **Paulo anatuambia wazi kwamba kama haitafanyika kwa upendo, kwa shauku ya moyo kumpendeza na kumtukuza Mungu hiyo haikubaliki.** 1 Korintho 10:31 inatuambia, "Iwe unakunywa au chochote ufanyacho ufanye kwa ajili ya utukufu wa Mungu."

Mabadiliko ya maisha ya Kikristo na huduma yote yamehusishwa na hsia halisi za mwanadamu. Hata kama mtu atamtumikia Mungu lakini kwa nguvu zao kunaweza kuonekana majaribu ya ubinafsi pale kazi ya mtu inaposhindwa kutambuliwa. Mungu alimtumia Paulo kwa sababu ya Neema ya Mungu na rehema lakini ni kwasbabau Paulo aliweka hisia zake sawa. Kusudi lake kuu katika maisha yake ilikuwa ni kumtukuza Mungu. Hiki ndicho peke yake Mungu amekikusudia kwetu sote– Upendo, Kutumika, na kumtii yeye ambayo inapelekea katika kumpendeza Yeye.

Mtari wa 9 inasema, *"Mungu nimtumikiaye kwa Moyo wangu."* Paulo anajua kwamba anapaswa kuunganishwa na Mungu katika Kristokabla roho yake haijahuishwa. Alipoyatoa maisha yake kwa Mungu Mungu alimbadilisha na kumfanya upya na kumpa uwezo wa kumtumikia Mungu katika roho yake. **Bila Kristo hatuwezi kumtumikia Mungu katika Roho kwasbabau roho zetu zimekufa na hazijahuishwa**. Huduma haina maana kama haujapokea mamabo ya kiroho kutoka kwa Mungu ili utumike. Huduma kwa nguvu zetu zinatimiza mambo ya binadamu. Huduma ya kweli inapaswa ujazwe na roho Mtakatifu. Paulo alikuwa ni mfarisayo, amefundishwa na kuelemishwa katika diniya kiyahudi . Alikuwa anajua jinsi wayahudi wanavyokuwa katika kumwabudu Mungu wao. Aliishi katika namna hiyo ya kuwa na njaa ya nguvu ubinafsi na hata unafiki. Mnafiki Ni nani? Mnafiki ni Yule anayejidai kuwa ni mwanadini kuliko hata alivyo. Sisi sote wakati mwingine tumeingia katika shida hii katika safari yetu ya maisha.

Katika Yohana 4:23-24, Yesu anamwambia msamalia katika kisima, "waabuduo katika kweli wanapaswa kuabudu katika Roho na kweli. Mungu ni roho wamwabufuo wanapaswa kumwabudu katika Roho na kweli ." Unaona, kabla Paulo hajawa mkristo amekuwa akimwabudu Mungu kitofauti ("Ikiwa mtu atajivuna kwa sababu ya mwili wake mimi ni zaidi: Nilitahiriwa siku ya nane, ya watu wa Israeli, wa kabila la Benjamini, mweburania wa waebrana, farisayo, nililitesa kanisa, kwa swala la sheria sikuwa na hatia. Lakini haijalishi ilikuwa vipi kwa ajili ya

faida yangu yote nayahesabu kuwa si kitu kwa ajili ya Kristo." Waflipi 3:4-7).

Ufunguo wa maisha ya Ukiristo ni kuwa na hisia za kweli ikiwa na maana kwamba uwe na wito wa ndani wa kumtumikia Mungu kwa ajili yake na si kwa ajili ya mambo yako. Hatuwezi kuhangaika. Kugandamizwa kunawafanya watu waasi au wageukie njia nyingine. Kwa fasheni hiyo hiyo hatuwezi kuongozwa na mila. **Tunaweza kuendeshwa na shauku ya kumpendeza Mungu yaani Mungu pekee wa kweli**. Maisha ya Paulo hayakuwa kwa ajili ya mambo yake; **ilikuwa ni kwajili ya kumfuata Mungu nay ale anayoyataka yeye afanye**. Paulo alikuwa ni mtu aliye Mruhusu Roho Mtakatifu kumuongoza, kumwelekeza na kuyaelekeza maisha yake.

Katika mstari wa 8-15, maneno ya Paulo yanaonesha alama za kweli, huduma ya kiroho. *"Kwanza **namshukuru** Mungu wangu katika Yesu Kristo kwa ajili yenu nyote kwa kuwa imani yenu inahubiriwa katika dunia nzima. Kwa maana Mungu nimwabuduye kwa roho yangu katika injli ya mwana wake nishahidi wangu **jinsi niwatajavyo pasipo kukoma**. Siku zote katika sala zangu nikiomba nije kwenu hivi karibuni Mungu akipenda kuifanikisha safari yangu. Kwa maana ninatamani sana kuwaona ili niwape karama za rohoni ili mfanywe imara; yaani tufarijiane ninyi na mimi kila mtu kwa imani ya mwenzake yenu na yangu. Lakini ndugu zangu sipendi msiwe na habari ya kuwa mara nyingi nalikusudia kuja kwenu nikauiliwa hata sasa ili nipate kuwa na matunda kwenu ninyi pia kama nilivyo nayo katika mataifa wengine nawiwa na wayunani na wasio wayunani nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima. Kwa hiyo kwa uande wangu mimi ni tayari kuihubiri injli hata na kwenu ninyi mnao kaa Rumi."* Hebu tuyaangalie maneno ya Msingi ili yatupatie uelewa sahihi wa kile paulo anachojaribu kukiwakilisha:

1) **Roho ya Shukrani** (Mstari. 8): Kushukuru kwa kile Mungu alichotufanyia. Vitu vyote vizuri vinatoka kwa Mungu. Mara nyingi mahitaji yetu hufunika baraka za Mungu alizotufanyia. Siku moja Rafiki yangu aliniita akaniambia, "Jana ilikuwa siku nzuri sana. Ilikuwa ni

siku yangu ya kuzaliwa na kijana wangu wa miaka 14 aliniimbia wimbo kwa mara ya kwanza." Kijana wake amambo mengi. Ilikuwa ni muujiza alisema. Mambo kama haya hutuweka katika hali ya kushukuru. Mara zote tumekuwa tukiangalia katika changammoto na mambo hasi yatikwamishayo katika maisha lakini kiukweli kuna mengi ya kushukuru kuliko hata yale tunayolalamika.

2) **Roho ya Kuwiwa** (Mstari. 9): Kujali mambo ya wengine. Mahtaji mengi yanatuhitaji kumuuliza Mungu nini cha kufanyaKuwiwa kwa ukweli ni tendo la kuonesha upendo wa kweli.

3) **Roho ya utii** (Mstari. 10a): Kutambua mamlaka ya Mungu juu yetu na kutiii uongozi wake.

4) **Roho ya upendo** (Mstari. 10b): Kufanya jambo bila upendo haina maana. Upendo ni kitovu cha maisha ya mkristo. Upendo wa Mungu hauna masharti. Halazimishi upendo wake kwetu na wala hatuendeshi.

5) **Roho ya unyenyekevu** (v. 11): Kuweka kando majivuno yetu na kutambua ni kwajinsi gani tunaweza kuwa katika hatari tusipokuwa na Mungu. Hii inatuleta katika swala la unyenyekevu.

6) **Roho ya Kuzaa** (Mstari. 12): Kuwa na roho ya upendo na huruma. Kuwa mwaminifu maana yake ni kuwa uanyejizalisha katika macho ya Mungu. Kipimo cha Mungu katika mafanikio ni mahusiano na sifa tulizo nazo kwake na wala si mafanikio ya pesa.

7) **Roho ya Utii** (v. 13): Kujitoa sisi wenyewe kwa Bwana. Hatuwezi kumpenda Mungu bila kuwa watii ikiwa na maana ya kusihi kulingana na viwango vyake na siyo viwango vyetu. Mungu anahitaji utii wetu kwasbabu hicho kinaonesha jinsi tunavyompenda.

8) **Roho ya kutamani** (v. 14): kujenga shauku ya kufuat makusudi ya kweli ya Mungu. Mtu anaweza kufuata makusudi yake lakini hawezi kuwa na furaha. Kila mtu alikuwa kakusudiwa na kaumbwa kwa kufuata makusudi ya Mungu ambayo matokeo yake ni amani. Huanza na roho ya kutamani.

9) **Roho ya ujasiri** (v. 15): Kuwa na ujasiri wa kusimama kwa ajili ya kristo. Wengu husimama kwa ajili ya vitu sahihi lakini Paulo anataka tusimame kwa ajili ya mambo ya kristo. Yoshua 1:8-9 inasema, "Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako bali yatafakali maneno yake usiku na mchana upate kuangalia kutenda sawa sawa na amneno yote yaliyoandikwa humo maana ndipo utakapoifanikisha njia yako kasha ndipo utakapostawi sana. Je! Si mimi niliyekuamuru uwe hodari na moyo wa ushujaa usiogope wala usifadhaike kwakuwa bwana mungu wako yu pampja nawe kila uendako.

Kumuruhusu Mungu kutubadilisha kuwa na roho kama ya Kristo ambayo Paulo anaiongelea katika sura hii ni ibaada pekee ya Mungu inayoweza kutimizwa. Tunapofika katika maisha yetu tunaona hatuwezi kwa nguvu zetu tunamuhitaji Mungu hapo sasa tunapaswa kujinyenyekeza na kuacha njia kwa ajili ya uongozi wake. Je utajitoa ili Mungu aweze kukuongoza katika njia yake?

SURA YA 3

KUISHI KWA IMANI

Warumi 1:14-17

"Kwa maana siionei haya Injili kwasababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye kwa muyahudi kwanza na kwa myunani pia."- Warumi 1:16

Rafiki yangu wa karibu mmisionari, Wade Akins, amekuwa akiishi kwa imani kwa zaidi ya miaka 40. Kuishi kwa imani siyo tu kumtumainia Mungu kwa jili ya kukupatia yale unayohitaji lakini pia kukupatia nguvu ya kukamilisha majukumu yako na kufanya sehemu yako. Hii sura inashughulika na swala la Imani, neno lenye maana nyingi. Imani inaweza kumanisha ni Uaminifu. Intumaini la kweli. Inamaanisha tumaini la ujasori. Waebrania 11:1 inatuambia, **"Iamni ni kuwa na uhakika wa mamabo yatarajiwayo mamabo ambayo ahajawepo wala kuonekana."** Paulo anamanisha nini hapa katika Warumi anapozungumzia juu ya imani iokowayo? Kabla hatujaanza kuchanganua ya jinsi Paulo anavyotumia neno hili katika sura hii, ni vyema kuelewa shauku ya Paulo katika maisha. Shauku ya Paulo tangu siku aliyogeuzwa na kuwa muumini aipokuwa akielekea dameski katika matendo 9, ilikuwa ni kazi yake kueneza Injili ya Kristo. <u>Jambo la mshingi la maisha yako ni kile inachokiamini kuhusu Yesu.</u> Haijalishi uko chama gani Republican au Democrat. Si kwamba wewe ni wadhehebu gani. Haijalishi wewe ni maskini au tajiri. Ni vile unavyoamini kuhusu mfufuka Kristo. Swala hli linaeleza mahusiano yetu na milele.

Paulo anatupa mtazamo safi jinsi gani tunapaswa kuutazama ulimwengu. Hebu tosome kuanzia msati wa 14*: "Ninawiwa na wayunani na wasio wayunani, wenye hekima na wasio na hekima."* Inamaanisha nini Paulo alipojiona yeye mwenyewe "Anawiwa" kwa ajili ya Kristo? Ngoja nikuulize swali: Unajisikiaje kuhusu uwajibikaji wako kwa Kristo? Unajisikia kabisa kuwa na jukumu la dhati au unampeleka mungu tu kama kwenye majaribio? Je unamruhusu Mungu akupatie siku 30 za

mateso na kama inawezekana je utakaa nayo au ikishindikana utaachana na huduma?

Paulo anawiwa *"na wenye hekima na wasio na hekima."* Maandiko yanatuonesha hapa kwamba mungu kaisha tupatia mwelekeo wazi sit u kuunganishwa na watu wanaoonekana kuwa kama sisi na wenye rangi kama yetu. Anatujulisha kwamba kila mmoja wetu analazimika kufundisha na kushirikisha injili kwa watu "Wote". Paulo alipojiona si kitu na kumruhusu Mungu kuongoza maisha yake, alianza kufanya kama kile Yesu alichokifanya– Kujitoa kwa wengine ili aihamasishe Injili.

Msatri 15: *"Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injli hata na kwenu ninyi mnao kaa Rumi."* Nini shauku yako? Unapenda kufanya nini haswa? Ni masaa mangapi unayatumia kuangalia TV? (Wastani wa wamarenai wengi hutumia masaa14 kwa siku wakiangalia TV, Facebook, barua pepe na Twitter). Unatumia masaa mangapi ukijifunza juu ya Mungu na ukiwekeza kwa wengine? Mara zote tunafanya tunayoyapenda sana. Najua vipaumbele vyangu vimeharibiwa. Msihi Mungu abadili shauku ya Moyo wako kama unahitaji mwongozo sahihi.

Mstari 16*: "Kwa maana siionei haya Injili kwasababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye kwa muyahudi kwanza na kwa myunani pia."* Ujumbe wa Injili unabadilisha maisha; inanguvu na iko kwa ajili ya kila mtu. Paulo anamwangalia Mungu na si mambo yake kwa sababu wokovu ni kwa kila mtu aaminie. Mungu aliwaita wayahudi wawe wateule wake (Mwanzo. 12:1-3). Kwa nini? Si kwasababu *walistahili* kuchaguliwa (Kumb. 7:7-8), lakini kwa sababu alitaka kushirikisha pendo lake na rehema, kwafundisha na kuwaandaa kwa ajili ya Kristo, Masihi.

Msatri 17: *"Kwa maana hali ya Mungu inadh9hirishwa ndani yake toka imani hata imani kama ilivyoandikwa "mwenye haki ataishi kwa imani:.'"* Injili inatuonesha ni kwa jinsi gani Mungu ni wa haki katika moango wake wa kutuokoa na pia jinsi gani tunaweza kustahilishwa kwa ajili ya uzima wa milele. Baada ya kumtumainia na kumwamini Kristo kinachofuata n mahusiano

yetu yanakuwa sawa na Mungu - “Mwanzo na mwisho.” Kwasababu ya imani yetu Mungu ametuhesabia haki. Hatuko haki kwasababu ya kile tulichokifanya lakini kwa kile Kristo alichokifanya pale msalabani. **Kuwa na imani, tunatakiwa kumtumaini na kuamini kwamba Mungu yeye ni yule ansemaye na anaweza kufanya kile anachokisema**.

Wakristo wegi wamekosa imani ya kweli katika Mungu. Imani ya kweli ni kumtumaini Mungu na kumruhusu Roho wa Mungu kuongoza njia zetu ili kwamba mapenzi yake yatimizwe katika maisha yetu. Imani ni kuamini kwamba Mungu anauwezo ya kuendesha mabo yote hata kama hatuwezi kuelewa ni kwa nini.

Kwa hiyo imani iokowayo ni nini? Ni pale mwanadamu anapoungana na Mungu kwa njia ya Imani katika Kristo. Imani iokowayo ni ya kiroho na inazaa tunda la roho. Imani iokowayo inatuhitaji kufa katika miili yetu na kumfanya Bwana kuwa uzima wetu. Imani iokowayo ni pale ninapoacha kujitegemea na kujiachilia katika ungozi wa Kristo. *“Kwanza walijitoa kwa Bwana.”* II Wakorintho 8:5

Je unataka kumpatia Mungu nafasi ili akuoneshe kwamba Yeye ni kweli? Utaishi kwa Imani? Utaanza kumtegemea kwa ajili ya mwongozo katika maisha yako? Je utajiachilia katika pendo lake kwa ajili yako?

SURA YA 4

NGUVU YA MUNGU IMEONEKANA KATIKA UUMBAJI WAKE

Warumi 1:18-27

"Kwasababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu-yanaonekana na kufahamika kwa kazi zake yaani-uweza wake wa milele na uungu wake hata wasiwe na udhuru."- Warumi 1:20

Hebu nikuulize swali: Kwa nini Mungu anahasira na watenda dhambi? Because they exchange the truth for a lie ("Wameibadili kweli ya Mungu na kwa ajili ya uongo, wameabudu na kutumikia vilivyoumbwa badala ya aliyeumba– ambaye milele anapswa kusifiwa. Amen." Warumi 1:25). Watenda dhambi wanafanya hivi kwasbabu wanahitaji kuamini mafundisho ya maisha yanayokubaliana na maisha yao. **Mungu hawezi kuvumilia dhambi kwasbabu asili yake ni maadili safi na kamili**. Mungu hawezi kukuacha au kuniacha tunapoanza kumuasi. Tunapokataa, kama wanadamu, kweli ya mungu, tunamkataa Mungu. Mungu huchukia tunapoendelea katika dhambi kwasbabau anataka kuondoa dhambi na kumrejesha mtenda dhambi. Tumemrahisisha Mungu na kusihi maisha yetu tunayoyataka. **Watu wote kila mahali wanasahili hukumu ya Mungu juu ya dhambi.**

Mistari ya 18-20: *"Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa mwanadamu waipingao kweli na uovu. Kwakuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhairi ndani yao kwa maana Mungu aliwadhihirishia kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana na kufahamika kwa kazi zake yaani uweza wake wa milele na uungu wake hata wasiwe na udhuru."* Je mtu anaudhuru juu ya kutokumwamini Mungu? Biblia inakataa! Je mungu atawatupa watu jehamanu bila kusikia Injili? Nini kitatokea kwa watu wa makabila wanaoishi katika visiwa jangwani ambao bado hawajasikia injili? Anapokufa anaenda wapi? Paulo anasema Mungu kajifunua kwa watu wote

kwa anjia ya uumbaji. Lakini kwa bahati mbaya watu wanaweza kukataa ufahamu huu wa msingi wa Mungu. Watu wanautabuzi wa ndani wa kweli ya Mungu, lakini wanaweza kuchagua kuikataa. Ngoja niweke kama hivi: Viwango vya watu vik juu kuliko hata tabia zao.

Ngoja tuangalie katika upande mwingine wa mijadala. Watu wengine hujadili kwamba kama Mungu kajifunua kupitia uumbaji wake kwa nini tunahitaji waminisionari? Rafiki yangu wa karibu, Wade Akins, ni mmisionari na amenipatia mtazamo mingi sana kuhusu nguvu ya umisheni. Kwa hiyo, Kunasehemu nyingi a majibu katika hilo:

1) Watu wanaweza kuuharibu ukweli kuhusu Mungu lakini wamisionari wanatoa namna gani ya kuishi maisha ya Kiristo na kuwaelekeza watu kumwona Kristo.

2) Wamisionari huonesha upendo wa Mungu kivitendo (kama vile msaada wa madawa, na vitu mbalimbali, chakula n.k.), na hivyo kuyafanya mataifa yaje kwa Kristo.

3) Wamisionari wanawaonesha watu madhara ya matendo yao.

4) Wamisionari wanalisaidia kanisa kutii utume mkuu ambalo ni kufanya wanafunzi.

5) Wamisionari wanawaeleza watu kuhusu Kristo.

Mstari wa 20: *"Kwasababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana na kufahamika kwa kazi zake yaani uweza wake wa milele na uungu wake hata wasiwe na udhuru."* Mungu huonesha asili ya uungu wake na ubora wake binafsi kwa njia ya uumbaji wake. Vitu vya asili vinatuonesha nini kuhusu Mungu? Ni Mungu mweza, mwnye akili, mamabo,rangi, uzuri na Mungu anayeendesha mambo kwa nguvu. Na kwa kurudi

kwa Kristo, Mungu anaonesha mfano tunaojifunza *upendo* na *msamaha*. **Nguzo za ukweli za ukristo zinzungusha kanuni ya *Upendo* na *Msamaha*.** Ni kwa upendo wa mungu na msamaha kwamba tumepata uzima wa milele. Kufupisha Mungu kajifunua kwa njia ya vitu vya asili (Uumbaji) na mwana wake(Yesu Kristo) ili tuweze kumwamini na kuwa na ushirika naye.

Mistari ya 21-23: *"Kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru bali walipotea katika uzushi wan a mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza wakjinenea kuwa wenye hekima wakapumbazika wakaubadili utukufu wa mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu alye na uharibifu naya ndege na yawanyama nay a vitambaavyo."* Watu ambao wanadai "kuwa wenye busara" wageukie miungu? Miungu inaanza pale watu wanapokataa kile wanachojua kuhusu Mungu. Badala ya kumtazama Mungu ambaye anaweka maisha wanahisi wao ndiyo waumbaji wa ulimwengu.

Kutoka katika mtazamo wa kisaikolojia, wakati mwingine tunajitazama katika vitu vinavyoendana na masiah yetu na matokeo yake vinafanyika kuwa miungu. Miungu yaweza kuwa kuwa ni malengo yetu, ubinafsi wa kutaka pesa, mamlaka, faraja, hata vitu vya dunia. **Kitu chochote kinachochukua nafasi ya Mungu hicho ni sanamu**. Hatuwezi kujifananisha na Mungu japo kwa namna nyingine ni kweli: Tuliumbwa kwa sura yake. Miungu ni pale tunapoweka matarajio yetu kwenye vitu vilivyoumbwa na Mungu. <u>Ibaada ni pale mtazamo wetu wote unakuwa kwa Mungu katika Kristo Yesu.</u>

Hapa kunamaswali machache ya kujiuliza: Ni kitu gani maishani unahisi kwamba bila kuwa nacho huwezi kuishi: gari, Nyumba, akaunti ya benki, n.k.? Una ndoto unayotaka itokee? Je Mungu ni wa kwanza katika maisha yako? Paulo amechanganua namna ya kuangukia katika miungu:

1) Kumkataa Mungu.

2) Kuweka mawazo yako kuhusu Mungu.

3) Kuanguka katika majaribu ya uzinzi, tamaa, shauku, uongo, kuseng'enya.

4) Kukomaa katika kumkataa Mungu na kuwashawishi wengine kufanya hivyo.

Kwa bahati , Wakolosai 3:12-15 inatuonesha namna ya kumwelekea Kristo na kusihi kwa ajili ya Mungu kila siku: **"basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu watakatifu wapendwao jivikeni Moyo wa rehema utu wema unyenyekevu, upole unyenyekevu, mkichukuliana na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake, kama Bwana alivyo wasamehe vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo ndiyo kifungo cha ukamilifu. Na amani ya kristo iamue mioyoni mwenu ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja, tena iweni watu wa shukurani."**

Msatri wa chini ni kwamba tunapaswa kuiga mtazamo wa Kristo: <u>Mungu alitusamehe, Hivyo tunapaswa kuwasamehe wengine.</u> Hata hivyo hatuwezi kufanya kwa nguvu zetu, hivyo tunapaswa kumruhusu Mungu atuongoze katika maisha yentu. Amani ya Kristo iamue ndani ya mioyo yenu – upendo ni jambo la muhimu sana ("kama nitatoa mali yangu na kuwapa maskini na hata kuunguza mwili wangu kwa moto lakini kama sina upendo, mimi si kitu." 1 Korintho 13:3). Tunapaswa kupenda bila kujali tofauti. Upendo siyo hisia, Ni tendo au maamuzi. Unapoishi kwa upendo inapelekea kuwa na amani. **Kumtumaini Kristo inakusaidia kumaliza migogoro na amani yake itatawala maisha yako**. ("Chochote ulichojifunza au kupokea au kusikia kutoka kwangu, au kukiona ndani yangu– Kiweke katika vitendo. Na Mungu wa amani atakuwa na wewe." Wafilipi 4:9).

Mistari ya 24-25: *"Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tama za mioyo yao waufuate uchafu. Hata wakavunjiana heshima miili yao. Kwa maana walibadili kweli ya Mungu kuwa uongo wakaisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya muumba anayehimidiwa milele. Amina."* Mtu anapomkataa Mungu, Mungu huwaacha waidhi kama wanavyotaka. Mungu huwaacha na

kumkabidhi shetani akiwaruhusu wateseke katika asili ya dhambi zao.

Watenda dhambi wote wanapaswa kumtumaini kristo ili waweze kuwa katika njia ya kurejeshwa. Paul states man's underlying wickedness: **Sisi sote tunaugonjwa wa dhambi na tunapojimimina na kujikabidhi kwa Kristo tunakuwa na aibu ya dhambi yetu**. Kadri tunavyosogea katika kutembea na Mungu ndivyo tunaanza kuona dhambi katika maisha yetu. Utambulisho wetu unapaswa kuwa katika kristo na si katika vitu alivyo vifanya Kristo. Wengi wetu tumejitambulisha katika vitu tunavyovifanya. Kama wanaume tunajifanya kuwa sisi katika kazi zetu, familia, marafiki au jumuia yoyote tunayokuwa tumeunganishwa nayo. Ikiwa mtu atakuuliza wewe ni nani au unafanya nini mara nyingi unajieleza kupitia mahusiano uliyonayo kati ya hivi tulivyovitaja. Lakini utambulisho wa kweli uko katika Kristo.

Je maisha bila Mungu yanamanisha Uhuru? Hapa, Uhuru unaweza kuja kama matokeo ya wokovu katika Kisto. Wasiokuwa wakristo huutazama ukiristo kama dini. Dini, kwa wasio wakristo, inamaanisha ni aina nyingine ya sheria na kanuni ambayo mtu anapaswa kuzingatia. Lakini uhuru wa kweli ulionesha pale Kristo alipoyatoa masiha yake ili kwamba tuwekwe huru milele. Nini kinyume cha Uhuru? Utumwa. Hakuna utumwa mbaya kama mtumwa wa dhambi. Watu huamnini uongo ambao hufunika matakwa yao binafsi na imani. Kuwa na makini na kile ulichowekeza katika akili yako juwa kuwa biblia pekee ni kipimo cha ukweli.

Katika nmna ambavyo maisha ya Kikristo yamewekwa katika dunia. Kabla sijawekwa huru kutoka katika ya kale na dhambi zangu lazima niwe "mtumwa" kwa Kristo. Lazima nikabidhi haki zangu, mawazo, ubinafsi kwake kabla ya kupata uhuru wa kweli.

Mistari 26-27*: "Hivyo Mungu aliwacha wafuate tama zao za aibu hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya*

mke ya asili wakawakiana tama, wanaume wakiyateda yasiyopasa wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu waoyaliyo haki yao."

Mungu anampango unaohusisha mahusiano ya jinsia. **Dhambi huharibu matumizi asili ya mpango wa Mungu.** Ushoga umekataliwa (Mambo ya walawi 18:22). Mungu kaweka vigezo hivi, siyo jamii. Kwakuwa jamii zetu zimeruhusu ushoga lakini Mungu bado anakataa. Kama wakristo tumeamuriwa kuchukia dhambi siyo wenye dhambi. Wanaofanya ushoga wanaendeshwa na tama. Kibaya ni nini – Ushoga au kutoka nje ya ndoa? Yote mawili ni kuendeshwa –na tamaa. Mstari wa chini ni kwamba tunatakiwa kujifunza namna ya kuongozwa na roho ili tushinde majaribu na siyo yatushinde. Njia pekee ya kuyashinda ni kuongozwa na roho wa Kristo. Je taweka mahusiano na kristo? Je utatafuta kuwa na mahusiano ya dhati na Kristo?

SURA YA 5

KUCHEMSHA CHURA

Warumi 1:28-32

"Na kama walivyokata kuwa na Mungu katika fahamu zao Mungu aliwaaacha wafuate akili zao zisizofaa wayafanye yasiyowapasa."- Warumi 1:28

Utamaduni katika marekani unabadilika kwa mwendo wa mwanga. Tuko katika kipindi ambaho ni kama tunapika chura: kama utamchkua chura na umweke katika sufuria lililo na maji yanayochemka atafanya nini? Ataruka nje. Lakini vipi kama utamweka katika maji ya uvuguvugu na halafu baadae uachilie joto? Chura atakaa katika sufuria hadi ataungua na kufa. Hiki ndicho kinahotokea katika maadili na maisha ya wamarekani wengi leo hii. Tumepikwa kwa kiwango cha kufa bila hata kujua.

Katika sura iliyopita tumezungumza jinsi mtu anavyoweza kuabudu sanamu na kuacha kumwabudu muumbaji wa vitu. Warumi 1:28-32 inashughulika na maswala mawili yaliyo katika katka jamii yetu leo: ulafi na ubinafsi. Ngoja niweke katika njia tofauti: Watu bnafsi huwa ni watu wenye tamaa. <u>Watu binafsi wamemezwa na uchungu.</u>

Watu binafsi wanakipindi kigumu cha kuwapenda wengine kwa sababu wao wenyewe hawajipendi. Watu binafsi mara zote huwalaumu watu wengine. Watu binafsi hujitawala wenyewe. Watu binafsi wamezungukwa na watu wenye mahitaji kama walivyo. Watu binafsi huwadanganya wengine waweze kutimiza matakwa yao. Watu binafsi mara zote hawasamehe kiasili. Watu binafsi huwa hawana kiasi. Kama sivyo huwa wanajisikia vibaya kutokana na mazingira yao. Watu binafsi hutafuta kusikilizwa; wanaishi katika ulimwengu ambao hutimiza mawazo yao. Hakuna jambo jingine. Watu binafsi ni watu walio katika uhitaji saa zote. Watu binafsi hujijali wao. Jambo la ajabu katika hili ni kwamba huwa hatujioni wenyewe kitu ninachofanya tatizo likuwe kila mara. Ukweli ni kwamba kila mtu ananamna ya ubinafsi

anaopambana nao kila leo. Jambo la kwanza unapaswa kugundua ubnafsi wako mana unakuzuia kuwa mtu kamili katika Kristo.

Ubinafsi wetu unafanya tumchanganye Mungu. Lakini hakuna namna ya kumchanganya Mungu. Tunapojaribu kumweka katika boksi hebu tafakari? Hatoshi. Tunapojaribu kumweka katika sehemu ya siri hebu tafakari? Mungu hawezi kuwa siri. Ili uweze kuishi maisha ya kikristo Mungu anapaswa kuwa katika kila sehemu ya maisha yetu. Wengine wetu tunaogopa kile watu wanaweza kusema; hata hivyo, familia zinazoomba kwa pamoja huwaambukiza watoto wake. Familia wanaosoma Biblia pamoja huwaambukiza watoto wao. Sasa tunajua vijana vijana wanaweza kuacha kidogo lakini watarudi tena katika hali yao ya kawaida. Katika kiini cha jinsi tulivyo wanadamu ni tofauti na ni ubora wa pekee: Sisi sote tuna nafsi. Tunauwezo wa kumpokea au kumkataa Mungu. Ikiwa tutampkea Kristo tunampkokea yeye ni nani na naweza kufanya. Ikiwa tutamkataa, tunakataa roho zetu zawadi yake ya "Milele." Kumkataa kristo kunapelekea kifo cha milele.

Maandko ya Paulo kwa kanisa la Rumi inatupa mtazamo mzuri kwa ulimwengu. Hebu tusome msatri wa 26: "Hivyo Mungu aliwaacha wafuate taaa zao za aibu hata wanawake wao wakabadili matumizi yao ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili." Mapenzi ya Mungu ni kwa mme na mke ni kuacha familia zao na kuwa wamoja kwa njia ya mapenzi (Mwanzo 2:24, Mathayo19:5, Waefeso 5:31). Wakati wowote mwanaume au anakuwa na mapenzi na mwanaume mwingine huyo moja kwa moja anapingana na uumbaji. Kufanya ushoga ni kuleta uchungu, ambayo ni shina la uovu. Na matokeo ya uchungu ni kushtakiwa moyoni, kuharibika kifikira, na msongo wa mawazo. Kile tunachopanda hicho ndicho tunavuna. Ikiwa tutakaa katika mwili tutavuna uharibifu lakini tukipanda katika roho tutavuna uzima wa milele.

Mstari wa 28: *"Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa wafanye yasiyowapasa."* – "akawaacha na akili zao mbaya." Kwa maneno mengine akili inayomkata Kristo hiyo ni akili mbaya isiyofaa. Kitu kibaya kabisa ni kwamba mtu anaweza kufikiri

kwamba anaakili nyingi kuliko Mungu– "Ukaidi." Hii ni namna mbaya ya dhambi inayopelekea katika kujivuna na uangamifu. Ujasiri katika Kristo ni tumaini halisi. Ujasiri katika wewe menyewe unapelekea ubinafsi na ukaidi.

Mistari ya 29-31: *"Wamejawa na ukarimu wa kila namna, uovu na tama na ubaya wamejawa na husuda na uuaji, nabfitina na hadaa watu wa nia mbaya wenye kungenya. Wenye kusingizia wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutakabari, wenye majivuno wenye kutakabari mabaya, wasio watii wazazi wao wasio na ufahamu wenye kuvunja maagano wasiopenda jamaa zao wasio na rehema.."* Hii mistari inatuonesha kwamba kuna hatua katika uovu. Mchakato unaanza na *wazo.* Mambo tunayoyaruhusu katika faamu zetu yanazaa *mitazamo. Mitazamo tunayoianzisha inasababia kuchukua kivitendo. Tunachukua hatua katika mitazamo juu ya kitu. Kuna maelezo 21 yameelezwa na paulo katika mistari hii*:

1) **Kutokuwa na haki:** Kumkataa Kristo.

2) **Uovu:** Kufurahia utendaji wa mabaya.

3) **Tamaa:** Kushauku juu ya vitu, kama mali kwa namna yoyote hadi ipatikane.

4) **Tabia mbaya:** uovu au dhmabi kwa jumla.

5) **Kijicho:** Kuchukia kwa sababu mtu Fulani kapata kile ulichokuwa unakihitaji.

6) **Mauaji:** Kijicho hupelekea mauaji kwa mfano Yusufu na Yesu.

7) **Ugomvi:** Kupigana juu ya vitu kwa mtazamo wa uchungu.

8) **Udanganyifu:** Kumtega mtu badala ya kuwa kweli.

9) **Mawazo:** Kumuwazia mtu vibaya.

10) **Useng'enyaji:** Minong'ono ya maelezo ya uongo.

11) **Umbea:** Minong'ono ya useng'enyaji, minong'ono ya hadharani.

12) **Adui wa Mungu:** Wale waliojawa na nguvu za mapepo na ubinafsi kiasi kwamba wamemkataa kabisa Mungu.

13) **Kujikweza:** Kuamini kuwa wewe ni bora kuliko mwingine.

14) **Ukaidi:** Kujaa mwenyewe badala ya kujawa na Mungu.

15) **Kujivuna:** Kujifanya mzuri kuliko ulivyo.

16) **Wapotoshaji:** wale wanaofurahia kuwaharibu watu wema.

17) **Kutotii wazazi:** Wale wanaoenda kinyume na mpango wa Mungu katika kufuata uongozi wa wazazi.

18) **Kujipumbaza:** Wale wanaokuwa wanakataa kuelewa hawako tayari kupokea yaliyo ya Mungu (Mathayo 15:16).

19) **Kukosa imani:** wasio kuwa kweli kwa Mungu, wanaojifanya wasiwe waaminifu.

20) **Kukosa upendo:** Bila kuwa na vitu vya asili (ilikuwa ni kawaida kwa wapagani kuuwa watoto wasio wahitaji – Ni sawa kabisa na kutoa mimba leo).

21) **Uchungu:** Wasio onesha rehema – wasio na rehema, wasio na moyo wa utu. Kama kwa mfano Msamalia mwema – wezi waliiba pesa na kumpiga yule mtu, lakini makuhani na walawi walimpita. Watatu wote hawa kwa mtazamo wa mungu wako sawa.

Dhambi inazaa dhambi. Kwa neema ya Mungu tu na nguvu na kwa njia ya shauku ya kumuheshimu yeye tunaweza kukua katika katika yeye. Neema ya Mungu huzaa utakatifu. Hatujifanyi watakatifu, lakini kwa kuwa Kristo anaishi ndani yetu utakatifu wake unadhihirika kupitia sisi.

Hakuna njia ya kuishi maisha kamili lakini tunamtumikia Mungu kamilifu. Nimeshagundua kwamba Mungu hatafuti uwezo wangu na wala si kupatikana kwangu bali ni kushindwa kwangu. Ni udhaifu wangu ndiyo anaotafuta. Ninapokuwa dhaifu ninajikataa na kujikabidhi kwake ili niyapate yaliyo yak wake. Umeshoka kusihi maisha ya kikristo? Unahangaika na kuficha dhambi za siri? Umefika wakati uache kutegemea nguvu zako na uanze kutegemea nguvu za Kristo.

SURA YA 6

HAKUNA NAFASI YA KUNYOSHEANA VIDOLE

Warumi 2:1-11

"Kwa hiyo wewe mtu uwaye yote uhukumuye huna udhuru kwa maana katika hayo umuhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale." - Warumi 2:1

Utasema nini ama nitakuuliza swali, "Hukumu ya haki ni nini?" katika sura hii, tutaangalia kwa karibu kile Paulo anachkisema kuhusu hukumu ya haki ya Mungu. Hebu tafakari barua ya Paulo iliposomwa katika kanisa la Rumi … ekila ichwa kilikuwa kinazunguka walipomsikia akiwahukumu wale waabudu sanamu, mashiga, wapotoshaji na watu wa vurugu. Hata hivyo alipoanza ksema nao, "hamna la kujitetea Ninyi ni wabaya," viongozi wa dini walichukia. Hii iliwapiga usoni kabisa.

Hebu tusome mstari wa kwanza 1: *"Kwa hiyo wewe mtu uwaye yote uhukumuye huna udhuru kwa maana katika hayo umuhukumuyo mwingine wajihukumu mwenyewe kwa na hatia; kwa maana wewe uhukumuye unafanya yale yale."* Paulo anasema kwamba halkuna aliye haki anaweza kujiokoa . Pia anasema bila kujali dhambi zako, haijalishi wewe ni muuaji, au mseng'enyaji, unatakiwa kutegemea neema ya Mungu kabisa upate wokovu. Paulo hazungumzii kiwango cha dhambi. Anatuambia kwamba dhambi yoyote inatosha kutuongoza ili tuweze kwenda kumtegemea Kriso. Sote tumetenda dhambi na bila Kristo hakuna njia inayoweza kutufanya kuwekwe huru kutoka katika dhambi.

Dhmabi za nani ni ngumu kuziona? Za kwetu. **Dhambi za nani rahisi kuziona**? Za yeyote yule. Tunapswa kujichunguza kabla hatujawahukumu wengine kwa sababu Mathayo 7:1-2 inasema, "kwa hiyo katika kila kitu, wafanyie wengine kile unachotaka na wewe kufanyiwa, kwa kuwa hili ndilo hitimisho la

sheria na manabii." Mambo yetu ya kibinadamu hujenga swala kukataa ndai yetu. Mara zote tunajaribu kuipanua kweli kuhusu sisi ili toonekane wema kuliko tulivyo. Mabo tunayoyachukia kwa wengine hivyo na sisi tuyachukie yaliyo katika maisha yetu. Kabla hatujamkarahisha mwingine tunapaswa kuyaangalia maisha yetu kwanza. Mtu naye angalia mambo yaw engine aii eyey huwa anamatatizo zaidi. Tunavyowahukumu wengine ndivyo tutakavyohukumiwa.

Mstari wa 2: *"Nasi twajua hukumu ya Mungu niyakweli juu ya wafanyayo hayo."* Hukumu ya Mungu imelalia wapi? Kweli. Kweli inatoka wapi? Yesu alisema, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima." Kwa hiyo, kweli inatoka katika Neno la Mungu na Kristo.

Mstari wa 3: *"Wewe binadamu uhukumuye wale wafanyayo hayo na kutenda hay ohayo mwenyewe je! Wadhani kwamba utajiepusha na hukumu ya Mungu?"* Je tunaweza kusalimika tukiwa tunawasema wengine vibaya halafu tufanye yale yale katika maisha yetu? hapana. Huu mstari unatuambia kwamba hatuwezi kuepuka Hukumu ya Mungu.

Mstari wa 4: *"au waudharau wingi wa neema yake na ustahili wake na uvumilivu wake usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu?"* katika wema wake, Mungu anacheleweshа hukumu yake na muda wote anatupatia Muda wa kutubu. **Mara nyingi tumechanganya uvumilivu wa Mungu na kibali chake**. Tunakosema halafu hatuadhibiwi, tunarudia kufanya tena tukidhani kwamba Mungu anafurahia. Kama Wakrsto tunapaswa kuomba, "Mungu nioneshe dhambi yangu. Zidhihirishe hisia zangu ili nibadilike na kupna." Kile Mungu anachotaka ni kuwa safi kwake. Hatuwezi kuendelea hadi pale tutakapokuwa tumetubu dhambi zetu kwa Bwana na mwokozi. Anatupenda tulivyo na anatuthamini na kutuona tunafaa.

Mstari wa 5: *"bali kwa kadri ya ugumu wako na moyo wako usio na toba wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu."* Ili tuwe huru kutoka katika dhambi zetu tunapaswa kumruhusu Mungu aondoe ukaidi wetu, na mioyo isiyo ya toba. Hukumu inatendaje kazi?

Yohana 12:47-48 says, “na mtu akiyasikia maeno yangu asiyashike mimi simuhukumu maana sikuja ili niuhukumu ulimwengu ili niuokoe ulimwengu. Yeye anikataae mini asiyeyakubali maneno yangu anaye amuhukumuye, neno hili nililolinena ndilo nitakalo muhukumu siku ya mwisho.” Kusudi la ujumbe wa kwanza wa Yesu ilikuwa siyo kuhukumu watu lakini kuwaonesha wapate njia ya kuiona kweli ya wokovu na uzima wa milele. Atakapokuwa amekuja mara ya pili kazi yake itakuwa ni kuhukumu watu jinsi gani waliishi hapaduniani au kama walimfuata au kutokumfuata katika utii. Neno la Mungu linatuambia kwamba wale waliokubali na kutii watafufuliwa katika uzima wa milele (1 Kor 15:51-57). Wale wanaomkataa yesu na kuishi wanavyotaka watakabiliana na hukumu ya milele (Ufunuo 20:11-15).

Mstari wa 6: *“atakaye mlipa kila mtu kwa kadri ya matendo yake.’”* Kila mtu atahukumiwa kwa kadri alivyoishi. Watu wengine wanasema kwamba washirika wengi wa makanisa ni wanafiki. Lakini Mungu anasema kwamba kila mtu atahukumiwa kwa ajili ya matendo yetu. Hatupaswi kuwaangalia wengine kwamba wamekuwa ni wanafiki badala yake tuangalie unafiki ulio ndani yetu na tutafute namna ya kuushughulikia.

Mstari wa 7: *“Wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika watapewa uzima wa milele.”* Paulo anasema wale wanaovumilia na kutafuta mpango wa Mungu watapata uzima wa milele. Anaweka wazi kwamba hatuokolewi kwa matendo mema lakini tunapoyatoa maisha yetu kabisa tunapenda kumfurahisha Mungu na kufanya mapenzi yake. Kwa hiyo, matendo mema ni matokeo ya kile Mungu alichokifanya katika maisha yetu na si njia ya kujipatia neema yake.

Msatri wa 8: *“na wale wenye fitina wasioitii ile kweli bali wakubalio dhuluma watapata hasira na ghadhabu.”* Mbinafsi ni yule anayetaka kutangulia kuliko mwingine kwa gharama za wengine. Watu hawa ghadhabu ya Mungu I dhahiri.

Mistari ya 9-11*: “dhiki na shida juu ya nafsi ya mwanadamu atendaye dhambi myahudi kwanza na myunani pia.*

Bali utukufu na heshima na amani kwa kila mtu atendaye mema myahudi kwanza na myunani pia. Kwa maana hakuna upendeleo kwa Mungu." Waovu watahukumiwa, na wenye haki watapewa taji– Mungu hana hukumu ya upendeleo. Kulingana na maisha unayoishi leo, utahukumiwaje

SURA YA 7

SI KWA KILE UNACHOFIKIRI

Warumi 2:12-16

"Kwa sababu si wale waisikiao sheria walio wenye haki mbele za mungu bali ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki."- Warumi 2:13

- Ni kitu gani kunatuzuia kufanya yaliyo haki? Kwa nini?
- Nini tofauti ya sheria na Neema?
- Sheria inakusaidiaje? Na vipi kuhusu Neema?

Katika tamaduni za leo, watu wengi wenye busara wametengeneza mawazo juu ya Mungu na dini. Mtazamo weetu kwa Mungu unatathimini mtazamo wetu kwa dunia. Sheria za ulimwengu zinabadilika badilika. Mungu anamtumia Paulo kuchanganua kwa ufasaha jinsi Mungu anavyoutazama ulimwengu wetu. Kwa maneno rahisi Paulo anasema mtazamo wa mwanadamu unapaswa kulingana na mtazamo wa Mungu. Huna chumba cha mtazmo wako. Si kwa kile unachofikiri bali ni kwa ajili ya kile Mungu anachofikiri.

Mstari wa 12: *"Kwa kuwa wote waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheia na wote waliokosa wente sheria watahukumiwa kwa sheria."* Watu wamehukumiwa si kwa kile wasichokijua bali kwa kile walichokifanya na wanakijua. 1 Kor 9:19-21 inatuonesha kwamba Paulo Paulo alihusisha uhuru na Adabu: "maana ingawa nimekuwa huru kwa watu wote nalijifanya mtumwa kwa wte ili nipate watu wengin zaidi. Nalikuwa kama myahudi kwa wayahudi ili niwapate wayahudi kwa wale waliokuwa chini ya sheria nalikuwa chini ya sheria (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria) ili niwapate walio chini ya sheria. Kwa wale wasio na shneria nalikuwa kama sina sheria (si kwamba sina sheria mbele za Mungu bali mwenye sheria mbele za Kristo) ili niwapate hao wasio na sheria. Hauwezi kuwa huru na salama katika Kristo wewe mwenyewe, ni vigumu kuwa huru na watu. Swala ni kuwa tayari na kuleta wengine kwa Kristo. Lengo la Petro ilikuwa ni kumtukuza Mungu na kuwaleta watu kwa Kristo. Alikuwa makini ili asije akaangukia katika falsafa au mitazamo ya kisiasa. Alibaki katika mtazamo wa kuwapenda watu kwa ajili ya kristo.

Mstari wa 13: *"Kwa sababu siyo wale waisikiao sheria walio wenye haki mbele za Mungu bali ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki."* Yakobo 1:19-22 inasema, "hayo mnajua ndugu zangu wapenzibasi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia bali si mwepesi wa kusema wala kukasirika. Kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio na kupokea kwa upole neno lililopandwa ndani liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu hali mkijidanganya nafsi zenu. Inasema nini." Mara nyingi, tunaidanganya tunapofikiri kwamba kwakuwa tumesikia ujumbe basi tumetimiza wajibu wetu. Hatua ya kwanza ni kulisikia neno la Mungu na hatua ya pili ni kutenda kama linavyosema. Nini Mungu anatafuta ni utii. Tangazo letu la kuwa haki ni Utii.

Mstari 14-16: *"Kwa maana watu wa mataifa wasio na sheria wafanyapo kwa tabia zao yaliyo ya torati hao wasio na sjeria wamekuwa sheria kwa nafsi zao wenyewe. Hao waioneshao kazi ya torati iliyoandikwa katika mioyo yao dhaminiri yao ikawashuhudia na dhamiri zao na*

mawazo yao wenyewe kwa wenyewe yakiwashtaki au kuwatetea katika siku ile Mungu atakapozihukumu siri za wanadamu sawa sawa na injili yangu kwa kristo Yesu." Kipimo kimekwisha wekwa na kipimo ni Kristo. Ikiwa umesafiri ulimwenguni utapata ushuhufa katika kila jamii na sheria ya Mungu katika mila mbalimbali. Unaweza kusema kwako na kwa Mungu kwamba hukuishi kwa Kiwango chake?

Hatua ya kwanza ya kuingiz katika timu moja ni hali Mungu kutambua una tatizo. Tunapoliona tatizo tulilo nalo twaweza kuja kwa Mungu na kutafuta msamaha. Nguvu ya injili iko katika msamaha. Kushindwa kuwasamehe wengine mwisho wa siku kunazuia kutumiwa na Mungu kwa kiwango anachotaka atukuzawe ndani yetu. Moyo usiosamehe ni ukosefu wa upendo wa Kristo.

SURA YA 8

TUTASIMAMA NA HATIA MBELE ZA MUNGU

Warumi 2:17-24

"Lakini wewe ukiwa unaitwa Myahudi na kuitegemea torati na kujisifu katika Mungu"- Warumi 2:17

Warumi 2:17-24 unakamata ukweli kwamba hata wale walio niwadini hawastahili mbele za Mungu. Matendo huzungumza zaidi ya maneno. Kama tulivoona katika sura chache zilizopita barua ya Paulo imetupatia uelewa mkubwa wa nguvu ya injili.

Aliwatahadharisha mataifa kwamba watawajibika kwa kila tendo chafu na kwamba ghadhabu ya Mungu haiwezi kuzuiliwa. Anasema wale tu waliovumilia kuishi kwa ajili ya bwana na kutafuta utukufu watapokea uzima wa milele.

Msatri wa 17: *"Lakini wewe ukiwa unaitwa Myahudi na kuitegemea torati na kujisifu katika Mungu."* Hapa Paulo anapanua mjadala wake na viongozi wa dini. Hebu fikiri Mtu awe anahubiri wachungaji akisema, "Mnaelekea kubaya na niko hapa kuwaambia kwamba kile mnachokifanya Ysi sahihi"? Paulo anahmiza viongozi wa kanisa kwa sababu wanaufahamu kuhusu Mungu unaotokana na kuyajua maandiko lakini hawayaishi yale wanayoyahubiri. Anawaambia kwamba hii itawafanya washutumiwe moyoni kama watu wa mataifa. Unakumbuka wazo lile tuliloanza nalo katika kitabu hiki? Kila mtu ni zao la jumla ya uzoefu wake. Kila wakati tunapojifunza kuhusu Mungu au kristo tunajukumu la kuwaeleza wengine– Kwa ufahamu tunakuwa na majukumu. Paulo anawaambia viongozi wa dini kwamba wanaufahamu lakini hawawajibiki kwa huo ufahamu.

Msari wa 21: *"basi wewe umfundishaye mwingine je hujifundishi mwenyewe? Wewe uhubirie kwamba mtu asiibe waiba mwenyewe??"* Paulo anasema, "Inahitaji kujifunza sheria mwenyewe – siyo wengine." **Kile tunachokifanya nichamuhimusana kuliko kile tunachokisema**. Ni rahisi kuzungumza mazungumzo lakini watu wa kweli hutembea matembezi bila kumfanya kila mtu ajuwe. Matendo yetu yananguvu kuliko uliko maneno. Viongozi wa kanisa waliijua sheria vizuri lakini walijifunza namna ya kukwepa lakini wakiwahimiza wengine wakati huo . jambo ni hili – Sheria ni kali kuliko mambo ya maadili. Ni mwongozo wa kuishi kulingana na mapenzi yake. Mara nyingi tunatumia utajiri kupima mafanikio lakini shria ni kipimo kinchotuongoza kutii bwana wtu kristo. Tunapotambua kwamba hatuwezi kuishi bila nguvu zake tunatambua kwamba Sheria inatupeleka kwa Kristo.

Mistari ya 22-23: *"Wewe usemaye watu wasizini wazini mwenyewe? Wewe uchukiaye sanamu wateka mahekalu? Wewe ujisifuye katika torati wamvunja Mungu heshima kwa kuivunja torati?"* katika mistri hii Paulo anajaribu kulalia kwa wayahudi kwamba japo ni wa mwili wa Kristo na wateule wake kunazaidi katika sheria si swala la kuijua tu. Kwa namna hiyo hiyo wakristo wengi leo hii wanashatkiwa na mengi ya jinsi hiyo hiyo. Tunaweza kukueleza kwa namna yoyote ya kutokufanya mabaya lakini mshihi Mkristo jinsi ya kuishi maisha ya milele kwa ajili ya Kristo atakautazama kama amemwona bwana Elvis Presley kafufuka. Kwa nini? Kwa sababu mara nyingi tumeangalia mila kana kwamba ni muhimu na sawa na utii nah ii si kitu

kizuri. Si kwasbabu nasema hivyo, lakini ni kwasababu Mungu anasema hivyo. Hakuna namna ya kumopendeza Mungu bila kuwa na mahusiano naye mema. Kuna muunganikano mmja kwa Mungu nao ni Kristo. Kabla hatujajiunganisha tunapaswa kuitambua nguvu ya upendo katika kristo na tutambue kwamba kutambulikana kwetu kwa kweli kuko katika kristo.

Hili hapa jambo la msingi: Ni rhisi kuwaeleza wengine namna ya kuishi maisha yao kuliko kuangalia maisha yetu katika utii sisi wenyewe. Twaweza kusema maneno yote mazuri lakini yanatupelekea kuchukua hatua na kuleta mabadiliko? **Bila mabadiliko, mifano ya tabia imewekwa**. Mungu anatafuta vitu viwili toka kwa wafuasi wake: Wale watakaomruhusu kristo kuishi ndani yao ili waweze kusema maneno ya kweli na kumrushusu kristo kuishi ndani yao ili wayaishi yale wanayoyasema.

Mtsri wa 24: *"'kwa maana jina la Mungu latukanwa katika mataifa yenu kama ilivyoandikwa."* **Ikiwa tunadai kuwa wamoja na Mungu maisha yetu yanahitaji kuonesha jinsi Mungu alivyo .** Tunaposhindwa kumtii Mungu tunamdharaulisha. Kile tunachofanya, tunakokwenda, tunayesema naye na kile tunachokisema– **inaongeza kuonesha jinsi tulivyo.**

Maisha yako yanamuonesha kristo? Ni maeneo gani ya maisha yako unataka uyakabidhi kwa Kriso?

SURA YA 9

UTII NI MUHIMU KULIKO MILA

Warumi 2:25-29

"Maana yeye si muyahudi aliye muyahudi kwa nje tu. Wala tohara si ile ya nje tu katika mwili. Bali yeye ni myahudi aliye muyahudi kwa ndani na tohara niya moyo katika roho si katika andiko;ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu."- 2:28-29

Sura hii inatugonga katika mioyo yetu kwa dini za siku hizi kwasababu kila dini inafuata namna Fulani ya mila. Kwa mfano, moja ya mila iliyofuatwa sana na wayahudi ilikuwa ni kutahiriwa. Nataka hapa upate uda wa kuwaza mila tatu amabzo unafikiri ni muhimu katika kanisa lako. Mila ni kitu chochote kinachofanywa mara kwa mara katika kanisa na nicha muhimu (i.e. mipangilio, ibada ya jumapili, Muziki, utaratibu wa bada, mavazi, meza ya Bwana, n.k.). kwa mistari hii, Paulo anafutilia mbali mawazo yetu kulingana na mila.

> Mstari wa 25: *"kwa maana kutahiriwa kwafaa kama ukiwa ni mtendaji wa sheria lakini ukiwa ni mvunjaji wa sheria kutahiriwa kwakokumekuwa kutokutahiriwa."* Kutahiriwa kunaonesha Agano la Mungu kwa watu wake maalumu. Kutahiriwa ilikuwa ni kwa wayahudi wote wa kiume (Mwanzo 17:9-14). Kulingana na paulo kuwa myahudi au kutahiriwa haikumanisha kitu kama mtu hakutii sheria ya Mungu. Kwa namna nyingine, wamataifa, wasiotahiriwa wanaweza kupokea upendo wa Mungu na kibali kama watatunza mahitaji ya sheria. Paulo anaendela kueleza kwamba Myahudi wa "kweli" ni yule anayempendeza Mungu na si yule aliyetahiriwa (myahudi "kwa nje"), lakini mtu ambaye Moyo wake u sawa na mungu na anamtii (Myahudi "kwa ndani"). Swala ni hili: Mungu anatafuta na anaalika watu wafanye mabadiliko ya ndani ili waweze kuwa ni watu wa kike na kiume kwa nje wakimuruhusu Mungu kuondoa majivuno yote ya mioyo yao.

Mistari ya 28-29: *"Maana yeye si muyahudi aliye muyahudi kwa nje tu. Wala tohara si ile ya nje tu katika mwili. Bali yeye ni myahudi aliye muyahudi kwa ndani na tohara niya moyo katika roho si katika andiko;ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu."* Paulo ansema kwamba mila za kiyahudi za kutahiriwa si kigezo cha kuwa Mkristo. Tunapaswa kumwamini Kristo katika imani ya toba. Anajaribu kuonesha kwamba kila mtu aliye sawa na Mungu na moyo wake u sawa na mungu ni "myahudi wa kweli" anaeleza wazi kwamba kuwa sehemu ya familia ya Mungu inahujsisha mambo ya ndani na si mambo ya nje. Kwa maneno mengine si kwasababu babu yalo ni tajiri na anajina zuri hakufanyi ndiyo ufike mbinguni.

Twende katika wagalatia 3:6-9 ambapo Paulo anatueleza wazi. "Mwangalie Ibrahimu: 'Alimwamini Mungu, na akahesabiwa haki.' Elewa, wale wanaoamini ni wana wa Ibrahimu. Maandiko yaliliona hilo mapema kwamba Mungu atawahesabia haki mataifa na akahubiri injili mapema kwa Ibrahimu: 'mtaifa yatabarikiwa kupitia wewe.' Kwa hiyo wale waio na Imani wamebarikiwa pamoja na ibrahimu, watu wa imani." Unaona viongozi wa wayahudi na mila zao wakakamatika. Hawakulielewa wazo la kwamba mtu anaweza kufanyika muumini bila hata kuwa myahudi kwanza na kufuata mila zao. Lakini pulo anawaambia kwamba tangu mwanzo kwamba mtu hakuokolewa kwa sababu ya sheria bali kwa Imani – "Ibrahimu alimwamini Bwana na akahesabiwa kuw mwenye haki" (Mwanzo. 15:6). Paulo anaonesha kwamba mahusiano

mazuri na Mungu yak kwa njia ya imani, na tumezungumzia hili katika sura ya 3. **Imani ni hali ya kusikia ndani ya moyo na ujasiri wa kusema Mungu ni yeye anayesema kuwa ni yeye na anweza kufanya kile anachesema anaweza kufanya.** Tunapotegemea katika hilo mahusiano yetu na Mungu yanakuwa katika Imani.

Hapa ndipo tunapata nyama na nyanya ya sura hii. Si kwasbabu unawke da kanisani, unaimba kwaya, unasoma Biblia yako, na unafanya masomo yako ya Biblia ya kila juma haimaanishi kwamba ndiyo umeingia katika timu ya Mungu. Kama vile kutahikriwa, hizi "Mila" zote za kanisa hazitustahilishi mbele za Mungu. Mungu anahitaji kujitoa na kutii (Kumb 10:1-6). Anataka atahiri mioyo yetu kwa kuondoa tama za miili yetu na kuweka shauku mpya ya kumpenda na kuyafanya maoenzi yake. Umewahi kujiuliza " Mungu anategemea nini kutoka kwangu?" <u>Mungu anategemea mambo matano kutoka kwa waumini wote:</u>

1) **Kumuheshimu Mungu:** Kumcha yeye. Usimuogope,bali umuheshimu kwa upendo na heshima.

2) **Kumfuata Mungu:** Kuongozwa na uwepo wa Roho wake mtakatifu (kusoma, kuomba, kutafakari, na kukuwa).

3) **Kumpenda Mungu:** Biblia iansema tunaweza kupima upendo wetu kwa utii wetu.

4) **Kumtumikia Mungu:** Kumtumikia Yeye 100% - si jumapili tu. Kutumika inamaanisha kuwa mnyenyekevu na kuwa tayari kuongozwa na Roho wake.

5) **Kumtii Mungu:** Ishi kile unajifunza; Fuata miongozo tuliyopewa na kristo.

Unapokuwa umechanganyikiwa na unajiona kupoteza dira hebu weka haya mambo matano na utaanza kuona amani ya kweli.

SURA YA 10

UAMINIFU WA MUNGU

Warumi 3:1-8

"Lakini ikiwa udhalimu wetu waithibitisha haki ya Mungu tuseme nini je Mungu ni dhalimu aletaye ghadhabu (nasema kwa jinsi ya kibinadamu.)"- Warumi 3:5

Katika sura hii tutaona Paulo anaharibu kujitetea watu wanavyotumia wanapokuwa wametenda dhambi. Kitu cha kufurahisha nyakati za Paulo miaka 2000 iliyopita na leo ni kwamba ahakuna kilichobadilika. Kuna sabau nyingi watu huwa nazo katika kujihesabia haki mbele za mungu lakini ngoja niorodheshe chache:

1) Sidhani kama kuna Mungu, kwa hiyo nafuata ufahamu wangu. (WArumi1:18-32)

2) Mimi si mbaya kama watu wengine. (Warumi 2:1-16)

3) Ninaenda kanisani sina shida. (Warumi 2:17-29)

Kwa hiyo katika sura mbili za Warumi paulo ameeleza jinsi dhambi inavyoharibu maisha ya ila mtu. Swala la msingi ni hili hapa: **hakuna siye na dhambi.** Sisi sote tunapaswa kuikubali kweli hii bila Kristosisi ni wenye dhambi mbele za Mungu. Tunapofikia hatua hii tu tunaweza kuelewa na kupokea zawadi ya wokovu.

Tusome mstari wa kwanza 1: *"basi myahudi anaziada gani? Na kutahiriwa kwafaa nini?"* Hapa Paulo, anaonesha picha nzito. Anasema kwamba sisi sote ni wapagani wa kimataifa, Ubinadamu, na watu wa mataifa waliohukumiwa kwa matendo yetu. Mungu katupatia shria ya kuonesha uovu wote wa mwanadamu kwa ajili ya mtazamo wa hadharani. Je kunatumaini lolote la ulimwengu? Kunatumaininlolote kwa ajili yangu na wewe? Paulo anatuambia lipo.

Hivi ndivyo inavyokuwa: Sheria inatuhukumu kwasbabu hatuwezi kuishi uu ya sheria. Hatuwezi kufuata sheria 100%. Hiyo ni kweli lakini msingi ni huu: Tumaini katika maisha yetu hayako katika sheria. Tumani letu katika maisha liko katika imani katika **Kristo**. Kwa sababu ya upendo wa Mungu kwetu alitupatia Kristo, alipatia Kristo na tumehesabiwa haki katika Yeye. Wewe na mimi tunastahilishwa kwa sabbu ya upendo wa mungu aliouonesha kwa njia ya mwana wake Yesu Kristo. **WTunapata wokovu, si kwa njia ya sheria lakini kwa njia ya imani katika Kristo Yesu**. Hakuna tunaloweza kulifanya kupata wokovu. Tunaweza kukubali kwa imani kama zawadi kutoka moja kwa moja Baba mbinguni.

Msatri wa 2: *"Kwa faa sana kwa kila njia. Kwanza kwakuwa wamekabidhiwa mausia ya Mungu."* Luka 12:48 inasema, "waliopewa zaidi watadaiwa zaidi." Taifa la wayahudi lina faida nyingi:

1) Walikuwa ni wateule wa Mungu.

2) Mungu alichagua Yesu azaliwe kupitia ukoo wao.

3) Walikuwa ni Warithi wa agano na Mungu mwenyewe.

Hata hivyo faida hizi haziwafanyi waonekane kuwa ni watu bora kuliko wengine. Walikuwa na majukumu mengi ya kusihi kulingana na maagizo ya Mungu. Kama wakristo, tunapaswa kuwa makini kutokukumbatia mtazamo ule ule kwa wasio amini . Wakati mwingine tunajiona kuwa na haki kitu kinachopoteza ushuhuda. Kwa maneno makali tunapeleka signo kwa wengine tunapojihesabia haki.

Mistari 5-8: *"Lakini ikiwa udhalimu wetu waithibitisha haki ya Mungu tuseme nini je mUngu ni dhalimu? Aletaye ghadhabu? (Nasema kwa jinsi ya kibinadamu) Hasha! Kwa maana hapo Mungu atawezaje kuuhukumu ulimwengu? Lakiniikiwa kweli ya Mungu imeweza kudhihirishwa utukufu wake kwa sababu ya uongo wangu mbona mimi ningali nahukumiwa kuwa mweye dhambi? Kwa nini tuseme (kama tulivyosingiziwa na kama wengine wanavyokaza kusema ya kwamba twaseha hivyo) natufanye mabaya ili yaje mema? Ambao kuhukumiwa kwao kuna haki.)"* Watu wengi katika makanisa wandhani kwamba kama watasema ndiyo kwa kristo wanaweza kugeuka na kuishi maisha wanayoyataka. Wanadhani kwamba Mungu ni kama shirika la BIMA kwa ajili ya wokovu wao. Baadhi ya watu waovu siku hizi wako makanisani. Kwa nini? Kwa sababu wanatoa maelezo haya:

1) Ni kazi ya Mungu kusamehe.

2) Mungu anaupendo sana hawezi kutuhukumu.

3) Dhambi si mbaya sana. Inatupa uzoefu na kutufundisha nini tusifanye.

4) Si vibaya kuishi kama tamaduni zetu zilivyo.

Kile Paulo anachokisema katika mistari hii ni kwamba, **"haijalishi utajiteteaje, Kila dhambi itaonekana na itashughulikiwa."** Kama tunavyojua, yesu alikuja mara ya kwanza kama mwokozi wetu. Atarudi mara ya pili kama hakimu wetu.

SURA YA 11

HAKUNA MWENYE HAKI BILA KRISTO

Warumi 3:8-20 (Waefeso. 2:1-3)

"basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya Torati ili kila kinywa kifumbwe na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu."- Warumi 3:19

Katika sura ya mwisho tumejadili kwa kina uaminifu wa Mungu na jinsi gani Kristo ni njia pekee ya wokovu. Nataa nianze sura hii na mstri katika maandiko unaokubaliana na mango wa wokovu katika kitabu cha Warumi:

Warumi 3:23	Kila mtu ametenda dhambi – Sisi sote ni wayenda dhambi bila Kristo.
Warumi 6:23	Mshahara wa dhambi ni mauti – Sisi sote tumeandaliwa kwa ajili ya kuzimu bila Kristo.
Warumi 5:8	ysu kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu– alilipa gharaa ili tuwe huru.
Warumi 10:8-10	Kusamehewa dhambin zetu tunatakiwa kuamini na kukiri kuwa yesu ni Bwana. Wokovu unapatikana kwa njia ya Kristo kwa Imani. Ni yesu tu anaweza kuokoa.

Paulo anaanza mstari kwa swali la maana sana , "Sasa vipi, Tunafaa?" Nini Paulo anauliza? Katika sura ya 1 na ya 2 katika Warumi, Paulo anaeleza kwa kina ni kwa jinsi gani ilivyo chukizo pale ushoga, upotoshaji, na lolote nje ya ndoa halali kuwa na mapenzi. Kwa maneno mengine ni dhambi sana. Anaendelea kuwakataliwa wamataifa na halafu viongozi wa wayahudi katika Rumi, Sura 3. Sasa analeta mtazamo kwake yeye mwenyewe na wafuasi wote wa Kikristo. Kile anachokiuliza kwa leo ni, "wewe ni mtu mzuri kuliko wengine?" hili ni swali la msingi sana. Utakavyojibu ndivyo moyo wako uatakavyokuwa. Hapa ndipo kuna tatizo: Wakristo wengi wanamitazamo mibaya juu yao wenyewe. Paulo anatumia hili kama nafasi ya kuwakumbusha kwamba sisi sote tuko katika mizigo ya dhambi mizito. Hakuna jinsi tunaweza kuiepuka dhambi. Si kwasbabu umekuaj kwa yesu ndyo umekuwa bora kuliko wengine. **Ongezeko lako katika haki si kwasababu yako ni kwasababu ya kristo anayeishi ndani yako.**

Hebu tugeukie Waefeso 2:1-3. Mistari ya 1-2: *"nanyi mlikuwa wafu kwasababu ya makosa na dhambi zenu ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu na kwakumfuata mfalemwa uweza wa anga* ***roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi„"*** – **"Roho yuko kazini kwa wale wsiotii."** Nina maswali mawili: Ni roho gani katika mstari huu? Roho anafanya nini? Ngoja nieleze. Kuna roho za aina mbili: Mwovu na mtakatifu. "Mtawala wa anga." Ni roho gani hii? Mwovu. **Roho wote waovu wanaletwa na shetani.** neno "Shetani" linamaanisha nini? **Mshitaki**. Kazi ya kwanza ya shetani ni kukushtaki. Katika waefeso 4:27, anaitwa pia "**Ibilisi**" – **"msimpe Ibilisi nafasi."** Paulo anatoa picha ya shetani kama myawala

wa dunia pamoja na mapepo yake. Shetani ni mtawala wa muda katika dunia hii. Shetani ananguvu zilizo na kikomo. Yesu ni mtawala wa milele na nguvu zake hazina mwisho. Shetani anaweza kushinda vita vingi hapa duniani, **lakini yesu ndiye aliyethibitishwa kushinda vita na kumwangamiza shetani mwishoni.**

Mstari 3*: "ambao zamani sisi sote nasi tulienenda kati yao katika tama za miili yetu tulipoyatiumiza mapenzi ya mwili naya nia tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine."* Pointi ni hii: watu wote wana asili ya dhambi. Kwa maneno mengine, sisi sote tunaugonjwa wa dhambi. Tumeangamia katika dhambi na hakuna a kujiokoa. Je mwanadamu anaweza kufanikiwa bila Mungu? Ndiyo lakini iwango cha Mungu ni muhimu sana. Pauloanatuambia kwamba hakuna mtu anaweza kuwa safi hata aweze kupata wokovu. Ikiwa tutamkataa Kristo tunakuwa Kama mstari wa tatu unavyosema 3, "wana wa ghadhabu." Kwa maneno mengine, ghadhabu ya Mungu itakuwa katika maisha yetu. Hata hivyo tunapopokea zawadi ya uzima wa milele tutaungana na kristo katika maish yake kamili na kuwa safi katika macho ya Mungu.

Ngoja nikuulize swali: Ikiw nitakuap zawadi, nini utatakiwa kufanya? "Kushukuru" – jawabu la kushukuru na kutambua. Wakrito wengi hawashukuru Mungu kwa ajili ya zawadi ya bure ya wokovu. Mara zote wao ndiyo wanataka washughulike kwa ajili ya wokovu. **Tumeokolewa kwa njia ya neema lakini kwa shukrani tunatakiwa kuwatumikia wengine kwa wema, upendo na upole.** Katika ukristo hatuna "Ubinafsi". Unaona Kristo siyo mwokozi wetu kwa ajili ya faida yetu. Tumeokolewa kwa faida yake na kwa ajili ya huduma yake ili uweze kukuza ufalme wake. Hivi ndivyo huwa naangalia: Kila mkristo atahukumiwa kwa kile wanachokisema na kwa kile wanachokifanya, **Kwa hiyo mitazamo yangu ya msingi katika maisha yangu ni kufanya mambo matatu :**

1) **Kumpenda Mungu.**

2) **Kuwapenda watu.**

3) **Kufanya wanafunzi.**

Hivi ni vitu vitatu kila Mrkisto anapaswa kuvikumbatia na kuvifanya kuwa vipaumbele katika maisha yao. Sasa hebu turudio katika Warumi 3:19-20.

Mstari 19: *"basi tajua ya kuwa mamabo yote inenayo torati hyanena kwa ajili yao hao walio chini ya torati ili kila kinywa kifumbwe na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu."* Mstari huu unauliza swali "ni dhambi gani uliyo nayo katika maisha yako inayokuzinga kuwa karibu na Bwana?" Mungu anataka tufanye vitu **vitano**:

1) Njoo ukiwa safi mbele za Mungu. Zikabidhi zambi katika maisha yako.

2) Jitoe kusoma na kukua katika neno la Mungu, biblia, kila siku. Litafakari neno la Mungu.

3) Jitoe kuomba na msihi Mungu kwa msaada na mshukuru kwa kila kila baraka.

4) Ushirika na kundi la waminio watakaokutia moyo na kukuimarisha.

5) Onesha upendo wako kwa wengine kwa njia ya ibada. Fanyika kuwa mikono na miguu ya Kristo.

Nukuu ifuatayo inatoka katika kitabu cha Adrian Rogers, Adrianisms:
- Biblia ni barua ya upendo kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto wake.
- Bblia inaonesha tatizo moja – **dhambi**.
- Biblia inaadui mmoja – **Shetani**.
- Biblia inashujaa mmoja – **Yesu**.
- Bibia inakusudi moja – **Kumtukuza Mungu**.

“Kadri unavyotoa neno la Mungu ndivyo litakavyo kaa kwako.”

“Wangapi wenu mnataka imani zaidi? Ingia katika Neno la Mungu.”

“Inapokuja katika swala la maombi inatakiwa kuwa ni wazo letu la kwanza na si wazo la mwisho.”

“Umewahi kujisemea, ‘Sijisikii kuomba’? kama kuna kipindi unapaswa kuomba ni kile kipindi ambacho haujisikii kuomba. Omba hadi ujisikie unaomba.”

“maisha yako ya kiroho hayawezi kuzidi maisha yako ya maombi.”

“Unapoomba, usimpe Mungu maelekezo, bali wasili kwake kama wajibu.”

“Maomba ni faida kubwa sana ya Mkristo.”

SURA YA 12

HAKI KWA NJIA YA IMANI

Warumi 3:21-26

"Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio maana hakuna tofauti."- Warumi 3:22

Kama tulivyojadili huko nyuma, Paulo aliandika kitabu cha warumi akiwa amekipanga kwa makini akiwakilisha maelezo ya imani kwa kanisa la Rumi. Hata hivyo Paulo aktika barua hii ameitumia kufanya mabo matatu:

1) Kuonesha ukweli wa Injili. (1:3)

2) Kuwatangazia watu wake kujito kwake kuifuata injili. (1:16-17)

3) Kujenga kasha la (upotevu)wa mwanadamu. (1:18-3:20)

Sura hii itafungua sehemu ya nne ya Warumi, amabpo Paulo anawakilisha ahabari njema –ujumbe wa akili. Kwa sura zote kumi na moja zilizopita tumejifunza kwamba watu wote ni watenda dhambi mbele za Mungu. Kila mtu anahitaji wokovu aktikaKristo kwasbabu hakuna anayeweza kuitimiza sheria. Kila mtu anatatizo la dhambi. Paulo katumia sura mbili anatueleza kwamba sisi tunahatia mabele za Mungu kwa sababu ya dhambi zetu . Sasa, Paulo anatupatia habari njema: kuna njia moja wapo ya kuwekwa huru na kuwa bila hatia.

Hebu tusome mstri wa 21: *"Lakini sasa haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria inashuhudiwa na torati na manabii."* – "Nje na Sheria (agano la kale) haki a Mungu imedhihirishwa." Imedhihirishwaje? Kupitia sheria na manabii. Biblia kimsingi imepangwa katika makusudi:

1) Agano la kale linatueleza **kuja kwa Kristo.**

2) Injili nne zinatueleza **kuzaliwa, maisha, kifo na kufufukakwa Kristo**.

3) Nyaraka za Paulo zinaeleza **Jinsi gani ya kuishi kwa ajili ya Kristo.**

4) Kitbu cha ufunuo kinatueleza **kuja kwa Kristo mara ya pili**.

Msatri wa 22: *"Ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo kwa wote waaminio maana hakuna tofauti."* Sisi sote tunahatia mbele za Mungu, lakini Imani katika Kristo inazalisha haki kwa wote waaminio. Tunapomtumainia Kristo atuokoe kutoka katika dhambi zetu inamaana kwamba tunaweka tegemeo letu lote kwake atusamehe dhambi na atuweke sawa na Mungu mtakatifu. **Anataka atubadilishe kwa kutuwezesha tuishi kwa neno lake na kuongozwa na roho Mtakatifu.**

Mstari wa 23: *"Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."* Kila mtu katenda dhambi. Dhambi natusababisha tutengwe na Mungu na inapelekea kwenye kifo cha

kiroho. Hatuwezi kuwa hai kikroho kama hatuna mahusiano na Mungu kwa njia ya Kristo. CKuja safi na dhambi zetu mbele za Mungu ni hitaji tunalotaliwa kuwa nalo kwanza kabla hatujajiunga na timu ya Mungu. Hatua ya kwanza ya imni ni ngumu kwakuwa inahitaji tukiri kwamba hatuwezi kufanya kwa nguvu zetu kuondoa dhambi zilizo katika maisha yetu. Watu walio na utajiri wa vitu inakuwa ni ngumu sana kuona kwamba wako katika uhitaji. Kwa njia hii ni ngumu kwa matajiri kumfuata Kristo (Marko 10:25).

Msatri wa 24: *"wanahesabiwa bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu* "Kuhesabiwa haki?" **Inamaana ya kutangazwa "kutokuwa na hatia."** Kama hakimu akikutangaza kuwa "huna hatia" kinatokea nini? Inakuwa kana kwamba haujawahi kushtakiwa. **Kwa maneno rahisi huu mstari unaamisha kwamba hatuna hatia kwa Neema ya Mungu.** Dhambi zetu zimesafishwa. Inamaanisha nini kukombolewa? **Ukombozi ni pale deni linapokuwa limelipwa.** Neno linatokana na mtu aliyekombolewa kutoka utumwani. Katika agano la kale kama utashindwa kulipa deni lako unachukuliwa utumwani ili ukalipe deni lako. Sheria imetoa hitimisho la ukombozi, ambapo mdhamini analipa deni na kununua uhuru wa mtu. **Mpango wa Munguwa ukombozi kupiti mwana wake yesu Kristo.** Tumehesabiwa haki (Tumetangazwa "hatuna hatia") kwa neema yake (upendeleo wa Mungu ambao hatukustahili) kwa njia ya ukombozi (malipo ya dhambi zetu) ulioletwa na Yesu kristo. Unachotakiwa kukifanya ni kuikubali zawadi ya wokovu na kuamini kwamba Yesu ni Bwana kwa kumwamini, na wokovu unatolewa bure.

Tunaokolewaje? **Ni kwa neema ya Mungu na imani yetu ndani yake inayotuokoa. Hufanya uokoaji.** Waefeso 2:8 Inasema, "Ni kwa neema umeokolewa kwa njia ya imani– nah ii haikutokana na wewe ni karama ya Mungu." Neema ni Nini? **Neema ni kitu hatuwezi kuipata kwa nguvu zetu yaani hatustahili – Ni upendeleo wa Mungu kwetu.** Neema ni kile Mungu anafanya kwa jili yangu. Sheria ni kile ninachokifanya kwa ajili ya Mungu.

Ngoja turudi kwenye kazi ya uokozi inavyofanyika. Fikiri wokovu kwa njia hii: Sijui kuogelea. Niko kwenye mtumbwi na watu nkinatereza na kuanguka kwenye maji marefu na sina vazi la kujiokolea. Nitafanya nini? Jambo la msingi ni kujitahidi kuogelea lakini kitatokea nini? Kiukweli nitazama na kufa maji. Niko katika sehemu isiyo na msaada. Kwa maneno mengine hakuna njia ya kujiokoa. Kadri ninavyojaribu kuogelea ndipo ninazidi kuzama. Ikiwa nitaomba msaada na niamini kwamba mtu aliye katika mtumbwi aanivuta na kunirudisha katika mtumbwi ninaweza kuokoka. Pointi yangu hii hapa: Sisi sote ni watenda dhambi tunazama katika dhambi na hakuna tunachoweza kukifanya ili kujiokoa. Lakini Mungu katupatia Mwokozi ili aweze kututoa katika kifo cha dhambi. Tunachotakiwa kukifanya ni kumwamini. Yohana 5:24 inasema, "anaye yasikia maneno yangu na kuamini anao uzima wa milele. Amepita kutoka mauti na kuingia uzimani."

Nini **uzima wa milele**? **Ni kuishi milele na Mungu.** Kwa sasa tunamkubali yesu kama mwokozi na maisha mapya yanaanza. Kwa njia hii maisha ya milele yanaanza tu pale mtu anapompokea Yesu. Wakristo wengi wanadhani kwamba muumini anapokufa maisha ya milele ndiyo yanaanza Lakini Yohana17:3, iansema, "na huu ndiyo uzima wa milele, kwamba wakujue wewe Mungu wa kweli, na Yesu Kristo uliye mtuma." Neno la Kiyunani "kujua" linamaanisha "kuwa na mahusiano ya ndani na." Kwa hiyo tunapokuwa na mahusiano ya kina na Mungu katika kristo tunkuwa na uzima wa milele. Tunapompokea Kristo Inakuwa ni biashara

iliyokamilika. Kifo cha mwili kitakuwepo hadi pale Kristo atakaporudi. Miili yetu itakufa roho zetu zitafufuliwa na kuishi milele Kristo atakaporudi. 1 Kor 1:15 inasema, “hakuna mtu atakayesema ulibatizswa katika jina langu.”

Mtsri wa 25*: “ambaye Mungu amekwish kumweka awe upatanisho katika damu yake ili aoneshe haki yake kwa sabau ya kuziachilia katika ustahimili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa.”* **Kristo ni “dhabihu ya upatanisho”** Kwa maneno mengine likfankwa niaba yetu kwa ajili ya dhambi zetu. Mungu alitangaza kifo cha Kristo kuwa ni dhabihu kamili na iliyostahilikwa ajili ya dhambi zetu. Dhambi zetu zimekwisha kwa sababu ya dhabihu yake iliyoleta ukombozi na uhuru kwetu na si kwa njia nyingine. Ni matumaini utajifunza neno hili katika sura hii mara nyingi ili upate kujua urahisi lakini wazo la msingi la mafundisho ya wokovu. Upendo wa Kristo unapatikana katika haki yake.

SURA YA 13

KUHESABIWA HAKI KWA NJIA YA IMANI

Warumi 3:27-31

"Basi twaona kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria." - Warumi 3:28

Tumegundua katika sura iliyopita maana ya neno: **Neema** – Upendeleo wa Mungu. Huwezi kuifanyia kazi. Neema ni kile Mungu anachonifanyia. **Ukombozi** – Gharama imelipwa ili tiwe huru. **Kuhesabiwa haki** – Tunapotangazwa "Kutokuwa na hatia" mbele za Mungu. **Kafara** – Pale kristo alipokufa kwa niaba yetu. Lakini pia tumejifunza kwamba asili yote ya mwanadamu haina haki mbele za Mungu. Kwa hiyo kitu pekee ambacho Mungu anaweza kufanya kukamilisha vigezo vyake vya haki ilikuwa ni kumtoa mwanawake kama dhabihu kwa wanadamu wote. Ikiwa tutasema kwa Mungu kwa imani, "Mungu ninaamini umesema wewe ndiye uliye sema ndiye na unaweza kufanya kile unachosema unaweza kufanya," tunatambua sasa ni nani ambaye ni mwenye haki. Ni Mungu. Tunapoamini kabisa Mungu anatuweka huru kutoka katka mateso ya dhambi. Kila mtu anabeba mzigo ambao unakuwa na uzito katika kipindi Fulani katika maisha yake – mahusiano mabaya na familia au marafiki, kupoteza kazi, mihadarati, pombe, majivuno, tatizo la pesa, na mengine mengi. **Bila kujali wewe ni nani, kila mtu anamatatizo yake, katika nyakati Fulani huonekana kuwa kubwa kiasi kwamba huwezi kulibeba.**

Hili somo linahusika na kuhesabiwa haki kwa imani. Kuhesbiwa haki maana yake ni kutangazwa "kutokuwa na hatia" kwa imani, kushukuru kwamba mopango wa Mungu wa wokovu ni pekee unaoweza kutuokoa. haya, ngoja tuigawanye. Je dhabihu ilihitajika? Ndiyo. Na nani? Mungu. Kwa nini Mungu? Kwa sabau ndiye pekee anayeweza kuanzisha dhabihu. **Unaoba, mwanzilishi wa dhabihu ni yule ambaye anaweza kumtangaza mwenye dhambi "Kuwa hana hatia" au kuhesabiwa haki katika Kristo.**

Tusome mstari wa 27: *"Ku wapi basi kujisifu?kumefungiwa nje. Kwa sheria ya namna gani?kwa sheria ya matendo?la bali kwa sheria ya imani."* Hapa Paulo nasema, "Ikiwa nitakupatia awadi hwezi kujivuna kwa sababu ya kuipokea zawadi unachotakiwa kusema ni "Asante.'" **Imani ni kusema ndiyo kwa ajili ya zawadi ya Mungu ya ukombozi na kutangazwa "Kutokuwa na hatia," inayoleta uhuru.** Kwa kusema ndiyo tunasema, "Mungu ninakuamini. Ninaamini unaweza kufanya kile unachosema unaweza kufanya na ninaamini kwamba wewe ndiye unayesema kuwa ndiye." Imani ni pale tunapoamini kweli Mungu ni halisi. Hapa kuna swali: kabisa unaamini Mungu ni halisi? Kama hauamini nataka nkupe kazi ya kuanza kuchunguza ili ugundue Mungu ni halisi, si kwasbabu nimesema ni halisi bali ni kwasbabu utaona jinsi alivyo katika maisha yako not because I say He is real, but because you experience who He really is in your own life. **Hautaweza kumfahamu Mungu hadi pale utakapokubali kuwa katika mahusiano naye.**

Mstari 28: *"Basi twaina ya kuwa mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matend ya sheria."* Uongo mkubwa katika ulimwengu uliofanywa na dini nyingi ni kwamba kwa kufanya vitu kadhaa mwanadamu anaweza kukubaliwa na Mungu. Sasa ikiwa ni matendo yanayotuokoa ni nini basi kinachotuokoa? Paulo anasema kwamba tumetangazwa "Kutokuwa na

hatia" tunapokubali uhuru wa kutoka katika dhambi maana Mungu ndiye aliyetupatia kwa njia ya Kristo. Hebu tuangalie vitu ambavyo haviwezi kutuokoa:

1) **Maadili**: Mtu aliye nje ya maadili mara nyingi hujipenda mwenyewe na maadili yake ni kwa ajili ya kujijali mwenyewe. Eti kwa sababu mtu ni "Mtu mzuri" katika macho ya watu lakini mbele za Mungu "Si mzuri"; Sisi **sote** ni watenda dhambi, haijalishi ni mzuri kiasi gani, mwema, mtoaji, mstaarabu n.k. tunaweza kufikiri kwamba tuko hiyo.

2) **Ufahamu wa Biblia**: kama viongozi wa kiyahudi tunaweza kufahamu kuhusu Mungu na kujifunza Biblia au maish ayote lakini kama hatuzieshimu kweli za Biblia na kuiishi imani hatwezi na hatutaokoka.

3) **Kwenda kanisani:** watu wengi wnadhani kwamba wakitimiza jukumu lao la juma la kuhudhulia kanisani Mungu atawapatia kibali cha bure cha kuingia mbinguni.

4) **Huduma yenye nguvu:** Yuda alikuwa mtedaji mzuri, lakini ndiye aliyemsaliti Yesu. Kwenda katika safari za kimisionari, masomo ya Bibliana misaada mingine ya kibinadamu haiwezi kukuokoa.

5) **Kushitakiwa dhambi katika maisha yako:** Kuacha maisha yetu ya dhambi si uthibitisho wa imani iokowayo. Tunaweza kuacha dhambi kwa nguvu zetu, lakini asipowekwa yesu hapo dhambi zingine zinaweza kujitokeza katika maisha yetu bale shetani ataona kuna utupu.

6) **Uhakima wa wokovu:** Eti kwa sababu tunahisi kama tumeokoka itufanye tuokoke? hapana. Biblia imetutahadhalisha juu ya watu wnaojifanya wameokoka kumbe bado. (Yakobo 1:22)

7) **Uzoefu wa maamuzi yaliyopita:** Ikiwa hakuna uthubitisho wa maisha ya kimungu sasa basi unapaswa kujihoji kama kweli uliokoka. Haijalishi ulifanya maamuzi gani magumu huko nyuma hicho si thibitisho la wokovu wako kama bado unamuasi Mungu.

Uthibitisho wa Kwamba Umeokoka:

1) **Kumpenda Mungu:** mtu aliye na imani iokowayo mara zote atampenda Mungu. (Warumi 8:7)

2) **Kutubu na kuchukia dhambi:** Mtu anayemoenda Mungu atakuwa na roho ya kuchukia dhambi. Toba yak we,I kukiri na kabisa unageuka kutoka katika dhambi. Mungu anapoyagusa maisha yetu mioyo yetu inaugua kwa ajili ya dhmbi zetu. Kama tutatenda dhambi halafu hatuumii hiyo inamaana hatujabadilika bado.

3) **Kuwa na unyenyekevu wa kweli:** Mtu hawezi kuokoka kama anajitegemea mwenyewe na kujiinua.

4) **Kujitoa kwa ajili ya utukufu wa Mungu:** Paulo anasema katika wafilipi 1:20-21, “Kama vile nilivyotazamia sana na kutumaini kwamba sitaaibika kamwe bali kwa uthabiti wake kama siku zote na sasavivyo hivyo kristo ataadhimishwa katika mwili wanguikiwa kwa maisha yangu au kwa mauti yangu. Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo na kufa ni faida.” Majivuno hutusababisha tutake kutambuliwa na kujitukuza, lakini tunapasw kuelewa kwamba kila kitu tulicho nacho katika maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu. Anapaswa kupokea utukufu **wote** na siyo sisi.

5) **Imani ni maombi:** Moyo wa muumini wa kweli utalia kwa mungu kwa ajili ya maombi.

6) **Upendo usio na ubinafsi:** Muumini wa kweli hutanguliza wengine kwanza kabla yake. Mtu ambaye hapendi wengine si Mkristo. Kama mtu hawezi kujipenda wmenyewe ni ngumu kupenda wengine. Mfano wa mtu asiye na ubinafsi ni Kristo Mathayo 20:28 inatuambia, “kama vile mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa bali kutumika na kuyatoa maisha yakekuwa sadaya kwa ajili ya wengi.”

7) **Kutengwa na ulimwengu:** Yohana 17:15-18 inasema, “Ikiwa mtu ataupenda ulimwengu upendo wa baba haumo ndani yake.” Japo tunaishi katika ulimwengu hatupaswi kuwa wa ulimwengu huu. Tunapaswa kuangalia mambo ya mbinguni, vitu vya milele, na si mambo ya dunia hii.

8) **Ukuaji wa Kiroho:** hatupaswi kudumaa. Tunapaswa kujua kwamba maisha ya kiroho yako ndani yetu na yanatakiwa kukua, tunapoendeleza tumaini la ndani na kumtegemea Mungu.

9) **Maisha ya utii:** Tukiliishi neno la Mungu na kujiruhusu kuwa ni makao yake tutafurahia kuishi maisha yasiyo na mwisho huku tukikumbatia imani iokowayo ya kristo.

Tunatakiwa kujua kwamba kuishi maisha ya kung’ang’ana yatatupelekea kuchanganyikiwa na kushindwa. Hatuhesabiwi haki kwa sababu ya kile tunachokifanya. Kuhesabiwa haki kumefanyika katika sehemu ya Mungu. Hatuwezi kijitangaza wenyewe “hatuna hatia.” Hakuna unachoweza kukifanya ili kuzuia usiwe na hatia kwa dhambi ulizozifanya labda uipokee zawadi ya bure ya wokovu kwa imani. Tendo hili linapotokea tunajawa na Neema. Kwa nini? Kwa sabau tunapokea kitu ambacho hatujakifanyia kazi, na wala hatukukistahili kutoka kwa Mungu Mtakatifu.

SURA YA 14

IBRAHAMU: ALIHESABIWA HAKI KWA IMANI

Warumi 4:1-12

"maana maandiko yanasemaje? Ibrahimu alimwamini Mng ikhesabiwa kwake kuwa ni haki. Lakini kwa mt afanyaye kazi jira wake hauhesabiwi kuwa ni neema bali kuw ni deni. Lakini kwa mt asiyefanya kzi bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki yeye asiyekuwa mtauwa imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki."
- Warumi 4:3-5

Paulo alikuwa anajuwa kwamba Warumi walikuwa wanajua kuhusu historia ya wayahudi. Kwa hiyo katika sehemu hii ya bara yake kwa hiyo anawaonesha Ibrahimu Baba wa wayahudi/Imani ya kikristo. Wayahdi walijisikia vizuri kuitwa wana wa Ibrahimu Kwa hiyo Paulo anamtumia Ibrahimu kama mfano wa mtu aliyeokoklewa kwa imani. Hapa kuna swali: Je tabiwa njema ya Ibrahimu na matendo mema yalimuokoa Ibrahimu au aliokolewa kwa Imani? Kama kunasehem ya Biblia iliyobadilishwa na kurekebishwa ni sehemu ya Mafundisho ya Wokovu. Ikiwa shetani anaweza kutfanya tuchanganikiwe katika sehemu hii ya Biblia ujue kafal kutuweka chini ya sheria yake. Kila dini katika ulimwengu imejengwa katika namna Fulani ya wokovu juu ya matendo. Kwa maneno mengine, napaswa kufanya jambo Fulani ili kumlipa Mungu aweze kukupa Wokovu. Hii inaharibu mafndisho ya Biblia juu ya wokovu.

Paulo anaeleza sura yote ya nne ya warumi juu ya Ibrahimu ili kueleza pointi ya kwamba mwanadam anaweza kuwa sawa na Mungu kwa Njia ya **Imani** katika kupata neema yake na si kwa **Matendo**. Paulo anatumia Ibrahimu kwa sababu: Halikuwa ni mwanadamu lakini aliheshimika na Wayahudi wote. Mpaka hapa Paulo anakuwa ameeleza Theologia ya kweli wa wokovu. Kwa mtumia Ibrahimu anatupatia mfano ulio wazi, damu na nyama. Ibrahimu alikuwa ni mfano mzuri wa mfano wa Biblia wa Imani ya kweli kwa wayahudi. Wayahdi wengi waliamini kwamba alinganishwa na Mungu kwa sabab ya maisha yake ya Haki. Walimtazama kama mwanadamu asiye na makosa. Kwa namna ya kwamba walimfanya kuwa Mungu mtu. Kwa hiyo Paulo anapofundisha kwamba matebdo ya Ibrahimu haki na hata utii havikumuhesabia haki anaharibu msingi wa imani ya wayahaudi wote. Ikiwa kutunza sheria hakukumhesabia Ibrahimu haki kwa hiyo wao wanatumaini gani? Hata hivyo inasema kwamba ikiwa Ibrahimu hakutangazwa kuwa"hana hatia" bali ilitegemea imani yake kwa Mungu hivyo kila mt anapaswa kuokolewa kwa njia hiyo hiyo. Paulo anarudia tena: analeta mchezo wa mpira kwamba inayokuwa imemshinda mwenzake. Anawamaliza Wayahudi katika mabishano yao.

Mstari 1-2: *"Basi tuesemeje juu ya Ibrahimu Baba yetu kwa jinsi ya mwili? Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa ajili ya metendo yake analo la kujisifia lakini si mbele za Mungu."* Hapa ndipo Paulo anaposema: Kwa sababau tunakubaliana kwamba Ibrahimu ni mfano mzuri wa mtu aliyehesabiwa haki (alitangazwa "hana hatia") katika macho ya Mungu, kwa nini tusimtazame kwa makini ili tupate msingi wa wokovu wake? Paulo anatuonesha kwamba maandiko yanatuonesha kwamba Ibrahimu aliokolewa kwa Imani yake katika Mungu pekee. "Kwa jinsi ya Mwili" inaeleza mambo ya ukoo. Pia inahusika na juhudi za mwanadamu. Ikiwa tutatangazwa kwamba "Hatuna hatia" mbele za Mungu kwa sababu ya jhudi zetu kwa hiyo tungejisifu sana kwa sababu ya "mambo mazuri" tunayoyafanya. Lakini Paulo anasema kwamba

hatuna la kujivunia mabele za Mungu. Hii inatuleta kwamba hakuna nayetakiwa kujiona Bora kuliko mwenzake kwa sababu kujivuna kwetu si kwa ajili ya kazi zetu bali kwa ajili ya kazi za Mungu.

Mstari 3-5: *"Maana maandiko yanasemaje? Ibrahimu alimwamini Mng ikhesabiwa kwake kuwa ni haki. Lakini kwa mt afanyaye kazi jira wake hauhesabiwi kuwa ni neema bali kuw ni deni. Lakini kwa mt asiyefanya kazi bali anamwamini yeye ambaye amhesabia haki yeye asiyekuwa mtauwa imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki."* – "Ibrahamu alimwamini Mungu, na akahesabiwa haki ." Kuhesabiwa haki haina maana ya kumfanya Mtu awe haki. Ina maanisha kwamba tunapokuwa na Imani katika Mungu, Tunatangazwa "Hatuna hatia" na anatuhudumia kana kwamba wenye haki. Kanuni ya "kuhesabiwa haki kwa imani" inakaa katika msingi kwamba Mungu kaweka haki kwa wasio haki kama zawadi. Hatuwezi kufanyia kazi wokovu. Bali umetolewa bure tunapoweka imani yetu na tumaini katika kifo cha mateso ya Yesu kristo. Tunafahamu Kwamba Imani ni kuamini kwamba Mungu ni yeye anayesema kwamba ndiye na anaweza kufanya yale anayosema anaweza kufanya. Imani yetu inaruhusu tupokee zawadi ya bure ya uzima wa milele.

Mstari 6-8: *"Kama vile Daudi aunenavyo uheri mt Yule ambaye Mngu amuhesabia kuwa na haki pasipo matendo. Heri waliosamehewa makosa yao na waliositiriwa dhambi zao. Heri mtu Yule ambaye Bwana hamhesabii dhambi.'"* Tunaweza kufanya nini ili tuachane na kushtakiwa? Msamaha huondoa kushtakiwa na furaha hupatikana tunapokuwa:

1) Tukiri dhambi zet mbele za Mungu.

2) Kumuomba Mungu atusamehe.

3) Tuachane na kushtakiwa na tumtumainie Mungu kwamba ametusamehe.

4) Msamaha unatuweka huru. Dhambi zilizoungamwa ni dhambi zilizosamehewa.

1 Yohana 1:9 inasema, "Tukiziungama dhambi zetu yeye ni mwaminif na wa haki atatusamehe na kutuondolea udhalimu wote."

SURA YA15

HAKI HUJA KWA IMANI

Warumi 4:13-17

"Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa Ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa Imani." - Warumi 4:13

Katika sura iliyopita tmejifnza kile Paulo anatuambia katika Warumi 4:3, "Ibrahimu aliwamini Mungu na akahesabiwa haki." Heb twende katika wagalatia 3:2: "Nataka nijifunze kitu kimoja kutoka kwenu: Je mlimpokea Roho kwa sheria au kwa kuamini kile mlichosikia?" Kile anachokiuliza ni: Tunampokea roho wa Mungu aktika maisha yetu kwa sababu tnafanya matendo mema, kwenda kanisani, kusoma masomo ya jmapili, kuwasaidia wazee kukatisha barabara au kuimba kwaya? Hebu tafakari. Je mamabo hayo yanaweza kutufanya tumpokee Roho wa Mungu katika maisha yetu? Hapana. Lakini vipi kama kweli tukimwamini Mungu? Hicho ndicho Ibrahimu alifanya. Alimwamini Mungu, Upendo wake, Nguvu zake, zuri wake, Neema yake, na Rehema zake. Tnapokea Roho ya Mngu tunapomwamini Yesu Kristo. Roho yake ndiyo njia ya Kutuunganisha na Mungu. Roho wake anatuongoza na kutuelekeza kila inapoitwa leo.

Hapa katika Wagalatia, **Paulo anajaribu kutuambia juhudi za wanadamu hazina mchango katika swala la wokovu.** Katika kanisa la Galatia washirika wengi wa kanisa walikuwa ni mashahidi wa jinsi watu walivyookoka katika maisha yao. Walimpokea roho Mtakatifu na wakajua kwamba si kwasbabau wamefanya jambo ila tu waliamini Mungu katika Kristo na sasa wakawa wamebadilishwa. Lakini walirudi nyuma walipokazia sheria za kiyahudi. Mara zote waumini wapya hufanya hayo. Wanaangukia katika mitego ya mila na tamaduni. Aina za Muziki, aina za kuabudu, meza ya Bwana, na amambo mengine wakati mwingine yamechukua nafas ya ibaada kuliko kuelekea kwa Yesu. Ninapenda kile Rick Warren alisema mwanzoni mwa kitabu chake, Kusudi linaloongoza maisha: "Ni kwa ajili yangu bali kwa ajili ya Mungu." Maelezo hayo yalibadili mtazamo wangu wa mwenendo wa imani ktika Bwana. Ilinileta katika kina cha uelewa cha ktambua mimi ni nani katika Kristo.

Tunapaswa kuelewa mambo muhimu sana kwamba ukuaji wa kiroho unatokea tunapomuruhusu Kristo kuongoza maisha yetu. Tunapomruhusu Kristo huwa anafanya mabadiliko. **Kanuni ngumu kuielewa ni kwamba si kwa jinsi gani tunavyotenda bali ni kwakiwango gani tunamuruhrusu atende ndani yetu .** katika dnia ya leo ni rahisi kukamatika katika kufanya juhudi zetu ili tutimize matakwa yetu. Tunahisi kana kwamba kuna jambo la zaidi sana zaidi ya hili. Kwetu kuamini na kuwa na imani katika Kristo tunaona ni rahisi sana. Funguo ya maendeleo ya uzima katika Kristo ni kuamini na usiruhusu kitu kingine kuingilia mwenendo wako na Yesu. Njia pekee ya sisi kuishi kwa ajili ya Mungu ni kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Kawaida ya binadamu ni kufanya mambo yale tunayoona yanafurahisha. Wakati mwingine tunaona kwamba mtu anapokuwa hana furaha tunaona kwamba anajambo Fulani baya kiroho. Siku moja nilikuwa nikicheza Gofu na mwalimu wangu alikuwa akiangalia na alikuwa akinipa maelekezo. Nilipiga mpira mara nyingi sana vizuri lakini ikatokea nikakosea kupiga mpira ndani ya yadi 30 kaibu na nilipotakiwa kuuingiza. Niliangalia nikamuuliza mwalimu wangu, "Nini kimesababisha?" Akasema, "Hebu tuache kwanza. Nataka kuzungumza nawe kitu

cha mhimu sana. Ukikosea mara moja usiulize, " Nimekosea wapi?" nataka ubadili namna ya kufikiri na iwe, 'Ngoja nipige mpira kama ambavyo nimekuwa nikiupiga.' Kwa maneno mengine, nataka uendelee kufanya mamabo yale nimekuwa nikikufundisha na ukikosea rudia tena mpaka upatie. Usikalie makosa tu." Wakati mwingine katika maisha yetu ya kiroho tunafanya vitu kama hivi. Muda mwingi tunaangalia mizigo yetu hali Yesu anataka tumwangalie yeye. Petro anatpa mfano butu wa kanuni hii wa kumwangalia Yesu aliposhuka katika mtumbwi na kumfuata Yesu akitembea juu ya maji. Kwa nini alizama? Aliacha kumwangalia Yesu Kristo.

Tusome Mistari ya 13-15: *"Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa Ulimwengu aipewa Ibrahimu na uzao wake si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani Maana ikiwa wale wa sheria ndiyo wairthi imani imekuwa bure na ahadi imebatilika. Kwasbabau sheria ndiyo ifanyayo hasira maana pasipokuwapo sheria hapana kosa."* Paulo anasema kwamba Mkristo anazaliwa tena si kwasbabu ya sheria bali kwa njia ya Imani katika Kristo. Hebu turudi katika Kitabu cha mwanzo kidogo. Ibrahimu alipewa agano kutoka kwa Mungu alipokuwa na umri wa miaka 75 (Mwanzo 12:1-4). Ibrahimu akatangazwa kuwa mwenye haki Abraham was declared righteou (Mwanzo 15:6). Akatahiriwa akiwa na umri wa miaka 99 (Mwanzo 17:1-14). Sasa pointi hii hapa: Ibrahimu alikuwa na imani katika Mungu kwa miaka 24 hata kabla hajatahiriwa. Kwa nini? Ujumbe ni kwamba kila mt duniani ananafasi ya kuwekwa na Mungu sawa kwa njia ya imani pekee, si kwasababu tunafuata taratibu sana. Sheria na ibaada ni kumbukumbu ya imani yetu. Zinatutia moyo na kutuinua kiroho, lakini hazitupatii wokovu wowote mbele za Mungu. Je kunakitu chochote maishani mwako umekitanguliza kuliko hata Mungu?

Kufuata tamaduni ni alama ya nje ya imani yetu ya ndani ya nguvu yake iokowayo. Tamaduni za Biblia ni nzuri. Mungu alitupatia mila kwa makusudi pekee ya kumwangalia yeye. Mara zote tunafuata mila na kumwacha yeye. Hili linapotokea inamaana tunakuwa tumetanguliza vitu Mungu alivyoviumba na kumwacha yeye. Mtazamo wa imani yet unapswa kuwa Kristo na tendo lake la kuokoa, na katika matendo yetu yanayoweza kutuokoa. Wakati mwingine watu kanisani huinuliwa zaidi hata ya Yesu. Mara zote hwainua watu kwa kile wanachokifanya. Si vibaya kuwapongeza watu kwa juhudi zao lakini mtazamo wa Imani yetu unapaswa kuwa kwa Yesu. **Tumeokolewa kwa Imani na kwa neema ya Mungu aliye hai katika Kristo.** Kumpenda Mungu hakutuokoi, Kutenda mema hakutuokoi, na hata kufanya mema ujumlishie na imani hauwezi kuokoka bali ni Imani peke yake. Kuwa na Imani na kumwamini Kristo na kumtumainia kutusamehe dhambi ndicho tunachokihitaji.

Kwa hiyo ikiwa hii ndiyo kweli, kwa nini tuwe na sheria? Nini kusudi la sheria? Hebu twende kwenye wagalatia 3:24: "Sheria iliwekwa ili ituelekeze kwa Kristo ili tuhesabiwe haki kwa imani." Sheria inatuonesha ni kwa jinsi gani tulivyo wabaya bila Kristo Hatuwezi kuikamilisha sheria Kwa hiyo sheria ni alama ya kutuambia kuwa tunahitaji msaada. Ikiwa hakuna njia tunaweza kuiishi sheria na kama tutahukumiwa jehanamu kama tutakosea tunapaswa kufanya nini? Hapa ndipo tunamruhusu Mungu awe Mungu. Ninamaanisha nini kwa kusema hili?

<u>Tukimruhusu Mungu awe Mungu tunamruhusu afanye kwa ajili yetu yale tusiyoweza kyafanya wenyewe.</u> Hatuwezi kuishi juu ya sheria hivyo hatuna msaada bila Mungu. Hatuwezi kujiokoa na hapa ndipi mwana wake yesu anakuja. Wakati mwingine tumetambua

tunavyoshughuika, na mara zote tunakuwa hatuna msaada wa Mungu. Matendo yanaambatana na juhudi. Katika taswira hii ya Mungu na sisi nani anafanya kazi? Ni Mungu. Tafakari juu ya mfano huu: mabarabara ya majimbo makubwa huwa yana magari mwengi yanayovuta matela Kwa mfano huu gari ni la nani na tela ni la nani? Mungu ni Lori Kwa nini awe ni roli? Yeye ni roli kwasbabau anatuvuta. Tela ni nani? Sisi ni matela kwasbabau tunamfuata. Swali langu linalofuata: Kwa umbali gani tunaweza kwenda tukijifanya kuvuta Lori kama sisi ni tela? Hatuwezi kwenda popote. Umewahi kuona malori mangapi yanavutwa na tela? Hapana bado. Kwa nini? Ni kwasababu ni kitu kisichowezekana. Kanuni ya msingi ya kiristo ni kutambua kwamba sisi ni tela na Mungu ni Lori na kazi yetu ni kufuata Lori linakokwenda. Kitatokea nini kama tela litaama kuvuta Lori? Litavunjika.

Wakristo wengi hawaelewi kanni hii na matokeo yake wamekuwa wakijaribu kuvuta Lori na kuyaweka maisha yao hatarini. Ikiwa umekuwa ukifanya haya ni wakati wa kuacha na umuruhusu Yesu awe Bwana wa maisha yako.

SURA YA 16

KAA UKIMTAZAMA MUNGU

Warumi 4:18-25

"Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini bali alitiwa nguvu kwa imani aimtukuza Mungu."
- Warumi 4:20

Sura hii itahitimisha Warumi 4 ambayo kwa kweli inazungumzia mambo ya Ibrahimu na imani yake. Ikiwa tutaangalia kwa makini katika mistari hii michache tutaona kwamba kielelezo cha Ibrahimu Paulo ametumia ni mfano mama katika agano la kale kwa imani iokowayo. Paulo anatupa picha iliyowazi inayohitaji imani ya mtu na neema ya Mungu kabla ya wokovu haujakamilika. Waefeso 2:8-10a inasema, "Umeokolewa kwa neema kwa njia ya imani ambayo haikutokana na nafsi yako bali ni karama ya Mungu na si kwa matendo ili mtu aisje akajisifu. Maana tu kazi yake."

Jina halisi la Ibrahimu alikuwa ni Abram likiwa na maana ya "Baba wa wengi" (Mwanzo 12:1-2). Mung alimwita Abram katika Agano na akamwambia kwamba uzao wake utakuwa ni mwingi kama nyota za mbinguni. Hebu tufikiri hili kidogo. Alikuwa na miaka 75 Mungu alipomwambia haya. Abramu alikuwa ni mtu tajiri aliyekuwa kamuoa mwanamke Sara. Hawakuwa na watoto kitu ambacho katika nyakati hizo ilionekana kama laana. Kwa hiyo Mungu alipomwambia Abramu atakuwa na watoto wengi hakuelewa. **Watu wengi walimcheka Abramu, mtu ambaye jina lake liliwakilisha uzao mwingi na hakuwa hata na mtoto wa kuthibitisha Jina Lake nab ado alikuwa mzee.**

Kama Ibrahimu kila mtu anakabiliana na changamoto katika maisha yake leo ambazo ni kubwa kuliko hata yeye. Wengine wana madeni makubwa kuliko hata pesa walizonazo, wamevunjiwa mahusiano au magonjwa – mambo ambayo yako zaidi ya uwezo wao.

Elewa hili: **Mapenzi ya Mungu ni makubwa kwetu hata zaidi ya jinsi tunavyofikiri na hata zaidi ya uwezo wetu.** Unafikiri kwa nini iko hivyo? Kwa sababu anataka tuwe katika sehemu ambayo tutaweka tumaini letu na imani yetu kwake kwa ajili ya utukufu wake na si wetu. Ikiwa tunataka tuone majina yetu yanang'aa na tunataka watu wajue kwamba sisi ni watu maalumu ujue hatuko tayari kupokea maisha mapya ndani ya Kristo. **Mungu itabidi atunyenyekeze na kutushusha kwa kiasi kwamba tunaelewa kwamba sisi si kitu na yeye ni kila kitu.** Hadi hapo, anaweza kturudisha aweze kututumia.

Paulo anaendelea katika mistari michche ya mwisho kwa kutuonesha kwamba imani inatokana na nguvu ya Mungu, si juhudi za wanadamu. Mwanzo 17:18-19: "Na Ibrahimu akamwambia Mungu, 'Ikiwa Ishameli ataishi chini ya baraka yako!' Halaf Mungu akamwambia, 'Ndiyo, lakini mke wako sara atakuzaliwa mtoto na utamwita jina lake Isaka Nitaweka agano langu kwake agano la milele na kwa kizazi chake baada yake.'" Walipozeeka Ibrahimu na sara walikuwa wanajaribu kufikia swala la kupata mtoto kwa nguvu zao na wakaishia kwa Ishmaeli baada ya kulala na Hajiri. Lakini Mungu alijua kile alichokuwa anakifanya na kwa muujiza sara akawa mjamzito akamzaa Isaka. Mungu alimtumia Isaka kama uthibitishi wa Nguvu zake za

kiungu na akambariki Ibrahimu. **Nje na mapenzi ya Mungu juhudi za Mwanadamu zitasababaisha uharibifu. Ahadi za Mngu zinatimizwa kwa nguvu zake.** Haijalishi wewe ni mjanja au una hekima kiasi ganikufuata mipango ya Mungu kunaleta uzima wa amani na huru katika Bwana.

Paulo anachanganua sifa **saba** za Imani ya Ibrahimu kwa Mungu :

1) **Aliamini kwa matumaini.** Matumaini na imani vinahusiana lakini havifanani. Matumaini ni shauku ju ya kitu Fulani kitakachotokea au cha kweli. Imani ni uhakika na kwamba itatokea. Msingi wa Imani ya Ibrahimu ilikuwa ni Mungu. Alitumainia pasipo na matumaini. Akaamini kwamba itatokea.

2) **Ibrahimu alimwamini Mungu bila kulegea katika Imani yake.** Ibrahimu kweli alimwamini Mungu. Unajiona kwamba unategemea nguvu zako badala ya kuweka juhudi zako kwa Mungu bila kujali hali gani?

3) **Imani yake ilimfanya asikate tamaa.** Juhudi zake za kupata mtoto zilikwisha Mungu huondoa juhudi za mwanadamu. Ngoja nikuulize swali: Mungu kaondoa nini ili kwamba kwa dhati uweze kumtegemea? Uko tayari kuweka tumaini lako kwa Kristo aliye hai?

4) **Aliamini japo Tumbo la Sara lilikuwa halizai.** Tunapoona mambo yamegoma huwa tunapoteza imani. Kwa nini? Tunaona kushindwa. Mungu anaona ni nafasi ya kujichukulia utukufu na kuonesha nguvu zake.

5) **Mambo yaliposhindikana Ibrahimu alisimama imara katika Imani.** Ni rahisi sana kumtumaini Mungu mamabo yanapokwenda vizri lakini tunapokabiliana na yasiyowezekana mawazo ya kibinadamu yanapiga hodina kusema, “Ngoja nifanye nitafaulu.” Mungu alipompima Ibrahimu nafikiri kilitokea nini? Alikomaa kiimani (Yakobo 1:2-4). Mwanatheologia liwahi kuandika, “Imani ya Kiungu haijajaa uelewa bali imejaa matumaini.”

6) **Imani ya Mungu inamtukuza Mungu.** Yule aayetoa Imani ndiye anayepokea sifa. Tunapaswa kuwa makini tusiibe utukufu wa Mungu. Ni rahisi kuhisi kwamba unahitaji kusifiwa lakini sifa zote niza Mungu.

7) **Ahadi za Mungu ni kweli na Nguvu yake inatosha.** Ahadi za ungu huwa hazirudi bure. Nguvu ya Mungu inatosha. Majawabu ya Mungu wakati wote yanatosha kutimiza jukumu alilokuitia ulifanye.

SURA YA 17

AMANI & FURAHA

Warumi 5:1-5

"Na tumaini halitatahayarishi kwa maana pendo la Mungu limekwisha kumiminwa katika mioyo yetu na Roho mtakatifu tuliyepewa sisi."
- Warumi 5:5

Yesu alipokuwa akitembea hapa duniani, alikuwa ni Emanueli, "Mungu pamoja nasi" (Mathayo 1:23). Sasa, Kristo, au tumaini la utukufu, liko ndani ya kila muumini. Kristo anatenda ndani yake na katika mambo yote ya maisha ya mumini ili kuwakuza wawe kama yeye katika kila jambo na kuendeleza uvumilivu na sifa njema. Paulo anatuambia kwamba, "Na tmaini halitahayarishi" (Warumi 5:5a). Kupitia barua hii Palo anawafundisha warumi kwamba tumaini linategemea mtazamo wa Mungu na kwamba linakuwa kadri wanavyoendelea kumtafakari Mungu na ahadi zake. Watu wengi wanatumia muda wao wakizungumza na kufikiri na kusoma juu ya *matatizo* yao kuliko ahadi za Mungu.

Tumaini wa Wakristo limeelezwa ni mtazamo chanya kwa ajili ya yajayo kwasbabau tunaweka tumaini letu kwa msulubiwa, mfufuka na atakayerusi haraka Yesu ambaye ni Bwana wetu na Mwokozi. Matmaini mengine hayako kenye msingi lakini heri yaliyo katika malisho mabichi. Watu wengi hununua tiketi za bahati nasibu. "Tmaini" lao la ushindi inakuwa ni kama pua inayoning'inia. Tumaini kwa ajili ya matumaini ni vizuri wala haizai matunda – tunapaswa kuweka tumaini let kenye mambo ya Msingi. <u>Kwa wakristo tumaini ni kitovu cha imani yetu.</u> Na kama wakristo tunaishi na tumaini la kwamba Mungu ndiye kila kitu na mwana wake Yesu kristo.

Mstari 1-2: *"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika Imani na mwe na amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana we Yesu kristo ambaye kwa yeye tmepata kwa njia ya Imani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani yake na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu." –* "Tunafurahi katika tmaini la utukufu wa Mungu."

Krsto huishi katika kila muumini kama tumaini lao la utukufu. Mistari hii miwili ya kwanza inaeleza kwamba, kama wakrsto tumepatanishwa na Mungu. Hii ndiyo maana rahisi ya msemo wa "Kuhesabiwa haki kwa njia ya Imani," ambayo tumeiangalia katika sura iliyopita. Imani na matumaini yetu katika Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi inaleta amani kai ya Mungu na sisi. BKwa kuwa katika hali hii ya amani ya kiroho kuana faida nyingi, na si katika machache ambayo tunayategemea hapo baadae kwa ujasiri kwamba mungu atatimiza ahadi yake ya kutuchukua kwenda kuishi naye milele. "Tumaini letu la utukufu wa Mungu" Ni kujuwa kwamba Mungu atakuwa mwaminifu kwetu na kwamba haijalishi nini kitatokea sasa maisha yetu ya baadae tayari yamekwisha kuandaliwa. Kristo hutenda katika vitu vyote katika maisha ya muumini kujenga sifa yetu ili tuwe kama yeye katika kila jambo.

Mstari 3-4: *"wala si hivyo tu bali mfurahi hata katika dhiki pia mkijua yaKUWA DHIKI huleta thaburi na kazi ya thaburi ni uthabiti wa moyo na kazi ya uthabiti wa moyo ni* ***tumaini****."* Sasa Paulo anatumia "Tumaini" mwishoni mwa mlolongo wa matukio unaoanza na mateso.

Paulo anafundisha Warumi kwamba tumaini lao huongezeka katika tabia za kimungu, kitu ambacho kitawasaidia kukua katika hali zote. Kwel;I kuu kuhusu tumaini katika Mungu ni kwamba halipunguzwi na matukio, kuhangaishwa au bahati mbaya. Wat wa matumaini katika nyakati ngumu hupatiwa nafasi kuu ya kshirikisha ushuhuda wao wa ujasiri katika Kristo. Ni wito wa kupokea na kukubali hali halisi ya mateso katika maisha yetu, tukimtumaini Mungu kwamba atatusaidia kuvuka. Hakuna jambo kuu ambalo limekwisha kukamilishwa wakati tumaini la ndani linapokuwa halijatokea. Kristo hutenda kupitia na katika vitu vyote katika maisha ya muumini ili kujenga sifa zao wawe kama Kristo katika kila jambo.

Mstari 5: *"Na **tumaini** halitahayarishi; kwa maana pendo la Mungu ,imekwisha kumiminwa katika mioyo yetu naRoho mtakatifu tuliyepewa sisi."* Roho mtakatif katika msiha yet ni kama wekezo lililofanywa na Mungu - Uhakika – kwamba siku moja yote yaliyoahidiwa yatatokea. Tumaini hujengwa katika upendo wa Mungu katika maisha yetu. Zaburi 33:18 inasema, "Lakini macho ya Bwana yako kwa wale wanaomcha, kwa wale ambao tumaini lao liko katika pendo lisiloshindwa." Tumaini ni furaha yenye nguvu katika maisha. Tumaini kwetu, katika vitu, na katika mausiano ni uharibifu. Tumaini letu linaweza kuimalishwa kwa mwenye uwezo Bwana Yesu. **Hili ndilo tumaini la kweli lililopo kwa ajili ya wanadamu wote.**

Tmaini la mkristo pia liko katika hali isiyopingika nay a ukombozi wa Yesu Kristo. 1 Wathesalonike 1:3 inasema, "wala hatuachi kuikumbuka kazi yenu ya imani na taabu yenu ya upendo na saburi yenu ya tumaini lililo katika Bwana wetu Yesu Kristo mbele za Mungu Baba yetu." Shemu ya mwisho ya Warumi hii inasema kwamba tumaini letu pia limejengwa katika uwepo wa Roho Mtakatiu katika maisha yetu. Kama wafuasi wa Kristo tumesimikwa kwa Yesu kwa hiyo kama watoto wa Mungu tuishi maisha yanayoonesha tumaini lililo hai na kweli.

Majanga yanapotokea katika dunia, wakrsto wanapaswa kutulia na kukumbuka ahadi za Mungu. Tumaini linaimarish mioyo yetu na kutuandaa kwa ajili ya yajayo. Lakini pia inatuongoza kufanya vitu katika uwezo wa Roho Mtakatifu, jamabo ambalo bila yeye ni "hakuna matumaini".

SURA YA 18

UPENDO WA KRISTO USIO NA MASHARTI

Warumi 5:6-11

"Bali Mungu aonesha pendo lake kwetu sisi: tulipokuwa tngali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajili yetu."- Warumi 5:8

Katika sura ya Mwisho tumesoma mistari yote mitano ya warumi 5. Kabla hatujaendelea nataka nipate dakika chache tupitie tena. Kuelewa sura nne zinazokuja, inatusaidia kukumbuka ukweli wa namna mbili wa maisha ya Kikristo. Katika pande mmoja sisi ni kamili katika Kristo – Kukubaliwa naye tuko salama– kwa sbaabu ya mabadilishano ya haki ya Kristo. Kwa upnde mwingine tena tunajitahidi kukua katika Kristo – tuwe kama Yeye Zaidi. Tuna hali ya ufalme na majukumu ya kiutumwa. Tunasikia uwepo wa Kristo na misukumo ya dhambi. Si tu kwamba tuna furaha na amani inayotokana na kumfahamu Kristo kama mwokozi lakini pia tunakabiliana na matatizo ya kila siku yanayosababisha tukue katika Imani.

Tunapaswa kuyaelewa maeneo yote mawili ya maisha ya Kikristo. Ikiwa tutafanya, hatutakatishwa tama tnapoingia katika dhiki. Badala yake tutajifunza namna ya kuzitegemea nguvu zilizopo kwa njia ya Roho Mtakatiu. Mahusiano yetu na Roho Mtakatifu yanaanza kwa imani – Imani ya kwamba Mung ni kweli na yu hai na anataka kuishi ndani na kupitia maisha yetu. Tumaini laweza kukua kadri tunavyotambua tabia za Mungu, ahadi zake na nguvu zake. **Tumaini linatupatia uhakika wa yajayo.** Kifuatacho ni upendo. Hatuwezi fanya lolote Biblia inatufundisha tusipokuwa na upendo. 1 Korintho 13:13 inatuambia, "Basi sasa inatumu imani, tumaini, upendo. Haya matatu, na katika hayo lililo kuu ni upendo." **Upendo wa Mungu unatujaza na kutupatia uwezo wa kuwapenda wengine.** Kina cha uoendo wako kwa ajili yaw engine unaonesha kina cha upendo wako kwa Mungu. Huwezi kumpenda Mungu bila kuwapenda wengine pia. Mtazamo wote wa Biblia umelala katika upendo. Ni upendo tajiri na wa kina unaotoka katika Mungu na unakuwa na kutufanye tuwe kama unavyotaka tuwe.

Mstari 3: *"wala si hivyo tu ila na mfurahi katika dhiki pia. Mkijua dhiki kazi yake ni kuleta thaburi."* Furahia uwapo katika Mateso. Je sasa unalo tatizo katika maisha yako?? **Matatizo ni mazuri.** Kwa nini? Kwa sababu matatizo yanapokuwa makubwa tunakuwa na maumivu makubwa na ndivyo tunavyo zama katika kumtegemea Mungu. **Tumaini letu linapozama, tabia zetu zinatengenezwa na tunakuwa hatujitegemei sisi bali tunamtegemea Mungu kwa ajili ya yajayo .**

Sasa katika mstari wa 6: *"Kwa maana hapa tulipokuwa hatuna Nguvu wakati ulipotimia Kristo alikufa kwa ajili ya waovu."* Sisi ni dhaifu na hatuna ngvu. Bila Mungu sisi ni wenye dhambi. Hatuwezi kujiokoa hivyo Mungu akamtuma mwanawake kutuokoa.
Mungu hahitaji nguvu zako bali udhaifu wako.

Mtsari 8: *"Bali Mungu aonesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi kwakuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi."* – "Tulipokuwa tungali wenye dhambi." Hii inamaanisha nini? Tulipokuwa hatuna msaada mbele za Mngu, hatustahili upendo wake wala neema yake. Hatuan nguvu ya kukimbia dhambi, hatuna nguvu za kumshinda shetani

na hatuna nguvu za kuwa na mahusiano na Mungu kwa namna yoyote. Kwa hiyo Mungu akaonesha pendo lake lisilo na masharti kwetu kwa kumtuma mwanawake kufa kwa niaba yetu. Alionesha upendo kamili. Upendo tulio nao wewe na mimi kwa wengine ni tofauti. Wanadamu wanauopendo wa tofauti– tunawapenda wale wanaotupenda. Ni rahisi kumpenda mtu anayekupenda lakini kumpenda anayekuchukia ni aina ya upendo unaotoka kwa Kristo. Kwa maneno mengine tunaweka masharti katika upendo wetu. Upendo wa Mungu hauna masharti hata tulipokuwa tungali wente dhambi.

Msatri wa 10: *"Kwa maana tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake zaidi sana baada ya kupatanishwa tukaokolewa katika uzima wake!"* Mung hujtuokoa si katika dhambi za mwanzo tu tunapookoka bali hata kwa dhambi za sasa na mahangaiko. Neema ya Mun gu inatosha tunapokuwa watoto wake kabisa.. **Baraka zote zinatoka kwa Kristo.** Tunaliona hili katika kitabu hiki cha Warumi:

1) Amani hutoka kwa Mungu. (Mst. 1)

2) Neema na utukufu wa Mungu. (Mst. 2)

3) Upendo wa Mungu umemwagwa ndani yetu na Roho wake. (Mst. 3-4)

4) Tumeokolewa kutoka katika dhambi kwa mateso ya kifo chake. (Mst. 5-7)

5) Ukombozi kutoka katika ghadhabu yake. (Mst. 8)

6) Upatanisho na Mungu. (Mst. 9)

7) Kuhifadhiwa katika maisha haya. (Mst. 10)

Upendo uliompelekea Yesu kufa kwa ajili yetu sote ni upendo ule ule unaomruhusu roho mtakatifu aishi ndani yetu na kutuongoza kila siku. Nguvu iliyomfufua Yesu kutoka katika wafu ni nguvu ile ile inayotuokoa sisi na iko kwa ajili ya maisha ya kila siku. **Mungu atatusubiri tumwite kwa ajili ya maisha ya kila siku na kusaidia upendo wake.**

Mstari wa 11: *"wala si hivyo tu ila pia twajifurahisha katika Mungu nkwa Bwana wetu Yesu Kristo ambaye kwa yeye sasa tumeupokea upatanisho."* Tnafrahi kwa sababu Mungu kafanya ambayo hatukuweza kuyafanya wenyewe. Alitwaa adhabu yetu msalabani. Huu ni upendo usio na masharti. Kwakuwa Kristo amefanya hili kwa ajili yetu tunauhakika wa kuwa na mwelekeo wa kuungana na Mungu kwa njia ya Kristo. Kwa kuwa tunaweza kujitambulisha na kitu tunachoweza kukiona, kukihisi, kukigusa, na kukipata Kristo alikuja duniani akiwa 100% mwanadamu. Kristo ni mwokozi kamili, dhabihu kamili, ni mwokozi kamili, mwokozi kamili, na rafiki kamili. Kwa sababu ya Kristo tumewekwa huru kutoka katika mizigo ya dhambi yetu na mizigo ya ulimwengu. Ni mfano kamili wa kufuata ili kuongoza maisha kamili hapa duniani na milele yote.

Ikiwa Mungu ameonesha pendo lake hali tulipokuwa ni furushi la mema kwa bila faida sasa hiyo inatueleza nini sisi katika wajib wetu kama wakristo? Tunapokuwa na kristo tumeitwa kuonesha pendo la Mungu kwa ajili yaw engine bila kujali wanasema nini au wanafanya nini kwetu. Mungu kabisa atamweka kila mmoja wetu kwenye naasi ya kuwapenda wale wanaotuchukia. Ni kipimo cha kuona ukomavu wetu katika Kristo. Inahtajika mkristo aliyekomaa kufaulu kipimo hiki.. **Mpende adui yako mbaya.** Wachungaji, wapendeni wanaoleta masumbufu katika makanisa yenu kama vile mnavyowapenda wale wanaotoa sana.. **Tnapaswa kumruhusu roho wa Mungu atufundishe namna ya kuwapenda watu tunaowachukia.** Tumruhuru roho wa Mungu atupatie nguvu ya kushinda vipingamizi katika maisha yetu.

SURA YA 19

MAISHA NDANI YA KRISTO

Warumi 5:12-17

"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya Yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa Yule mmoja Yesu Kristo."- Warumi 5:17

Umeshawahi kufikiri ni kwa jinsi gani mt mmoja anaweza kuwaathiri wanadamu wote? Inawezekanaje dhambi ya mtu mmoja usababishe ulimwengu kuwa wa watend dhambi (Mwanzo 2:15-17)? Adamu na Eva walikuwa watu w kwanza kuumbwa na Mungu. Waliumbwa kwa mfano wake Kwa maneno mengine walitengenezwa na kuumbwa tofauti na viumbe wengine. Wanadamu wana nafsi. Hakuna kiumbe kingine Mungu alichokifanya kina nafsi. Adamu na Eva waliposhindwa kumtii Mungu kutokutii kwao kukatengeneza gonjwa linaloitwa dhambi. Dhambi ikamtenda adam na eva mbele za Mungu. Eva alikuwa wa kwanza kutenda dhambi lakini Paulo anaiweka dhambi kwa Adamu kwa ajili ya watu wote. Kwa nini? Mungu alimpatia Adamu amri ya moja kwa Moja asile kutoka katik mti na alikuwa kiongozi wa Eva. Alitakiwa kusisitiza ili atii.Unaona kuna uongo hapa katika maisha ya Kikristo umekuwa akifanyika:

1) **Watu wote wanamaamuzi huru.** Adamu alikuwa na nguvu ya maamuzi na kwa sababu ya kutokutii kwake madhara yalikuwa ni dhambi, matokeo ni adhabu.

2) **Maamuzi tunayoyafanya yanatabiri mambo yetu ya baadae.** Kwa nyongeza kuna amri juu ya ujinga wote. Amri ya Mungu ni Mungu, Kristo na mwanadamu. Hii ni Amri. Adamu aliwajibika japo Eva alifanya dhambi. Kwa nini? Kwa sababu ya amri ya Mungu.

Msatri wa 12: *"Kwa hiyo kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni na kwa dhambi hiyo mauti na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi."* – "Dhambi iliingia ulimwenguni kwa sababu ya [Adamu]." Angalia Paulo hasemi kwamba chanzo cha Dhambi ni Adamu kwa sbabu ililetwa limwenguni na shetani. Shetani alimkabili Adamu na akamwathiri kwa gonjwa la dhambi Kifo cha mwanadamu ni matokeo ya dhambi. Hatufanyiki wenye dhambi. Sisi ni wenye dhambi kwa asili. Dhambi ikaleta mauti na kifo cha kiroho ni kutengana na Mungu. Wazo hili la dhambi na haki ni nguvu. Nini ilikuwa kusudi la sheria? Kuwasaidia watu waone dhambi yao na kuwaleta kwa Kristo. Dhambi ni tengano wa ndani kabisa kati ya njisi tulivyo na jinsi tulivyokuwa tumeumbwa. Sheria inatupa mazingira ya dhambi yetu, lakini haitupi kibali cha kutosjereza dhambi zetu bali ni kifo. Kwa hiyo kiutendaji sheria inatupatia kanuni ya kuona jinsi gani tulivyo wenye dhambi kitu kinachotupelekea kwenda kwa Kristo mwokozi. Ni kwa neema ya Mungu tumekamilishwa kwa njia ya mwana wake.

Mstari 13-14: *"Maana kabla ya shria dhambi ilikuwako ulimwenguni lakni dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria. Walakini mauti ilitawala tang Adamu hadi Musa nayo ilitawala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu aliye mano wake yeye atakaye kuja."* Mauli niyaulimwengu. Hatuwezi kuepuka. Hata kabla ya sheria kulikuwa na kifo. "tangu nyakati za Adamu."

Mstari 15: *"Lakini karama ile haikuwa kama kosa kwa maana ikiwa kwa kukosa kwake Yule mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mngu na kipawa na kipawa kilicho katika neema ya mwanadamu mmoja Yesu kristo kimezidi kwa ajili ya wale wengi!"* Kifo kilikuja kwa njia ya adamu. Uzima wa milele unapatikana kwa njia ya mtu mmoja, Kristo. Sisi sote tumezaliwa katika amilia ya mwili ya Adamu na kwa sbabau ya dhambi sisi sote lazima tufe milele. Kila mtu katika ulimwengu amerithi asili ya dhambi. Hata hivyo Mungu kafanya njia ya mwanadamu kukiacha kifo na kuwa na uzima njia ya kuacha hukumu kwa kuwa na msamaha na kuiacha dhambi na kuwa haki ya Kristo. Kama tulivyoza,iwa katika familia ya adamu tuna uhuru wa kuchaguwa kuzaliwa katika familia ya Mungu kwa njia ya Kristo. Mti wa familia ya Yesu unaanza na msamaha na kutupeleka katika uzima wa milele. Ikiwa hatutachagua, maana ake tumechgua kifo kwa njia ya Adamu; lakini tunapokuja kwa Mungu katika imani, tunakuwa na maisha mapya katika Kristo. Kwa hiyo swali ni hili: **Unataka uwe katika familia gami?**

Mstari 17: *"kwa maana ikiwa kwa kukosa kwa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu bya Yule mmoja zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema na kile kipawa cha haki watatawala katika uzima kwa Yule mmoja Yesu Kristo."* Hii ni kanuni nyingine ya maisha ya Kikristo. 2 Petro 3:18 amatumuru, "Kukua katika neema na ufahamu wa Bwana na Mwokozi Yesu kristo." Kanuni si kuwa na sheria nyingi na miongozo au orodha ya yapi fanye na yapi usifanye. Sheria hazibadili; bali mahujsiano na Kristo kunatufanya tubadilike tulivyo. Tnapofanya chini ya sheria nyingi tunatengeneza tabia katika nyakati, kanuni haziwezi kutubadili ndani nje. Jamii zet zinahitaji hatua tatu kufaulu, hata 10 kuwa wanyenyekevu, na 8 uacha mihadarati. Hatuwezi kupunguza imani yetu katika Kristo kwa kufuata hatua. Ikiwa tutafanya tjue ni juhudi na siyo yale mahusiano.

Wafilipi 1:6 inatupa ahadi mbili za ajabu:

1) Ikiwa Mungu ataanzisha jambo katika maisha yetu, mpango wake ni kulikamilisha. Lengo lake ni kutugeuza tuwe katika Mfano wake.

2) Ukomavu uko katika Kristo na si katika hatima; Ni mchakato wa ukuaji unaoweza kutenda ndani yetu tang tunapompokea Yesu hadi masiha yetu yote.

SURA YA 20

HUKUMU YAWEZA KUBADILISHWA KWA MSAMAHA

Warumi 5:18-21

"Basi tena kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote waihesabiwa haki ya uzima."
- Warumi 5:18

Nini lilikuwa kusudi pekee la Yesu alipokuwa hapa duniani? Msingi na kusudi pekee la maisha ya yesu ilikuwa ni kufanya mapenzi ya Mungu. **Yohana 4:34 inasema, "chakula changu ni kuyatenda mapenzi ya Baba aliyenituma na kuimaliza kazi."** "Chakula" hapa inamaanisha kustawishwa kiroho inayotokana na kusoma neno la Mungu kuomba, na ushirika, lakini zaidi ya yote ni kfanya mapenzi yake. Yohana 5:30b inatuambia, "Natafuta si kujipendeza mwenyewe bali yeye aliyenituma." Yohana 6:38 inasema, "Nimekuja kutoka mbinguni si kufanya mapenzi yangu bali kufanya mapenzi ya yeye aliyenipeleka." Masiha ya yesu yalijawa na utii kamili kwa baba yake wa mbinguni. Yesu aliangalia kuongozwa na Mng kufanya mapenzi yake. Wafilipi 2:8 inasema, "akajinyenyekeza kwa kuwa mtii hata mauti, mauti ya msalaba."

Msatri wa 18: *"basi kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima."* Paulo anatuambia hapa kwamba mtu mmoja alileta adhabu kwa watu wote Adamu aliharibu watu wote kwa sbabu ya kutokutii kwake; lakini, anatukumbusha tendo moja la **Haki** katika Kristo limetuweka huru. Nini maana ya Haki? Kumtii Mungu. Tndo moja la Yesu kumtii Mungu ilikuwa khesabiwa haki kwa dhambi zetu zote. Kama tunavyofahamu, kuhesabiwa halki ni ktangazwa "Kutokuwa na Hatia"." Ikiwa tnataka kutambua asili yetu ya dhambi tujitambue kuwa sisi si kitu mbele za Mungu, tbu, geuka, acha dhambi na weka tumaini na Imani kwake, atatuwezesha kuishi maisha ya kweli ya Kristo. Paulo anaeleza kwa wazi umuhimu wa utii wa kristo na utayar wake wa kufanya mapenz ya Mungu. Hatuwezi kuokoka kama hanta utii kwa Kristo. Kwa namna hiyo hiyo Yesu anatupa mfano mzuri ya jinsi maisha yetu yanavyoweza kutengenezwa tukimtii Kristo. **Lengo la maisha yetu inatakiwa iwe ni kufanya mapenz ya Baba .** Kufanya mapenzi ya Baba mtu anatakiwa awe ameunganishwa na Mungu na aongozwe na Roho Mtakatifu.

Mstari 20: *"Lakini sheria iliingia ili kosa liwe kubwa sana na dhambi ilopozidi neema ilikuwa nyingi zaidi."* Kama mwenye dhambi uliyetengwa na Mungu unaweza kufanya na kujaribu kuweka njia zako za kukufikisha kwa Mungu lakini unaona ukifikia hatua mbili au tatu unaanguka na unakata tama. Je umeshawahi kukutana na hili? Au unaogopa refu wa ngazi na unaogopa kupanda hata hatua moja kwa sababu naogopa watu watakusema? Paulo anatuambia Yesu anataka atupandishe katika ngazi apande kila hatua pamoja nasi tunapokuwa tukitafuta mapenzi yakena kutupeleka moja kwa moja kwa Mungu . hapo tutakuwa tumewekwa huru kumtii na kufanya mapenzi yake kwa upendo na si kwa lasima na kupitia nguvu za Mungu na si ngvu zetu.

1 Yohana 2:12-14 inasema, "Nawaandikia ninyi watoto wadogo kwasababu mmesamehewa dhambi zenu kwa ajili ya jina lake. Nawaandikia ninyi akina Baba kwasababu

mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi vijana kwa sababu mmemshinda Yule mwovu. Nawaandikia ninyi watoto kwasababu mmemjua aliye Baba. Nimewaandikia ninyi akina baba kwasababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi vijana kwasababau mna nguvu na neno la Mungu linakaa ndani yenu nanyi mmemshinda Yule mwovu." Mistari hii inaeleza hatua tatu za mchakato wa Kiroho:

1) **Hatua ya 1 – Utoto:** Muumini anapotabua dhambi zake zimesamehewa kwa sababu ya kristo. Anaelewa msamaha na wokovu katika Kristo.

2) **Hatua ya 2 – Vijana / Kufuaswa:** Muumini anapoanza kutumia na kutegemea maandiko kupambana na majaribu ya Yule mwovu.

3) **Hatua ya 3 – Ubaba/ Kufasa wengine:** Muumini anapofuaswa, anakomkaa katika imani na lengo katika maisha yake ni kufuata mapenzi ya Mungu. Anajua kwamba haya yanakamilika kwa kujizalisha katika kuwafundisha wengine.

Kila hatua ni muhimu katika ukuaji wa imani ya Kikristo. Hatuwezi kuruka hatua hata moja katika mchakato huu. **Sisi sote tunapaswa kufuaswa. Lengo la kila Mkristo ni kuwekeza maisha yako katika maisha ya wengine.** Tunapoanya hili tunafanya Agizo kuu (Mathayo 28:19).

Utaruhusu mtu mwingine akufuase katika swala la Imani? Je utamfuasa mwingine? Kufuasa ni kuwekeza maisha yako kwa mtu mwingine. Ni kuishi maisha ya mtu aliye katika hatua ya 3. Inaitwa "Kuishi katika Uzima." Si kufanya mafunzo ya Biblia, ni zaidi ya hapo. Ni kuchukua swla la maisha na kuyapeleka maswala hayo katika macho ya Kristo.

SURA YA 21

KUFA, KUWA HAI KATIKA KRISTO

Warumi 6:1-7

"Tuseme nini basi? Tdumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi?"- Warumi 6:1

Nilipokuwa mtoto, mara zote nilikuwa nafanya vitu vya ajabu, kama vile kutema pembeni mwa barabara, kutupa uchafu kupitia kwenye dirisha la gari, kuwadanganya kaka zangu, - mambo yote ambayo nilifundishwa kutokufanya nilikuwa nayafanya. Kwa nini? Niliyafanya kwa sababu niliweza. Mara zote katika ulimwengu war oho tunaona Neema kama kwamba inaturuhusu kufanya kila jambo. Hiyo inaitwa Neema rahisi. Neema rahisi ni pale tunapoendelea kuafnya nje na mapenzi ya Mungu katika maisha yetu, tunakuwa tunajua dhambi ni nini lakini tunatumia neema kama kigezo cha kujitetea. Tunaomba msamaha, lakini tunakuwa tunajua kabisa hatuwezi kujitoa kabisa kufanya marekebisho ili turejee.

Hapa kuna swali ninalo kwa ajili yako: **Ikiw msamaha wa dhambi umehakikishwa je tuna uhuru wa kutenda dhambi kama tunavyotaka?** Paulo anasema, "Hapana." Hebu nikwambie hadihi nzuri. Katika ujana wake, John Newton aliondoka England na akaungana na jopo la meriya watumwa. Miaka kadhaa baadae akijikuta amekuwa mtumwa kwa mwanamke mweusi wa mfanya biashara wa watumwa mzungu katika Africa. Alihudumiwa vibaya sana. Alikula mabaki ya chakula kilichoachwa na watumwa wengine na akala mizizi ya mimea aliyoichimba wakati wa usiku ili aweze kuishi. Baada ya kutoroka kambi ya watumwa akaishi katika kundi la wenyeji kwa muda na baadaye akafaulu kuwa nahodha wa Meri.

Newton aliishi maisha machafu, lakni mwaka 1748 maisha yake yalibadilika sana baada ya kutoa maisha yake kwa Yesu. Akarudi England na akwa mtumishi wa Injili asiyechoka na asiye na ubinafsi huko London. Wakati huu aliandika nyimbi nyingi sana ambazo bado zinaimbwa duniani ukiwemo unaojulikana sana na yamkini ni wimbo unaoimbwa sana duniani, "Katika Neema." Newton akawa ni mchungaji katika kanisa huko England na eneo la kanisa kuna jiwe la kaburi lake aliloliandika mwenyewe: "John Newton, karani, once an infidel and libertine, mtumishi wa watumwa katika africka, kwa neema kubwa ya Bwana wetu yesu kristo, aliyewekwa, akarejeshwa, akahurumiwa na kuchaguliwa kuhubiri imani aliyokuwa nayo kama mzigo." John Newton califika katika hatua maishani mwake aliona mkono wa Mungu kazini katika maisha ya watu. Alichagua kumfuata kristo na kwa hiyo akachagua uzima na utii kwa Mungu. **Kama unasema unamwamini Mungu na unaendelea katika uasi yawezekana hukuwa na wokovu wa kweli.**

Mara nyingi tunatumiamakundi au namna mbalimbali za nje za kujaribu kushinda dhambi katika msiha yetu.. **Hiki huwa nakiita dhambi chini ya utawala.** Dhambi huwa haishindwi wala kutawaliwa. **Inatakiwa iuawe, na njia peke ya kuiuwa dhambi ni kuipeleka kwa Kristo.**

Hebu turudi kwenye 1 Timotheo 1:12-13: "Nami namshukuru Kristo Bwan wetu aliyenitia nguvu kwasbabau aliniona kuwa mwaminifu akaniweka katika utumishi wake. Ingawa hapo kwanza nilikuwa mtukanaji mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri lakini nalipata rehema kwakuwa nalitenda hivyo kwa ujinga na kwakutokuwa na imani ." Paulo anatuambia japokuwa

alikuwa ni metnda dhambi, lakini bado Mung alimuonesha rehemana neema. Nenda katika 1 Corinthians 1:2: "Watendao mabaya hawataurithi ufalme wa Mungu." **Dhambi ni tatizo kubwa katika maisha ya mwanadamu.** IKatika asili, dhambi inatuonesha tulikuwaje na Kristo inatuonesha tunaweza kuwaje.

Hapa kuna swali: Maisha yako yanaonesha nini? Maisha yetu hayafanywi kulingana na jinsi tunavyosema kwamba tunaweza kuwaje bali ni kutokana na kile tunachokifanya. Matendo yetu yanaeleza jinsi tulivyo.

Mstari 1: *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi nkuwa nyingi?"* Je tnaendelea kutenda dhambi kwa sababu neema ya Mungu itafunika dhambi zetu? Paulo anasema , "No hasa! Sisi tulioifidhambi tutaishije katika dhambi?" Muumini hayuko chini ya vifungo vya dhambi. Tunapokuwa tumeokoka tunaanza njia takatifu ya maisha, inayoishiwa na nguvu ya Mungu inayotenda katika maisha yetu. Kwa asiye amini dhambi inaharibu kila kitu anachokifanya kwa sbabau ndiyo maisha yake. **Lakini Mumini aliye na maisha mapya hujiachilia kwa Mungu na roho wake na hana sababu ya kuendele katika maisha ya dhambi.** Je mtu anayesema kwamba ameokoka lakini anaishi katika katika misha ya giza je anaweza kuwa mwana wa Mungu? Wengi wanweza kusema kwamba ndiyo lakini Paulo anasema Hapana.

Dunia ya Magharibi imeizimisha Injili kwenye micro wave kwa dakika 30. Eti tu kwa sababu mtu kanyoosha mkono na kusema "Ndiyo" kwa Kristo anapita mbele na kuzungumza na mchungaji na kuandika karatasi je hii inamfanya apate tiketi ya kuingia binguni? Marekani imeifanya Injili kama badiliko. Lakini kwa namna mbalimbali huwa hawaiishi Injili. Tunashindwa kuyaweka maisha yetu kwa Kristo. Wengi wanamwita mwokozi lakini ni wachache wanamwita kuwa ni Bwana. **Je namweka mbele ya kila kitu katika maish yako? Kama siyo basi si Bwana.** Ni kama tunataka atupatie tiketi ya kwenda mbinguni na baadaye anatuacha. Je Yesu ni Bwana wako au ni kama Bima unayotaka kuitumia mwishoni mwa maisha yako?

Tumekuwa ni watu huru sana ambao tumeharibu Baraka z baba zetu waliopigana kwa ajili ya nchi hii na kuwa katika moyo wa Mungu. Mungu anataka tumtegemee. Tunapokuwa hatumtegemei tunakuwa tunajitegemea na kujiondoa. **Yesu Muda wote alikuwa na watu.** Wakristo wengi wamejitenga na ulimwengu. Wanajizungushia watu walio kama wao, wanaozungumza kama wao na hata kuishi kama wao. Wamejitenga na ulimwengu. Yesu anasema sisi ni chumvi na Nuru ya ulimwengu (Mathayo 5:13-16). **Tunawezaje kuuangazia ulimwengu kama tunakataa kuingia katika huo ulimwengu?**

Msatri 2: *"Hasha! Sisi tlioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?"* itawezekanaje kufa katika maisha haya na uishi tena katika maisha mengine? Hatuwezi. Tunapokufa, kinatokea nini– tunawekwa katika jeneza na kuzikwa. **Paulo anatuambia tuyazike mambo yetu ya kale.** Ikiwa mtu wa kale hajazikwa ujwe hatujaokoka. Maisha ya kiroho hayawezi kuwa na maisha ya kifo cha milele . 1 Yohana 3:9 inasema, "A;iyezaliwa kwa roho hatendi dhambi" kwa sababu mbeg zake zinaishi ndani yake na hawezi kurudia dhambi kwasababu amezaliwa na Mungu. Tunapokuwa na mai9sha ya kweli ya mfufuka yesu kristo katika maisha yetu tnakuwa na uwezo

wa kuishinda dhambi. Tunapokuwa tmeokoka kweli tunakombolewa. Mungu hatutangazi kuwa tu wenye haki tu lakini pia huanza kuendeleza haki ya Kristo ndani yetu.

Wokovu siyo swala la kubadilisha tu bali ni muujiza wa kugeuzwa. Wokovu wetu hauwezi kkamilishwa kwakuwa maisha ya Kikristo ni mchakato "Hadi siku ya Yesu Kristo." Wafilipi 1:6 inasema, "nani niliaminilo ndilo hili ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema ndani yetu ataimaliza hadi siku ya Kristo Yesu." **Kristo anapokja katika maisha yetu maisha yetu ya kale yanakuwa ni maiti – yanakuwa hayana uzima.** Kwa hiyo mambo ya kale yanakuwa hayana maana kwa sababu ni dhambi na hayawezi kumpendeza Mungu; Lakini maisha mapya, mtu aliyempokea Yesu katika imani anayeju kwamba hana msaada bila Yesu huyo anakuwa kapatanishwa na Mungu. Anampendeza Mungu kwa sababu ya Kristo na asili yake mpya ni Mungu na Haki basi. Mtu mpya kiroho yuko hai na utakatifu wa Mungu unatenda kazi ndani ya maisha yake. Hatuwezi kuwa na maisha ya kiungu bila kuishi kiungu. **Wokovu si mabadilishano bali ni Kugeuzwa.**

Msatri 3: *"Hamahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?"* Hapa Paulo anachanganua kanuni tatu zinazohusiana na mahusiano yetu na Kristo:

1) **Wakristo wote wa Kweli wamebatizwa katika Kristo Yesu**. Paulo hazungumzi swala la kubatizwa kwa maji. Ubatizo wa maji ni alama au udhihirisho wa nje wa kuzamishwa katika Kristo. Kuna watu wanaamini kwamba tunapaswa kuzamishwa katika maji ili tupate kuokoka. Hiyo si kweli. Kilicho kweli ni kwamba wokovu ni kwa njia ya neema kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Paulo anazungumza kwa mfano ubatizo wa Kiroho wa Mwamini ndani ya Kristo kwa njia ya Roho. Wagalatia 3:27 inasema, **"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo Yesu Mmemvaa Kristo."** Katika jamii ya Kirumi kijana aliyekuwa akikua alikuwa analiacha vazi la utoto na kuweka jingine jipya. Vazi hili lilikuwa linaonesha kwamba sasa anaelekea ukubwa kitu kilichomptaia haki na majukumu ya uraia wa Kirumi. Sawa na kwamba tunapokuwa wakristo tunaweka kando mambo yetu ya kale kwa kuzamishwa katika Kristo na kuvaa vazi jipya la haki. Tmezungukwa na kuunganishwa na Kristo tunapokfa katika mambo yetu ya kale na kumvaa Kristo.

2) **Wakristo wote wametambuliwa na Kristo kwa njia ya kifo chake na ufufuko.** Kanuni hii ni kituo cha kanbuni ya kwanza. Tnabatizwaje katika kifo chake? **Ili tweze kuishi na Kristo kwanza tufe.** Hatuwezi kuwa sehemu ya maisha mapya katika Kristo hadi pale maisha yetu ya kale yamekuwa sehemu ya kifo chake. Kabla hatujahesabiwa haki lazima tutangazwe "Hatuna hatia." Tutakapokuwa tmetangazwa "hatuna hatia," tunakuwa watakatifu, si kwa sababau ya utakatifu wetu bali ni kwa sababu ya utakatifu wa Kristo ndani yetu. Nioneshe mt anayeishi kwa ajili ya Bwana name nitakuonesha aliyejifia na kuzikwa pamoja na Kristo na kufufuka pamoja na Kristo katika maisha mapya. Mstari wa 4 unasema, *"basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* Maisha mapya yanakuja kutoka katika kujitoa kwenye mauti ya Krist. **Kifo katika maisha yetu kinahitajika na kinapaswa kutokea kabla hatujaishi maisha mapya katika**

Kristo – Mauti katika shauku zetu zote, uongo, udanganyifu, mawazo machafu na hata mihadarati (Wakolosai 3:12-14). Kwa katili, mtu asiye mkaribishaji, mkaidi, majivuno, kujiinua na mabishano hayajaingizwa haya yote katika maisha mapya ndani ya Kristo. Warumi 6:7 inatuambia tumekwisha kuwekwa huru kutoka katika dhambi.

3) **Kristo anaishi ndani yangu**. Hati ttakapoelewa kwamba mtu wa kale lazima afe hatwezi kuwa na maisha mapya ya kristo ndani yetu. Tunapopokea maisha mapya, tunabadilika – mioyo yetu inabadilika, roho zet zinabadilika, tunakuwa na tumaini jipya, nguvu mpya na imani mpya. Hakna hata moja ya Baraka hizi zinazounganishwa na maish yet ya kale. Mungu anasema. Zika. Songa mbele na Yesu na usitazame nyuma. Wengi wetu tunashughulika na vitu vinavyopaswa kufa. Hatuwezi kuuona uhalisi wa Kristo ndani yetu kama Kristo haishi ndani yetu. Chochote kisicho cha Kiroho ni ubatili katika macho ya Mungu. Tunashitakwa tnapokuwa tunashughulika sana na vitu vya dunia. **Mtu wa kale akifa, sasa twaweza kuvitegemea hivyo vilivyo vya Kiroho – Yesu Kristo**. Kabla hatujaokoka, tulikuwa watumwa wa dhambi; lakini kwa kuwa na Kristo tumeishinda dhambi. Wakalatia 2:20 ni mstari mzuri kwa kuishi nao: “Nimesulubiwa pamoja na Kristo, si mimi ninaye ishi lakini Kristo ndani yangu.” Mung huwaona waumini kana kwamba wamekua pamoja na Kristo. Tuko na Kristo katika mahusiano yetu. Nguvu ya kushinda changamoto za dhambi inatoka kwa Kristo; sisi hatuwezi.

Hebu tupitie hiyo michakato mitatu ya kuzaliwa upya katika ukristo:

1) Nimesulubwa pamoja na Kristo. Mtu wangu wa kale kafa kama vile Kristo alivyo kfa kwa ajili ya dhambi zangu .

2) Mimi mtu wa kale hatuna maisha yoyote kwa sababu yamekufa. Dhambi haiwezi kuniendesha tena.

3) Kristo anaishi ndani yangu. Nimemezwa na Kristo. Tunapaswa kuzamishwa katika Kristo maana hatuwezi kuishi bila Kristo. Hapo ndipo twaweza kusema Kristo anaishi ndani yangu.

Ni lini utamruhusu Kristo awe zaidi katika maisha yako? Ni matumaini yangu kuwa utatafuta uhalisi wake alio nao kwa ajili yako.

SURA YA 22

MUUMINI HAOGOPI KIFO

Warumi 6:8-14

"Lakini ikiwa tulikufa pamoja na Kristo twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye."- Warumi 6:8

Kuna swali kwa ajili yako: Unaogopa kifo? Katika sura hii, Paulo anatuonesha kwamba tunapaswa ka kifo cha kiroho kabla hata ya kupata uzima wa kiroho. Kwa maneno mengine, tunapaswa kufa wenyewe kabla hatujapata nafasi ya kusihi maisha mapya ndani ya Kristo. Kipingamizi kikubwa cha mwenendo wetu na Bwana ni dhambi tu. Tukikubali maisha mapya tnabadilishwa katika sra ya Kristo. Kila mtu anaugonjwa wa dhambi. Bila Kristo tutakuwa katika vifungo vya mambo ya kale mamabo ambayo yataendelea kuendesha maisha yetu. **Watu waio nje na ushirika na Bwana wanaogopa kifo.** Mkristo anayetembea na kumtumaini Mungu haogopi kifo . Kwa nini? Mkristo aliyekomaa anaelewa kwamba kifo ni machakato wa Muumini. Biblia inatufndisha kwamba " Tunapita" katika dunia hii. Hii ni nyumba ya Muda kwa Wakristo. Nyumba ya kudumu ya muumini iko mbinguni na ni milele. Milelel ni ahadi tuliyopewa na Mungu huko mbinguni.

Hebu tuangalie mstari wa: *"Lakini tukiwa tulikfa pamoja na Kristo twaamini ya kuwa ttaishi pamoja naye."* Tunakufaje pamoja na Kristo? Kama Kristo alivyokufa msalabani akilipa deni la dhambi zetu hivyo dhambi zet zife tusamehewe na kusamehewa tunapoweka tumaini lote na imani kwa Bwana. **Kifo cha amamb ya asili kinapotokea, maisha mapya yanaanza yakiwa na asili mpya.** Asili yetu mpya inaonesha sili ya Kristo ambayo ni tabia ya Mungu. Wao ni wamoja kwa hiyo kufa katika Kristo kwa hiyo ni kuishi na Kristo.

Msatri 9: "Tukijua kwa hakika kuwa Kristo akiisha kufufuka tena katika wafu hafi tena wala mauti haimtawali tena:

1) **Hakuna haja ya kuogopa kifo.** Jambo la msingi katika maisha ya Kikristo ni Kristo kufufuka kutoka wafu. Yu hai. Alifufuka siku ya Tatu baada ya kusulubiwa ili tupate kuishi. Dini zingine, kama uislamu, ubuda, Wahindu, Hare Krishna, etc., wanaabudu mtu aliyekufa anayewakilisha Mungu wao. Ni mwokozi pekee ndiye anayeishi – Yesu Kristo. Kristo ni mtu pekee/ Mungu wa kuishinda dhambi kwa sababu ya dhabihu yake na sisis kama waumini tumepatiwa nafasi ya kushinda kifo kwa njia yake. Kwa hiyo hatupaswi kukiogopa kifo.

2) **Ni wakati wa kufisha mambo yetu.** Kwa kuwa Kristo alikufa mara moja na kufufuka toka wafu hawezi kfa tena. Kwa hiyo tnapokufa kifo cha kiroho inamaanisha kwamba **tumezika mambo ya kale** na tnapomruhusu kuishi kwa imani maana yake tumefufuka katika **maisha mapya**." Kwa namna hiyo Kristo anakuwa ni sisi. Kueleza vizuri: Ni kama kuongeza cherry Kool-Aid kwenye shimo la maji. Kool-Aid inapopenya katika shimo la maji unajikuta kwamba molekuri za maji zinaungana na inakuwa ni vigmu sana kuvitenganisha. Hiki ndicho kinachotokea kwa mtu anayekuwa na Kristo katika maisha yake. **Kristo huingia katika kila nyuzi y roho na mtu anakuwa na mawasiliano na ahwezi kutenganishwa.** Mtu wa kale anapokuwa amekufa amekufa. Tatizo tulilo nalo ni kwamba huwa hatufi. Tmerhusu

sehemu yetu iishi na hatutaki kuiangamiza. Swali langu hili hapa: **Ni mambo gani katika maisha yako hayajazikwa? Mpaka hayo tuyaangamize ndipo Yesu atatuweka huru vinginevyo tutaishi maisha matupu yenye michanganyiko masiha yasiyo na furaha wala amani.** Krito ni njia ya kweli ya kuondoa mizigo katika maisha yetu.

3) **Tymefufuka katika Kristo.** Kristo alipofufuka kutoka kaburini milango ya kuzimu ilitikisika na shetani akashindwa milele. Mungu kamruhusu shetani kuikalia dunia kwa kipindi hiki lakini shetani anajua kwamba siku zake zinahesabika. **Unaona maisha ya shetani inamaanisha ni kifo na maisha ya Kristo inamaanisha Uzima.** Kwakuwa kaburi halikumshikilia Kristo kaburi haliwezi kutushikilia kama tutakuwa waumini wa kweli katika Bwana.

Mstari 10-11: *"Maana kwa kule kufa kwake aliifia dhambi mara moja tu lakini kwa kule kuishi kwake amwihia Mungu. Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu."* Angalia hapa, mifo kimoja na uzima vimeajwa. Tunapomruhusu kristo ktawala maisha tunamuiga Kristo na utii wake kwa Mungu d. **Tunaishi kwa ajili ya Kristo. Kristo anaishi kwa ajili ya Mungu. Ujue kwamba hatuishi kwa ajili yetu wenyewe.** Wazo hili ni jipya kwa ulimwengu na gum kwa Wakristo wapya kulielewa. Inabidi Nguvu ya Roho Mtakatifu kutubadilisha tuwe kama yeye Kristo.

Mstari wa 12: *"Basi dhambi isitawala ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti hata mkazitii tama zake."* Ukweli ni kwamba sisi sote ni watenda dhambi na njia pekee ya kuishinda dhambi ni kuweka mahusiano ya karibu au muunganikano wa Kiroho na Kristo. Wale ambao hawaamini ni wenye dhambi. Wanaubinafsi. Mtu mwenye haki huamini kwamba wao ni bora kuliko mtu mwingine na wanakila kitu. **Unaona, dhambi inanguvu ya kutuendesha. Hatuwezi kuiendesha dhambi. Njia pekee ya kuishinda dhambi ni Kristo.** Hakuna mtu duniani, kwa hiari yake mwenyewe anaweza kuishinda dhambi. Dhambi hushinda wakati wote.

Mstari wa 13: *"wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kfa na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki."* Mungu anataka tuyatoe maisha yetu kwake. Muda wote tuwe mali ya Mungu– pesa zetu, nyumba zetu, magari yetu, hata familia zetu. Yesu alijaribiwa na shetani lakini alikataa kwa kuomba na akimjibu shetni kwa njia ya Neno la Mungu. Njia peke ya kutembea njia ya furaha na amani ni kuwa na mahusiano na Mungu, katika Kristo kwa njia ya Neno lake.

Mstari wa 14: *"kwa maana dhambi haitawatawala ninyi kwasababu hamwi chini ya sheria bali chini ya neema."* Hapa Paulo anawaambia Wakristo kwamba kwakuwa wamekufa na kuzika mambo yao ya kale na kukombolewa na damu ya Kristo wanamaisha mapya. Maisha mapya ndani ya Kristo ni neema katika Kristo. Unaona katika Agano la kale mafari9sayo waliamini kwamba wanaweza kuhesabiwa haki kwa kutii "Sheria" kama tunavyofahamu ilikuwa ni taraibu zilizowekwa na wayahudi na zilikuwa jumla ya sheria 700 . Na Yesu alisema njia pekee ya Mtu kuwa huru kutoka sheria ni kuzitii sheria zote kwa ukamilifu. Kitu ambacho hakiwezekani na hivyo mtu chini ya sheria anahatia mbele za Mungu.

Hii hapa sehemu nzuri. Kristo alipokufa kwa ajili yetu alilipa deni la dhambiz etu na kw sababu ya hili tunapomwamini Yesu tunakombolewa “Kuhesabiwa haki” – Tunatangazwa “hatuna hatia” mbele za Mungu. Tunapohesabiwa haki tunaonekana kama **“wenye haki”** katika macho ya Mungu.

Kuwa haki maana yake kuwekwa sawa na Mungu. Ni wenye haki si kwa sababu ya kile tulichofanya bali Kristo alichofanya. Mungu alimtuma mwanawake wa Pekee ili kwamba tuhesabiwe haki na kustahilishwa mbele za Mungu mtakatifu. Tunapookoka tnazika yaliyopita na kuchukua maisha mapya na hatuendelei kuishi tena chini ya sheria, tunaitii sheria lakini hatuishi maisha ya kushindwa chini ya sheria. Kutokuwa wakamilifu kutatufanya tuishi kwa kuchanganikiwa. Kwakuwa Kristo ni mkamilifu na anaishi ndani yetu hatuwezi kuishi chini ya sheria tukijaribu kujipatia kitu tusichoweza kukipata. Kristo ameyafanya kwa ajili yetu.

SURA YA 23

DHAMBI INA NGUVU

Warumi 6:15-18

"Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi mkawa watumwa wa Haki."- Warumi 6:18

Katika sura hii tunakwenda kuzungumza juu ya dhambi na haki. **Dhambi ni nguvu inayosumbua sana ilyowahi kuingia ulimwenguni.** Dhambi naharibu roho ya mwanadamu. Ina iba nguvu na hata umuhimu wetu. Dhambi ina nata, sumu, uasi na ina ubinafsi. Dhambi inatudhoofisha katika mitego ya ibilisi. Dhambi huahidi furaha lakini humaliza kwa huzuni. Paulo anatuambia kwamba Mtu wa asili ni mtumwa wa dhambi. Dhambi ni nini? Dhambi ilitokeaje duniani? Nini matokeo ya dhambi? Kwa nini watu wanatenda dhambi? Swali loa mwisho – tunashindaje dhambi?

Sisi katika hali yetu ya kutokuwa kamili hatuwezi kuishinda dhambi. **Dhambi ina nguvu sana kwa Mtu asiye na Kristo.** Dhambi ni kutenda mambo yasiyokuwa katika mpango wa Mungu. Hakuna mwanadamu katika ulimwengu anayeweza kuishinda dhambi kwa nguvu zake. Kile pal anachokisema ni kwamba tnapompokea Kristo hatuko chii ya sheria bali chiniya neema. Tnapaswa uelewa kwamba sheria ni kitu mfu. Sheria isingeweza kuishi kwa sababu ili kuitimiza sheria mwanadamu anapaswa kuishi kwa ukamilifu; vinginevyo atatangazwa kuwa ni "Mwenye hatia."

Hakna njia ya kufika kwa Kristo bila ya Mungu kutupatia neema ya wokovu katika Kristo. **Paulo anatupa mawazo mawili: Kutii dhambi au kumtii Kristo.** Ikiwa tutamchagua Kristo tutaangukia katika neema ya Kristo. Paulo anasema hatutaishi katika sheria tena ambayo hapo mwanzo imetushinda bali tutakuwa chini ya neema. Kwasababu ya imani yetu katika kristo tumetangazwa "Hatuna hatia." **Wakristo wote wameokolewa kwa neema**. Neema haituhesabii haki tu bali inabadilisha hata maisha tuliyookolewa nayo. Maisha amabayo haytoi uthibitisho wa mabadiliko ya kiroho na wala ushuhuda wa wokovu**.**

Mathayo 6:24 inasema, "hakuna awezaye kutumikia bwana wawili**.** Maana atamchukia huyu na kumpenda huyu ama kumchukia huyu na kumpenda huyu. Huwezi kumtumikia Mungu na mali." Jambo la msingi ni kwamba mt hawezi kusi maisha ya aina mbili yanayopingana. **Tunapokuwa tumeokolewa hatuwezi kuishi katika upinzani wa dunia.** Paulo anasema ni vema kuwa mtumwa wa dhambi au kuwa mtumwa wa mungu katika Kristo ambayo matokeo yake ni haki. Tunapompokea Kristo tunayatoa maisha yetu kuwa maisha ya **utumwa katika haki**. Yohana anasema katika 1 Yohana 3:9, "Aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi kwa sababu neno la Mungu linakaa ndani yake." Kwa maneno mengine tunapookoka Mungu anabadilisha DNA ya Ukiroho wetu. Anatuokoa na kutuandaa kuwa wenye haki. Muumini wa kweli haendelei katika dhambi. Anakuwa ni mpinzani sana na maisha yake ya zamia ya dhambi na ahawezi kuendelea kuishi katika dhambi. Yohana 8:34-35 inasema, "Mimi [Yesu] nakwambia iliyo kweli yeyote atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." 2 Petro 2:19-22 inatuabia, "Mtu huwa mtumwa kwa kile kilichomjaza." Kuwa na nguvu katika Bwana. **Kuwa mtumwa wa Kristo na uwe njia ya kukimbia Dhambi.**

Mstari 17: *"Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi lakini mlitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake."* Ni muhimu sana sisi sote kutii mafundisho ya neno la Mungu. 2 Timotheo 1:13-14 inasema, "shika kielelezo cha maneno ya uzima liyoyasikia kwangu katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu ilinde ile amana nzuri kwa roho Mtakatifu akaaye dnani yetu." Paulo anazungumzia Wakristo wanaoishi kwa kumtegemea Kristo kabisa . Hapa kuna maswali mawili: Umewahi kumtegemea Kristo kabisa? Kwa moyo wako wote umewahi kulitii neno la Mungu. Utaanza leo kumtegemea Mungu kabisa na kumtumainia?

Mstari 18: *"Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi mkawa watumwa wa haki."* Kama wakristo lengo letu linatakiwa kuwa ni kuwa watumwa wa Haki. Ngoja nikupe mambo manne ninayoamini yanaweza kutupelekea kuwa watumwa wa haki katika Kristo:

1) **Kujishusha:** Usijivune. Kujivuna ni kinyume na kunyenyekea. Majivuno yanaharibu. Majivuno ni kujiangamiza. et rid of pride. Pride is the opposite of humility. Unyenyekevu ni mambo ya Mungu. Mwache Mungu akutengeneze na akufanye kwa Neno lake. Neno la Mungun litaondoa majivuno yote na unyenyekevu tachukua nafasi katika kiini cha utu wako.

2) **Utii kwa Mkuu:** Tathmini kile Mungu anataka wewe ufanye na uwe tayari kumtumainia kwa mipango yake yote na achana na ubinafsi wako. Je uko tayari kujiachilia kwa ajili ya mapenzi ya Mungu?

3) **Utayari wa kufanya kazi:** hakuna nafasi ya uvivu katika kristo. Ni vema tuifanyie kazi imani yetu katika utii na mambo ya kiroho. Ni lini mara ya mwisho lijihatarisha kwa ajili ya mambo ya kiroho? Safari ya Imani ni lazima ihusishe sehemu yetu na si jukumu letu lakini kwa upendo wa Mungu.

4) **Kumshukuru Mkuu:** hatutakiwi kuuharibu mwanga wa neno la Mungu usiangaze duniani. Tnaposhindwa kumshukuru tunazuia utukufu wa Mungu kung'aa duniani. Tunaposhindwa kumshukuru utukufu wa Mungu hautuangazii. Mungu anapaswa kupokea utukufu kwani yeye ni mkuu na katika yeye tnatimiza kazi yake. Elewa ni kwa ajili yake. Ni wakati wa kujikabidhi kwake.

Mtumwa hana haki. Mtumwa yuko kazini 24/7. Mtumwa anamtii mkuu wake. Mtumwa anatii mamlaka. Anatafuta kumfurahisha mkuu wake. Mtumwa hatafuti ktambulika. Mtumwa humtegemea mkuu wake kwa mahitaji yake ya kila siku. Hajisifii kwa ajili ya kazi yake. Ili uwe huru katika Kristo lazima uwe mtumwa katika Kristo.

Je utamruhusu Kristo akuweke wazi kwa haki yake ili ujifunze kuwa mtumwa kwa haki ya Kristo?

SURA YA 24

MUUMINI SI MTUMWA WA DHAMBI

Warumi 6:19-23

"Nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu. Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumie kwa ajili ya uchafu na uasi mpate kuasi vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na hakim pate kutakaswa ."- Warumi 6:19

Hii sura infungua mlango wa maada ambayo imekuwa ikisumbua wakristo wengi. Kwa miaka mingi nilikuwa na kusudi zuri la kufanya mazoezi wakati treadmill imekaa kwenye kona ya chumba chang cha kulala na nguo zikining'inia. Unajua nini kinaweza kutugundisha na jambo la sisi kufanya? Fungua mlango wa mtihano wako mwenyewe. **Kujiangalia kunatupelekea kujitathmini yapi ni mazuri na yapi si mazuri kuhusu sisi wenyewe.** Wakati mwingine tumekuwa vipofu kwa mambo yasiyofaa kwa sababu shetani amekuwa akitumia uchakachuaji ajaribu kutudanganya na atuendeshe. Ni rahisi kuona kosa kwa mwingine kabla hatuajaona kosa kwetu wenyewe. Katika mistari hii Paulo anatuambia kwamba bila kuwa Kristo kama Mkuu wetu sisi kama wanadamu tutakuwa tukiendeshwa na mambo ya ulimwengu.

Kuna nguvu za aina mbili – nzuri na safi inayotoka kwa Mungu na uovu na potofu inayotoka kwa shetani. Paulo anasema katika mstari wa 19a, *"nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu."* Paulo anataka tutambue kwamba bila Kristo sisi ni dhaifu . hatuwezi kukabiliana na mikikimikiki ya kila siku katika maisha. **Tumechanganikiwa kwasbabau kuna kusudi linalopotea ndani yetu.** Kwa hiyo anaendelea katika huo mstari wa 19b,
"kwa kuwa kama mlivyotoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi vivyo hivyo vitoeni viungo vyenu vitumie na hakim pate kutakaswa." Hapa Paulo anatupa mtazamo tofauti jinsi ya kushika maisha ili kushinda mambo yet binafsi. Kama wakristo tunapaswa **"kuacha kila kitu ili tuweze kuishi maisha ya utii katika Kristo."** Kuna mambo yaliyojificha katika mtazamo huu wa maisha amabo ni kwamba tunapokuwa waumini katika Kristo au tunapoyatoa maisha yetu kumfuata Kristo, tnapokea nguvu kutoka kwa Roho Mtakatifu kukataa dhambi zinazoweza uwa katika maisha yetu. Nguvu ya Mungu inatosha. Neema ya Mungu inatosha. Hakuna utaratibu wa kushinda njia zako. Paulo anatueleza kwa njia ya kawaida kabisa ya jinsi ya kuacha kilichokibaya na kuwa mtumwa wa haki. Ikiwa tutafuata mafundisho yake katika swala hili itatupelekea katika maisha ya ":Utakatifu". Mungu anafurahi unapokuwa na maisha safi na matakatifu mbele zake.

Msatri 20: *"kwa maana mlipokuwa watmwa wa dhambi mlikuwa huru mbali na haki."* Paulo anatujulisha kwamba kabla hatujawa waumini hatukuweza kutoka katika mitego ya dunia. Dunia inataka kukushawishi kwamba kile unachokifanya ni sahihi. Tunatakiwa tufikie hatua ya kuamua tuendeshwe na mambo ya mwili au tunendeshwe na haki ya Mungu.

Msatri 21: *"Ni faida gani basi mliyoipata siku zile kwa mamabo hayo mnayoyatahayarikia sasa. Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni mauti!"* Hapa Paulo anabonyeza kitufe cha kurudisha nyuma na kuturudisha kipindi hatujamwamini Yesu Kristo. Anatujulisha kwamba njia za ulimwengu mara zote zitatumalizia katika mauti ya kiroho. **Kifo**

cha kiroho ni pale tunapotengwa na mahusiano ya Mungu. Kuna tokeo moja tu katika dhambi nalo ni mauti. Matokeo ya haki ni uzima wa milele.

Mstari wa 22: *"lakini sasa mkiisha kuwekwa huru na kuwekwa mbali na dhambi na kufanywa watmwa wa Mungu mnayofaida yenu ndiyo kutakaswa na mwisho wake ni uzima wa milele."* Katika mstari huu Paulo anaeleza ni kwa jinsi gani mambo ya Ukristo yanavyotenda kazi:

1) Maisha ndani ya Kristo ni maisha yeney nguvu dhidi ya dhambi – tuko **"hru kutoka dhambi."**

2) Tnafanyika watumwa wa Mungu. Hatujimiliki. Mngu anatumiliki na sisi ni mammeneja wa vitu tulivyo navyo kwasababu kila kitu chema hutoka kwa Mungu.

3) Utakatifu unapatikana kutokana na kuishi maisha ya utii.

4) Kuishi kwa ajili ya kristo ni kuishi maisha ya milele pamoja na Kristo mbinguni.

Msitari 23: *"kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Bwana wetu."* Paulo anatuonesha kwamba uzima wa milele katika Kristo ni zawadi ya bure kutoka kwa Mungu. Hatuwezi kuianyia kazi zawadi ya bure. **Zawadi ni kitu ninachokupa kutokana na upendo wangu kwako na si kutokana na nguvu zako ili unilipe.** Jawabu la mtu anapokupa zawadi ni kupokea kwa shukuranina neema. Wokovu wetu katika Kristo ni zawadi ya Mungu, si malipo ya kitu Fulani tulichofanya. Waefeso 2:8-9 inatuambia, "mmekombolewa kwa neema kwa njia ya imani– na kwa matendo mtu asije akajisifu." Mungu hutoa zawadi hii kwa watu wote. Anatuonesha rehema, si kwasabu ya kitu chochote cha haki tlichokifanya bali ni kwa kile alichokifanya kupitia mwanawake Yesu Kristo.

Sehemu nzuri kabisa ya picha hii ni kwamba hatulazimishi hii zawadi. **Tnatakiwa kuipokea zawadi yake kwa Imani kwa sababu zawadi inatakiwa izinduliwe.** Kwa mano ninaweza kukuletea zawadi kutoka dukani ya thamani ya dola $100, lakini kama utaikataa hiyo kadi kwa kutokuitumia ili ufanye manunuzi faida ya ile kadi itapotea. Kwa namna ileile "tuna kadi" imewekwa ndani yetu na Mungu. Kabla roho haijahuishwa tunatakiwa tukubali kuipokea zawadi ya bre ya Mungu kwa njia ya imani katika Kristo. Zawadi hii imetolewa kwetu kwa nguv ya Roho mtakatifu. **Ni njia ya Mungu ya kuonesha upendo wake usio na masharti na msamaha wake kwa watu wote.** Ni njia ya kuhuisha nafsi ukombozi wake kwetu naturuhusu kuunganishwa na kila kitu alichonacho Mungu hapa duniani na mbinguni.

Mungu maeanzisha zawadi kwa matumizi hai ya Roho Mtakatifu. Kuikubali zawadi ya wokovu ni maamuzi yetu; Mungu halazimishi wokovu. Hutupatia nguvu na imani inayohitajika ili tuje kwake tukiwa hatuna msaada, tukihitaji na kuikubali zawadi ya wokovu. Zawadi hii ni fnguo inayofung mlango wa maisha ya amani ma maisha ya milele mbinguni. Ikiwa hujawahi kuhuishwa kwa kuikubali neema ya mungu ya wokovu je unaonaje kama utachukua hatua hiyon leo? Utajitoa kukaa katika njia takatifu na kukaa kwa amani katika neema yake na pendo na kuimarishwa na nguvu yake ya ubadilisho? Pendo la ukombozi la Kristo ni picha wazi ya upendo lake la kweli lisilo na masharti kwa ulimwengu mzima.

SURA YA 25

NI YESU TU ANAYEWEZA KUTUWEKA HURU

Warumi 7:1-6

"Kadhalika ndugu zangu ninyi pia mmeifia torati kwa njia ya mwili wa Kristo mpate kuwa mali ya mwingine yeye aliyefufuka katika wafu kusudi tumzalie Mungu matunda."
- Warumi 7:4

Katika Warumi 7:1-6, Paulo anatuonesha kwamba sheria haina nguvu kumwokoa mwenye dhambi. Katika sura za mwanzo tumesema kwamba wote tumehukumiwa mbele za Mungu na sheria na wokovu haupatikani kwa kutunza sheria. Haijalishi tukoje ni Yes pekee anayeweza kutuweka huru. Ngoja nikuulize swali: Je sheria inahusika name kama nimekufa? Hapana. Kwa nini? Adhabu haiwekwi kwa mtu aliyekua. Tunapomwalika Kristo katika mioyo yetu, fikiri nini kinatokea? **Tunakufa. Tumeshakufa katika asili yetu sasa ni viumbe vipya.** Nini kilitawala asili yetu? **Sheria**. Kwa hiyo pia tunapaswa kufa katika sheria.

Baadhi yetu kama wakristo tumezingatia katika utendaji nab ado hatujafa katika asili zetu za zamani. Mamabo yetu ya kale yanahitaji utendaji kuoneonekana vizuri, na kuwafurahisha wengine.– katika asili, utu wa kale ni kwa ajili yetu. Utu wetu wa kale umejawa hofu wakati wote. Utu wa kale hauwezi kuturuhusu kila kitu tukiache kwa Mngu na tumtegemee. Utu wa kale unataka ujitawale katika mazingira yake. Utu wa kale nataka uwe risasi. Utu wa kale nataka kusikilizwa na kusifiwa. Utu w kale unajisikitikia. Utu wa kale unataka kupambana. Tatizo letu si kwamba Yesu anashindwa kutusaidia tatizo ni kwamba hatumtegemei Yesu na kuuacha utu wetu wa kale. Kabla haujawekwa hur unatakiwa usijiangalie wewe bali nahitaji kubadilishwa na kumwangalia Yesu.

Je naelewa kabisa nini maana ya kuwamfuasi wa Kristo? Inahitaji kujidhabihu. **Hatua ya kwanza ni kumtumaini Kristo, turuhusu na kufa katika utu wetu wa kale.** Paulo anatangaza kwamba imani ktika Kristo inaleta kifo kwenye sheria na uhuru kutoka katika adhabu ya sheria. Unaona, tunaporuhusu utu wetu wa kale kufa, tunakuwa hatujaolewa na sheria. Ndoa yetu ya kwanza ni kwa Kristo, Bwana harusi mkuu wa kanisa. Kwa nini tunafungishwa ndoa na Kristo? Kwa nini tunauhusiano mpya naye? Nini kusudi halisi? Ni kwamba tuweze kuzaa matunda. Kusudi la mahusiano yetu na Kristo ni kutumiwa na Mungu kuuzidisha ulimwengu ili na wengine wawe na ndoa ile ile na Yesu Kristo (Wagalatia 2:19-20). Tunda la roho hutokea katika namna mbili:

1) **Mtazamo**: Roho mtakatifu atamwongoza Mtu ndani kuonesha mtazamo wa upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, uaminifu, kiasi (Wagalatia 5:22-23).

2) **Matendo ya Mungu**: maandalizi yetu ya kuja kwa Yesu mara ya pili. Wafilipi 1:11 inatuita tuwe "tumejazwa na tunda la haki linalotokana na Yesu Kristo."

Hili ndilo wazo la kuwekwa huru: Ikiwa maisha yetu ya ukristo yatawekwa chini ya mlolongo wa sheria jue utu wetu wa kale bado unatawala na tutaishi maisha ya bila amani. Lakini kama tutamrhusu Mngu ktawala maisha yetu na turuhusu mioyo yetu ihuishwe tutapokea upendo wa Mungu usio na kikomo na taonekana katika maisha yetu. Ikiwa mitazamo yetu au matakwa yetu ndicho kinachotawala katika maisha yetu sasa ni kipi ndicho kitakachokuwa

chanzo cha nguvu. Ikiwa tutajinyenyekeza kwa Yesu kutuongoza na kutuelekeza hapa tutakuwa tunatumia nguv ya Mungu. Hatuwezi kutumia njia zetu kfoka kwa Mungu. Kuishi maisha ya kujitahidi –yatatupelekea katika uangamifu. Kadri ninavyoendelea kukua ndivyo ninavyogundua uhuru wangu katika Kristo. Usalama wangu uko katika Kristo– si katika yale ninayoyafanya. Mara nyingi tunakosa kiasi na maisha ya nidhamu si kwa sababu hatufati sheria lakini ni kwasababu hatueloewi wazo la upendo wa Mngu na neema. Kama tutamruhusu roho wa Mungu abadili mitazamo yetu kutoka katika utendaji wetu na kumwangalia Yesu atatuweka huru tuishi na kumtumikia yeye kwa upendo na shukurani. Hii, rafiki yangu, ni kuishi **"katika namna ya Roho Mtakatifu"** (Mstari. 6). Wengine wanapokufanyia vitu vya kukuumiza utu wako wa kale ni kuangalia namna ya kurekebisha haraka iwezekanavyo. Lakini Paulo anatuambia katika msari wa sita 6 **"mtumike katika namna mpya ya Roho."** Kutumika katika njia ya Roho inamaanisha kuacha mambo yako yote ya tama mbaya, shauku za ajabu na yote ambayo ni ukinzani kwa Bwana na kumruhusu Kristo akujaze kwa roho wake. Tunatakiwa kuongozwa na Kristo Mtu anayeongozwa na Kristo ni Mkristo aliyejazwa na roho anayezaa tunda. Mtu anayejiita Mkristo lakini anajiendesha huyo ni Mkristo mwongo.

SURA YA 26

MAPAMBANO YETU YA DHAMBI

Warumi 7:7-13

"Tusemeje basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria kwakuwa singalijua kutamani kama torati isingalisema usitamani.'"- Warumi 7:7

Katika sura iliyopita tulitazama kwa undani jinsi gani yesu ametuweka huru kutoka katika utu wetu wa zamani. Kama wafungwa wa utu wetu wa kale baada ya kujaribu kujipima kwa sheria tumeona hatuwezi na wakati wote sisi ni wafungwa wa dhambi. Kabla hatujamtumaini Kristo na kuyatoa maisha yetu kwake tunakuwa tnaendeshwa na utu wetu wa kale. Lakini tunapomtumaini Kristo aendeshe maisha yetu yote tunakufa katika sheria (mstari. 5-6) na hatuwezi kuishi katika utu wa kale. Sasa **"tunatumika katika namna mpya ya Roho"** (Msatri. 6). Mtu aliyepotea hawezi kufanya jambo lolote kwa nguvu zake ili aende mbinguni iwe kwa kutunza sheria au kutenda matendo mema na hata kujaribu kutii amri. Atachanganikiwa na atakatishwa tamaa.

Paulo anatuambia kwamba tumruhusu Roho mtakatif aondoe macho yetu kutoka katika juhudi zetu na kumwelekea yesu. Roho mtakatifu atatuweka huru ili tumtumikie kwa upendo na shukurani. Hiki ndicho mstari wa sita unasema unapozungumzia katika kuishi **"kwa namna mpya ya Roho."** Katika sura zilizopita Paulo amesha sema kwamba sheria haziwezi kutuokoa (Warumi 3-5); haiwezi kututakasa (Warumi 6); na haiwezi kumuhukumu muumini (7:1-6). Na sasa anasema kwamba sheria inaseza kumanya mtu ajue shida yake awe anaifuata sheria na wale wanatenda dhambi (Mstari. 7-13). Mstari wa 7 unatupa swali zuri sana. Je sheria ni dhambi? Kwa maneno mengine kama tunapaswa kua katika sheria je tunatakiwa kuishi kwa viwango vya sheria? Je hii inamaanisha kwamba tunaweza kuishi kama tunavyoona? Paulo anasema, **"Hasha!"** Sheria siyo dhambi. **Sheria inatumika kama chombo cha kumuonesha Mkristo dhambi yake.** Paulo anaonesha pinti kadhaa zinazoonesha umuhimu wa sheria kwa wakristo wote, lakini nataka tuangalie moja tu katika sira hii: **Sheria huonesha dhambi**.

Mstari wa 7: *"Tueseme basi? Torati ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria kwa kuwa singalijua kutamani kama torati isingalisema usitamani.'"* Swala la dhambi ni la ndani. Ni vita iliyo katika mioyo yetu na katika akili zetu. Ni nguvu tu ya ubadilisho ya roho Mtakatifu inaweza kuondoa dhambi ya moyo na kuisafisha ili nikubalike kwa Mungu. **Jukumu la sheria katika mabadiliko ya mtu ni kutufanya tuelewe dhambi yetu.** Inatuonesha kwamba tunahitaji msamaha na ni Mungu pekee anayeweza kutupatia na inatulazimisha kukubali au kukataa kazi ya ukombozi ya kristo. Sheria inatuonesha kwamba hatuwezi kufaulu bila kuwa na nguvu ya mahyusianoya kweli ya kristo na mahusiano ya Kiroho na watu.

Tatizo tulilo nalo ni kwamba tunaweka imani kubwa katika mambo ya nje – malengo yetu, mapigo yetu, na kujisifia. Hii inaharibu sana hasa kwa wale tunaoona kuwa wamebarikiwa. Nioneshe mtu ambaye amefaulu name nitakuonesha watu kumi wanaomsema na wanajaribu kumshusha. Tunapaswa kuelewa maana ya m,afanikio. Mafanikio hayapimwi katika ukamilisho au kuona unastahili. Mungu anaeleza mafanikio kuwa na mahusiano na kumtii yeye. Katika macho ya Mungu mahusiano yetu naye na wakristo wengine ndicho jambo la maana.

Tunaweza kweli kabisa kumruhusu Mungu atupende bila masharti na tacheb kujitegemea? Hatupaswi kujitahidi ili tuonekane kupendwa. Hatupaswi kwamba lazima watu watukubali. Tunapojaribu kuwa kama watu wanavyotaka ndiyo maana tunashindwa. **Upendo wa Mungu ni bure.** Wengi wetu tunafuata sauti za ulimwengu. Kwa nini tunazifuata? Tunataka tukubalike. Tunataka tuupate upndo wa dunia. Kufuata sauti za dunia kunaonesha upngufu wa imani. Tunapaswa kuhakikisha kwamba tunafuata mopango wa Mungu katika msiah yetu na si mwtu mwingine. Kama tumepumzika, tna hasira, kujisikia vibaya, tama, shauku mabaya ujue hatuongozwi na roho wa Mngu na hatutembei katika imani ya kikristo. **Tafakari hili: Mungu anatupenda sana hataki atutawale. Wala hawezi kulazimisha upendo wake kwetu.** Ana Roho mtakatif anayeweza kutuonesha na kutusogeza kwake lakini mwishoni anataka tumtafute sisi wenyewe.

Wengi wetu tumekuwa na masharti katika upendo wetu. Wengi wetu tumeingia katika maswal ya kibiashara mamabo ambayo yametupelekea kuishi kwa nguvu zetu. Kama hatutatenda sawa kama tulivyokusudia kinatokea nini? Tunakata tamaa. Jambo ni hili: tuna uchaguzi. Tunakubali mambo ya ulimwengu au tunadai uhuru tlio nao kama watoto wa Mungu? Yuda alimkana Yesu. Petro alimkana yesu. Wote walikuwa wana wa Mungu waliopotea. Yuda hakustahimili alijinyonga. Petro alitambua akarudi kwa machozi. Petro alichagua uzima. Swali langu kwako utachagua nini?

Kujaribu kujipatia upendo wa Mungu si njia nzuri ya kuishi. Mungu anatupenda hapo tulipo. Ni vema tukavua sura za bandia ili tuonekane uhalisia wetu. Tutakapofanya tutajiona kuwa ni watu tulio tayari kupenda katika kristo. Wale wanaokuchukia kwa jinsi ulivyp wanaweza kuwa si aina ya watu unaowahitaji katika maisha. Kristo anataka atusamehe. Anataka atupende na aturejeshe. **Hatuwezi kujirejesha.** Hiyo ni kazi ya Mungu. Kama tutajaribu lazima tushindwe na kukata tamaa. Yesu anataka tuje kwake kama watoto. Anataka tumwache Mungu awe Mungu. Tumwache atufanyie yale hatuwezi kuyafanya.

Wafilipi 3:7-9 inasema, “lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya buzuri usio na kiasi kumjua Kristo Bwana wangu ambaye kwa ajili yake yeye nimepata hasara kwa ajili ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi kwa ajili ya kristo. Tena nionekane katika yeye nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani.” Utaacha mahangaiko yako ya dhambi kwa Kristo? Utamtegema kwa ajili ya nguvu ya kushinda dhambi? Hii inatokea tinapoweka mwenendo wa karibu na wa dani na Kristo na tunatamba kwa jinsi gani pendo lake lililo kwa ajili yetu.

SURA YA 27

MAPAMBANO YETU BINAFSI

Warumi 7:14-25

"kwa maana tunajua ya kwamba torati asili yake ni rohoni bali mmi ni mtu wa mwilini nimeuzwa chini ya dhambi."- Warumi 7:14

Sura kadhaa za mwisho tmeshughulika na swala la mapambano ya dhambi na jinsi gani ya kuwekwa huru katika Kristo. Tumejifunza kwamba dhambi ni kitu chochote tunachokifanya bla kumtii Mungu na kupngukiwa na utkufu wa Mungu. **Msingi wa kwa nini tunamapambano ndani yetu ni kwa sababu ya dhambi.** Katika sura hii aul kwa kweli amejiweka wazi na anatuambia jinsi alivyokuwa akihangaika kuhusu yeye mwenyewe.

Msatri wa 14: *"Kwa maana twajua ya kuwa torati asili yake ni rohoni; bali mimi ni mtu wa mwilini, nimeuzwa chini ya dhambi."* Utu wangu wa kale si wa kiroho na kama nitaung'ang'ania nitahangaika mimi mwenyewe na kuangukia katika nguv ya dhambi. **Hatuwezi kuishsha nguvu ya dhambi.** Hatuwezi kushinda vita vya dhambi sisi wenyewe. Hakuna hata mmoja bila nguvu ya Roho Mtakatifu tutashindwa na dhambi. Mungu kampatia kila mkristo nguvu ya pekee nguvu ya roho Mtakatifu. Tunaposhindwa nguvu hii ya kiungu inaturejesha tena. Haijalishi unamambo gani katika maisha wakati wote fahamu kwamba natumaini katika ubwana wa Kristo.

Msatri wa 15: *"maana sijui lile nifanyalo kwasababu lile nilipendalo silitendi bali lile nilikuialo ndilo ninalolitenda."* Paulo anaeleza kanuni tatu za msingi alizojaribu kuzifanya aliposhughulika na utu wake wa kale :

1) **Ufahamu siyo jawabu.** Anasema kadri alivyojifunza kuhusu Mungu ndivyo alivyojiona kuwa hafai kwa kulinganisha.

2) **Kujitathmini siyo jawabu.** Kujaribu kujitoa katika dhambi kwa nguvu zetu siyo jawabu. Tutashindwa mara zote na kuendelea kujisikia vibaya.

3) **Tabia nzuri siyo jawabu.** Tunapokuwa wakristo haimaanishi kwamba maisha yetu hayatajkuwa na dhambi. Kuwa kama Kristo ni mchakato wa muda mrefu. Tunatakiwa kuitegema nguvu ya ukombozi ya kristo kwa ajili ya wokovu wetu. Wala haupatikani kwa nguvu na juhudi ya tabia zetu nzuri.

Mstari wa 21: *"Bsi nimeona sheria hii ya kuwa kwang mimi nitakaye kutenda jema lipo lililo baya."* Popote tunakokwenda maovu yanatufuata na ndiyo maana siku zote tunatakiwa kujikabidhi kwa Bwana. **Tuufishe utu wa kale kila siku ili Kristo aweze kukaa nasi kwa utimilifu wote.** Paulo anasema nasi uhalisia wa maisha. Unaona mmisionari mkubwa kama huyu anateseka na matatizo ambayo hata wewe unashghulika nayo kila siku?

Msatri wa 22: *"kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani."* **Paulo anatuambia msingi wake kama Mkristo ni kuon njaa na kiu kwa ajili ya haki ya Mungu.** Yesu anasema katika Mathayo 5:6, "Heri mwenye kiu na njaa ya haki kwasababu atashibishwa."

Paulo anasema katika 2 Koritnho 4:16, “ijapokuwa ut wetu wan je unachakaa lani utu wetu wa ndani (Roho) unaanywa upya siku kwa siku.” Pia anasema katika Waefeso 3:16 kwamba “kufanywa imara kwa nguvu kwa kazi ya Roho wake katika utu wetu wa ndani.”

Kadri tunavyokuwa katika Kristo ndivyo tunavyoichkia dhambi. Kadri tunavyopenda kunyenyekea katika haki ya Mungu. Tunapokomaa katika Kristo tunatamani uhusiano wa kina na Yeye inayopelekea kuwatumikia wengine bila kutegemea kulipwa. Dhambi ian nguvu hata mtu aliyeokoka huendeshwa na utu wa kale katika kyafuata mapenzi ya Mungu ya mtu wa ndani. Bila Kristo dhambi itatulemea. Kwa sababu ya wokovu katika Kristo haiku sababu ya kuendelea kujaribu kuishinda dhambi kwa nguvu zetu. Kristo aliishinda dhambi na tumewekwa huru kwa nguvu zake.

Mstari wa 23: *“lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali inapiga vita na ile sheria ya akili yangu na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu.”* Hapa Paulo anazungumza kazi ya sheria ndani yetu– dhambi ianyoendelea kuishi ndani yetu ambayo hatujaiacha. Dhambi gani ndani yako inaendelea kukusumbua? Paulo alikuwa na shida hii ya ndani na ilikuwa halisi kama watu wengine walivyo . shida yako ni nini? Chochote unacho shughulika nacho unatakiwa kujuwa haya:

1) **Ni kubwa kuliko ulivyo.**

2) **Inakuendesha zaidi ya unavyojuwa.**

3) **Kuna njia moja tu ya kushinda mahangaiko yako** – kwa maombi kila siku yakabidhi kwa Mungu. Mwombe akupatie nguvu na akuweke huru.

Unahitaji msaada? Unahitaji uthibitisho kutoka kwa Mngu juu ya kitu Fulani? Mung atakusaidia kushinda mahangaiko yako. Iache nguvu halisi ya kristo ikuinue kwenye uhalisi ya ushindi dhidi ya dhambi.

Anza kuishi katika ushindi siyo kushinda. Kuishi ili ushinde unaishi maisha ya kjitahidi kitu ambacho huwezi. Kuishi maisha ya ushindi maana yake kwamba ushindi tayari uko katika Kristo. Kufahamu mwisho wa hadithi itakupa jasiri wa kwamba kristo anaelewa na kwamba wakati wote atakuwa pamoja nawe bila kujali mambo yakoje.

SURA YA 28

UZIMA KWA NJIA YA ROHO

Warumi 8:1-8

"Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya roho wa Uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru mbali na sheria ya dhambi na mauti."- Warumi 8:1-2

Katika jamii zetu tunamifumo ya haki. Mtu anaposhindwa kutimiza sheria Fulani sheria a haki inachukua mkondo ili kuleta usawa na kosa. **Ktika ulimwengu wa Roho kuna sheria ya haki pia.** Mifumo ya Mungu inatusihi tuishi kwa ukamilifu chini ya sheria ambayo hatuwezi kuikamilisha au kuikubali zawadi yake ya bure na kuwekwa huru kutoka mbali na sheria ya dhambi na mauti. Katika sura ya 8 ya Warumi Paulo anasema kwamba kama waumini wale tulio na maisha mapya ndani ya Kristo hawataingia katika hukumu waliyostahili walipokuwa wenye dhambi. Ikiwa mtu ameshatakiwa mauwaji uje atakabiliana na sheria ya ifo halafu inatokea hakimu anasema "hakuna hatia wala hukumu" kwa mtu huyu, inamaanisha nini? **Hashitakiwi. Mwachieni**.

Msatri wa 1: *"Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio ktika kristo Yesu"* Swala tunalokabiliana nalo ni kwamba kila mwanadam duniani yuko katika hukmu ya kifo. Kila mtu anahatia ya dhambi na kwa sababu ya hilo kila mtu anaelekea katika kifo cha milele. Mungu aliumba nafsi ziishi milele. Bila Kristo tunaelekea jehanamu; lakini Bwana asifiwe tunapoweka imani kwake anatutangaza "hanta hatia." Anatupatia zima wa milele na nguvu za kushinda dhambi na kufanya mapenzi yake.

Msatari wa 2: *"Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru mbali na sheria ya dhambi na mauti."* Roho wa uzima ni Roho Mtakatifu. 1 Wakorintho15:45 inatuambia, "Mtu wa kwanza Adamu akawa nafsi hai Adamu wa mwisho ni Roho yenye kuhuisha." Adamu wa mwisho ni Kristo. Kristo alifufuka kutoka wafu na kwa hiyo ni Roho iliyo hai. **Kristo ni roho inayotoa Uzima.** Paulo anasema nini katika Warumi 8:1. Watu wengi najaribu kuokolewa kwa sheria za Agano la kale na hadi wanachoka kwa kutunza sheria, na maelekezo na sheria za kiyahudi. Nani anayeyafanya haya? Ni makanisa ya leo. Kama tutaangalia kanuni na sheria hatujawekwa huru. Tunapomtumaini Krito atuokoe anaondoa mzigo wa kujaribu kupima na kuona hatwezi.

Unataka kuishi maisha ya uhuru? Fungua 2 Korintho 3:17-18: "aliporoho wa Bwana kuna uhuru." Kristo hatupatii uzima tu lakini pia uhuru. Tunapokubali na kuelewa kweli za Mungu tunafanywa kuwa kama yeye Kristo. Kristo ni taswira ya Mungu. **Kugeuzwa kwetu ni matokeo ya kuwa tayari kukubali majukumu kwa ajili ya Bwana wetu Kristo na shauku ya kumjua yeye.** Moja ya funguo za maisha ya kikristo ni kufa katika maisha yetu ya utu wa kale ili aweze kuishi ndani yetu na kupitia sisi. Funguo nyingine ni kuishi maisha ya kuongozwa na Roho. **Hii inamanisha kufuata Roho ya Bwana katika kila Nyanja ya maisha.** Kadri tunavyomfuata Kristo kwa Karibu ndivyo tunavyoendelea kuwa kama Yeye.

Mstari wa 3: *"Maana yale yasiyowezekana kwa sheria kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili Mung nkwa kumtuma mwanae mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa*

dhambi na kwa sababu ya dhambi alihukumu dhambi katika mwili." Yesu yeye mwenyewe alijitoa kama"sadaka ya dhambi" – sadaka ya dhambi zetu. Katika gano la kale, sadaka za wanyama ziliendelea kutolewa katika mahekalu. Dhabihu hizi zilionesha kwa jnsi gani waisraeli walikuwa wanaichukia dhambi. Dau ilibidi imwagike kwa ajili ya kuondoa dhambi (Mambo ya walawi 17:11). Lakini damu ya wanyama haikuweza kmaliza tatizo la dhambi za wanadamu. Waebrania 10:4 inasema, "haiwezekani damu ya mafahari na mbuzi kuondoa dhambi." Dhambihu hizi zilikuwa ni za muda tu hadi pale Yesu alipokuja na kuwa dhabihu ya kudumu. Yesu akalipa deni la dhambi zote kwa kufanyika kuwa dhabihu kamili pale msalabani.

Msatri wa 5: *"kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili bali wale waifuatayo roho huyafikiri mambo ya Roho."* Kuna aina mbili za watu katika ulimwengu: wale wanaoongozwa na maisha ya dhambi/wao wenyewe na wale wanaoongozwa na Mungu. Wale wanaojaribu kuendesha maisha yao mara zote hua kifo cha kiroho; lakini wale wanaoongozwa na Mungu wanaishi maisha ya furaha na amani. Kuendeshwa na roho haimanishi kila kitu kitakuendea vizuri haimanishi kwamba hautakabiliana na matatizo na changamoto katika maisha. Inamanisha kwamba utapata amani ya kuingu na nguvu ya kiungu kwa chochote kitakachojitokeza katika maisha. Tunamruhusuje Roho wa kristo katika Kutuongoza?

1) <u>Achilia.</u> Kabidhi kila kitu kwa Bwana. Sisi ni mameneja wa kila kitu alichotukabidhi.

2) <u>Njoo ukiwa safi</u> uje ukiwa safi mbele za Mungu – kuwa mwaminifu, uwe wewe. Huwezi kumdanganya Mungu.

3) <u>Kufa katika utu wako wa kale.</u> Ishi na ufe katika utu wako wa kale kila siku. Kabla ya kuishi kweli lazima tufishe tu wetu wa kale.

4) <u>Omba.</u> Omba kila asubuhi kabla ya kuanza siku yako. Ombea kila chakula. Omba kwa ajili ya kulala. Ombea wali katika mahitaji. Maomkbi ni kuzungumza na Mungu– ukimshukuru, ukimsifu, wasilisha mahitaji yako na mwombe akuongoze.

5) <u>Soma Neno la Mungu.</u> Litafakari na uliishi kila siku. Yoshua sura ya 1 inatueleza jisni gani tunaweza kufanikiwa.

6) <u>Mtumikie Mungu kwa ajili ya utukufu wake.</u> Jihusishe na mambo ya kanisa. Sisi sote ni mawakala wa Mungu katika safari ya kukamilisha kazi yake.

Mstari wa 7-8: *"kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu kwa maana haitii shria ya Mungu wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu."* Dhambi hainyenyekei mamlaka ya Mungu. Yakobo 4:4 inasema, "Enyi wazinzi hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? **Yeyote anayechagua kuwa rafiki wa dunia huwa adui wa Mungu."** Majivuno ndiyo hupelekea tuwe marafiki wa dunia. Inatufanya tujione sisi na tunaona kwamba tunastahili yale ambayo dunia inayo. Inaleta tama. Tunawezaje kuyaondoa majivuno. Biblia inatufundisha kwamba tunaweza kushinda majivuno kwa unenyekevu kwa njia ya nguvu yaKristo. Tunatakiwa kutamba kwamba kila kitu kuhusu dunia ni dhambi. Yatatupelekea katika uharibifu. Kile Mungu anachoweza kutupatia ni zaidi. Ni maisha ya furaha

inayopelekea amani ya milele na amani ipatayo mambo yote. Unataka kumkumbati Roho wa Mungu na umweke awe dereva wa maisha yako?

SURA YA 29

UTAMTAMBUAJE MKRISTO

Warumi 8:9-15

"Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu ninyi hamfuati mwili bali mwaifuata roho lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo huyo si wake."- Warumi 8:9

Ikiwa itakuwa kama bata itatembea kama bata na italia kama bata na lazima itakuw ni bata, si ndiyo? Hata hivyo mambo huonejkana kufanana lakini kwa hali halisi hayafanani. Mtu mmoja alisema, "usiamini kile unachokisikia na uamini nusu ya kile unachokiona." Hii inaleta swali zuri la kitheologia. Unawezaje kumjua kwamba huyu ni Mkristo? Je ni Mkristo kwa sababu nasema mimi ni kristo?

Katika sra iliyopita tumesema kwamba Mtu asiye na Kristo anaongozwa na utu wa asili ya kale lakini palipo na roho wa Mungu humwongoza Muumini. Ikiwa hauna roho wa Kristo haujaokoka. Katika sura hii Paulo anaendeleza jambo hili na anatupatia mambo ya kuangalia katika maisha yetu wenyewe.

Moja ya jambo muhimu la sisi kuelewa ni kwamba kila aliye na Roho wa Mungu huyo ameokoka. Utajuwaje kama Roho wa Mungu anaishi ndani yako?

1) **Utaamini kwamba mwana wa Mungu ni Yesu na uzima wa milele unapatikana katika yeye.** 1 Yohana 5:5 inasema, "mwenye kuushinda ulimwengu ni nani? Isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni mwana wa Mungu."

2) **Maisha yako yataonesha sifa za Roho wa Mungu.** Wagalatia 5:22 iansema, "lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, uvumilivu, wema, uaminifu."

3) **Utajuwa nani ndiye chanzo cha Nguvu.** Warumi 8:26-27 inasema, "kadhalika roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo. Lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuuguwakusiko weza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijuwa nia ya Roho ilivyo kwakuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."

4) **Utawezeshwa kumtumikia Bwana na kufanya mapenzi yake.** Matendo 1:8 says, "lakini mtapokea nguvu akiisha kuwaijilia juu yenu Roho Mtakatifu nanyi mtakuwa mahahidi wangu Yerusalemu, Yudea, samaria na hata mwisho wan nchi."

5) **Utakuwa sehemu ya mpango wa Mungu kulijenga kanisa.** Waefeso 4:12-13 inasema, "kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu hata kazi ya huduma itendeke hata mwili wa kristo ujengwe. Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu hata kuwa mtu mkamilifu kuika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo."

Mstari wa 9: *"lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu ninyi hamfuati mwili bali mnamfuata Roho lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo huyo si wake."* Ikiwa roho

wa Mungu anaishi ndani yako wewe ni Mkristo. Paulo anawelekeza wasomaji wake katika ukweli kwamba shetani ana nguvu zilizo na kikomo, zinazoathiri maamuzi tunayoyafanya kila leo. Anafafanua kuathiriwa kama "asili ya dhambi." Ni muhimu kwetu sisi kuelewa kwamba asili yetu ya dhambi inaharibu mawazo yetu, tama nahata matendo. Mkazo umewekwa katika Roho wa Kristo. Hii inathibitisha kwamba hatjimiliki. Kama wakristo tunamilikiwa na Kristo.

Mstari wa 10: *"Na Kristo akiwa ndani yenu mwili wenu mekufa kwa sababu ya dhambi bali Roho yenu I hai kwa sbaabu ya haki."* Ikiwa Kristo anaishi ndani yenu basi utu wenu wa kale umekufa, "kwa sababu ya haki ya Kristo roho yenu imehuishwa." Fikiria hivi: mwili ni sehemu yako ambapo dhambi ilizaliwa na ni sehemu ambapo dhambi ianweza kukaa. Hata hivyo tnapompokea Kristo kwa imani tunageuzwa na kuwa mtu mpya. Mtu mpya anachanzo cha nguvu mpya ambacho ni Kristo. Kristo ndani yetu mwili wetu mekufa. Mwili unapokfa dhambi inakiosa sehemu ya kuishi. **Hii inatuhitaji tufe kila siku ili dhambi isijidhihirishe katika miili yetu.**

Msatri wa 11: *"lakini ikiwa Roho mtakatifu yeye aliyemfufua Yesu Kristo anakaa ndani yenu yeye aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu atahuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa kwa Roho wake anayekaa ndani yenu."* Paulo ahapa nanasema Roho Yule Yule aliyemfufua Kristo kutoka wafu ni Roho Yule anayeishi dani yetu kama Wakristo. Roho mtakatifu ni ahadi ya Mungu na arabuni ya uzima wa milele .
1 Wathesalonike 4:14 inasema, "Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka vivyo hivyo na hao walio lala katika Yesu Mngu atawaleta pamoja naye." **Dhambi hutulemea kama wanadamu**. Gonjwa la dhambi limemuharibu kila mwanadamu. Inamshusha kila mwanadamu. Dhambi inaiba aamni yetu na furaha na kuweka maumivu na shida. Hakuna mwanadamu anaweza kushinda dhambi kwa nguvu zake. Dhambi inatusababisha tuendeshwe na shetani. Yohana 12:31 inasema, "Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo. Sasa mkuu wa ulimwengu huu atatupwa nje."

Sasa nini hatima ya kumaliza matatizo yetu ya kibinadamu? Kila mtu anapaswa kuamua. Nani akutawale, Yesu au shetani? Kila Mkristo wa kweli anaroho wa Mungu anaye ishi ndani yake. Roho wa Mngu anamfanya asiwe muongo, mwizi, kujivuna, uchungu kwasbabau hayo ni mambo ya watu waliopotea. Mtu aliyeokoka hpendelea mambo ya Mungu. Mtu aliyeokoka ni mnyenyekevu. **Hajivuni au kusifiwa kwasababau usalama wake uko katika Kristo.**

Msatri wa 13: *"kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili mwataka kufa. Bali kama mkiyaisha matendo ya mwili kwa Roho mtaishi."* **Ikiwa sitamruhusu Kristo kuiangamiza dhambi dhambi itaniangamiza.** Dhambi ni tatizo na Kristo ni jibu. Shauku ya mioyo yet inapaswa kuwa ni kumtii Mungu na kufuata mapenzi yake. Si kwa sababu tunaishi kwa maadili na kufanya vizuri haimanishi kwamba eti ndiyo tujisikie vizuri. Kuishi vizuri kwa ajili yetu bila kumruhusu Mungu ndiye achukue nafasi haitufaidi kitu. Kila kitu tunachokifanya kinatakiwa kiwe kwa ajili ya kristo. **Ikiwa ni muhimu kupata sifa kwa ajili ya yale tunayoyafanya hiyo itakuwa ni majivuno na kujipenda na siyo kunyenyekea na kuwa na upendo usio na masharti.** Majivuno yanatuendesha tunapojifariji kwamba tunauwezo wa kutawala dhambi za siri maishani mwetu. Shetani atatuvamia tunapohisi kwamba eti tuko vizuri kiroho. Wale wanaojiona kuwa wamekamilika wanajidanganya. Wakati mwingine njia rahisi ya kujidanganya ni sisi wenyewe. Tunaweza kufanya mema yote lakini kwa mtazamo mbaya na

roho nyingine na kupoteza malengo mazima ya maisha ya Ukristo ambayo ni kuishi kwa upendo wa utukufu wa Mungu.

Mstari wa 14: *"Kwakuwa wote wanaoongozwa na roho wa Mungu hao ndiyo wana wa Mungu."* Paulo anasema wale wanaoongozwa na Roho wa Mungu ni "wana wa Mungu." Katika tamaduni za Rumi mtu liyefanywa kuwa mwana anapoteza haki zake zote za famil;ia yake ya kwanza anapata haki mpya kwa familia aliyoingia mpya. Kwa hiyo anakuwa ni mrithi kabisa wa mali za baba yake. Tunapokuja kwa Kristo tunapata faida zinazoendana na kuwa mwana wa Mungu. **Tunapata urithi sawa Kma Kristo.** Tunakuwa wana wa Mungu.

Mstari wa 15: *"kwakuwa hamkumpokea tena roho wa utumwa iletayo hofu bali mlipokea roho ya kufanywa wana ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba.'"* Kama wana wa Mungu hatupaswi kuogopa bali uwe na furaha kwani ba do tunahiriki katika hazina za mbinguni.

Hapa kuna njia tano za kuuwa dhambi katika maisha yako kwa njia ya nguvu ya Kkristo:

1) **Ungama dhambi zako kwa Mungu katika maombi.** Hatua ya kwanza ni sisi kuwa safi tnapokuja kwa Mungu. Hadi tuwe wenyewe kabisa katika misha yetu.

2) **Elekeza Moyo wako kwa Mungu.** Unapoelekeza Moyo wako kwa Mungu naishi kwa ajili yake na unaweka ulinzi mkubwa dhidi ya shetani.

3) **Tafakari Neno la Mungu.** Tenga muda kwa siku wa kujifunza neno la Mungu. Soma kwa ubora na si kwa idadi. Yaishi maandiko kwa njia ya kivitendo.

4) **Piga magoti kwa ajili ya maombi.** Unapokuwa katika magoti yako huwezi kushindwa. Watu wanaopiga magoti mbele za Mungu ni ishara ya unyenyekevu kwa Bwana Kristo. Muda mwingi Mungu huwa nafurahi tnapopiga magoti kwa kumpenda, bila kumwomba atatue matatizo yaliyo katika maisha yetu.

5) **Uwe mtii kwa Mungu.** Mungu anataka tutembee naye. Hataki ujadili naye kama vile, "Bwana kama tanibariki nitakupatia 25% ya Baraka ulizonipa." Swali ni, "Ni kiasi gani natoa sasa?" Utii ni wa maana sana kuliko dhabihu yoyote unayojaribu kufanya.

Swali ni: Nini kinakuzuia usimanye Mungu awe halisi katika maisha yako?

SURA YA 30

NI LAZIMA TUISHI KWA ROHO

Warumi 8:10-13

"Basi kama ni hivyo basi tu wadeni—si wa mwili tuishi kwa kufuata mambo ya mwili kwa maana kama tukiishi kwa kufuata mambo ya mwili mwataka kufa bali mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho Mtaishi."- Warumi 8:12-13

Umewahi kufikiri maisha ya Kikristo yanaweza kuwaje bila kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu? Ninaposafiri kwenda Brazili kufanya kazi na watu wa Brazili, tunajenga makanisa, vituo vya jamii, vituo vya afya, shule za ufundi stadi na msingi wa ujenzi wote ni Zege. Zege ina nguvu na inaimarisha. Kutengeneza zege inahitaji mchanga, kokoto, maji na simenti. Vitu vyote hivi ni muhimu sana katika kutengeneza Zege; hata hivyo, **cha muhimu zadi katika vyote ni simenti.** Bila kuwa na simenti yale mahitaji mengine yatakuwa hayana uimara. Katika maisha yetu ya Kiroho Roho mtakatiu ni muhimu sana kwa ajili ya sisi kuishi maisha katika Kristo.

Swali jingine linaweza kuwa, "Roho mtakatifu yuko katika maisha yako? Je unaelewa kabisa kaziya Roho Mtakatifu? Anafanya nini? Kusudi lake ni nini?" katika sura ya mwisho tumezungumza kwamba kuna aina mbili za watu katika dunia: wale wanaoongozwa na asili yao ya dhambi na wale wanaoongozwa na Roho Mtakatifu. Ikiwa roho Mtakatifu jaendeshi maisha yako uje unakoelekea siyo. Badala yake unakuwa kama watu wanaosema "Ndiyo" kwa Kristo lakini hawaishi kwa ajili ya Kristo. Hili ni jambo la kimila katika dunia leo hii. Paulo anasema kwamba kuishi kwa ajili ya kristo ni ushahidi wa kwamba tuna Roho Mtakatifu.

Ukweli ni kwamba shetani anataka tuone kwamba tunaweza kuishi kama tunavyotaka ili mradi tu tusimdhuru mwingine. Paulo anasema hiyo siyo kweli. Katika mstari wa 12 Paulo anasema kwamba "tuna deni lakini si la maisha ya dhambi." Kama wakristo jukumu letu ni "Kuishi kwa Roho na kufisha matendo ya mwili" (Mstari wa 13). Maisha matakatifu yanatoka kwa Roho Mtakatiu. Bila Roho hatuna uzima. Ikiwa tutakuwa waminifu na tukajiaminisha ujue tutaishia katika mambo ya Muda lakini ndani tutapungukiwa amani ya kweli amabyo inaweza kupatikana kwa mahusiano na Kristo tu.

Itakuwa ni mbaya sana kuja kwa Mungu siku ya hukumu halafu aseme, "Mwanangu uliokolewa kama mtoto lakini umeharibu miaka yote kwa kufanya uliyoyataka bila kuniuliza ulitaka ufanye nini"? Kama Wakristo sisi ni mali Mungu katika Kristo. Mungu anataka tuishi katika uwezo wa Nguvu za Roho Mtakatiu. Roho yake ni mwalimu, wakili, kiunganishi chetu na Mungu, mlinzi na mwelekeo wetu.

Tukirudi katika mstari wa 11 Roho mtakatifu ni arabuni ya uzima wa milele kwa wale wanaomtumainia. Roho mtakatifu yuko ndani yetu kwa imani tunauhakika wa kuishi na Kristo Milele. Katika Wagalatia 5:24, Paulo anasema, "waliomali ya Kristo wamesulubisha mambo ya asili." Kile Paulo anachosema ni kwamba kama kweli, katika imani, tulipokea zawadi ya bure ya wokovu katika Kristo nguvu ya Roho Mtakatifu pamoja na uamuzi wetu, anatangaza, "ni wakati wa kufisha ya kale." Kuna nyakati katika maisha ya kila mtu tunapaswa kuchora msatri ardhini. Tunapaswa kuwa wa Mungu kabisa au la.. kama tutakuwa wa Mungu Mungu atatupa nguvu na ujasiri wa kuangamiza na kuzika yale ya kale. Labda baadhi yetu tunaruhusu mambo ya kale

kutuendesha. Lakini jambo zuri kwa Mungu ni kwamba anatupenda sana, anataka tumrudie na kusema, “Bwana, nisamehe, Bwana nirejeshe. Nataka nikufahamu zaidi nataka nyazike ya kale nianze upya na kuwa na maisha mapya na wewe.”

Hiki ndicho tunatakiwa kukifanya katika maisha yetu. Ilinitokea nilipokuwa na umri wa mika 28. Nilikuwa Mkristo lakini nilikuwa siishi kwa ajili ya Kristo. Sikumruhusu Yesu kuniongoza. Nikaamua kwenda safari ya kimissionari ili nimtumikie Mungu. Mungu alinipeleka umbali wa mile 5000 ili kunionesha kwamba ananipenda. Mngu alibadili sana mfumo wangu wa maisha. Tangu hapo Mungu akaanza kunibadilisha na kunisaidia kuelewa mapenzi yake maishani mwangu hata leo, anaendelea kunitengeneza ili niwe mtu anayehitaji niwe. Je ungependa yesu we si mwokozi wako tu lakini Bwana wa maisha yako? Hatuwezi kuwa kamili. Kila mmoja wetu anajinsi yake anavyotabika lakini tukimruhusu Kristo kutawala katika maisha yetu tutaona amani ya ndani na nguvu ya ndani ambayo itakuwepo anapokuwepo.

SURA YA 31

WAMINI WANASHIRI KATIKA UTUKUFU WA MUNGU

Warumi 8:17

"Na kama tu watoto basi tu warithi, warithi wa Mungu warithio pamoja na Kristo naam tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye."- Warumi 8:17

Miaka ya 90 nilipata muda wa kuwa na ndugu anaitwa Daudi. Daudi alikuwa ni mtu aliyetembea kwa imani kila siku. Alikuwa na kazi nzuri ya urubani katika kampuni kubwa. Mungu akasema naye kuanzisha huduma yake. Aliacha kazi yakena akaanza huduma ya khubiri kwa watu katika mitaa kwa kutumia rangi zing'aazo na taa nyeusi. Rafiki yangu, Wade Akins, alifundishwa kitu kilekile nay eye pamoja name tulisafiri miji mingi tukionesha mkanda wa maisha ya Yesu na kuchora hiyo michoro kwa hizo rangi na taa. Siku moja baada ya mkutano daudi na mimi tulikuwa tunazungumza nikamuuliza kipi kilikuwa ni muhimu kwangu kama mkristo kujuwa. Alizsema, "Usiguse utukufu wa Mungu. Utukufu wa Mungu ni wake yeye na anatupatia kwa sababu ya jinsi tunavyompenda. Ikiwa tutaugusa, na kuharibu tnakuwa tumechukuwa makusudi ya utukufu wake."

Sura hii inahusika na ukweli kwamba Roho mtakatifu wa Mungu ni arabuni ya utukufu wetu kwa sbaabu ya wokovu katika Kristo. Kama waumini hatuko chini ya dhambi. Kwa kuwa dhambi bado inatukabili tunawez kuishinda tutakapo mtumainia Bwana na kuweka adabu ya kumfuata na kutimiza mapenzi yake. **Mungu kanipatia yote mema aliyo nayo kwa sababu ya jinsi anavyonipenda.** Mwana wa Mngu alikuwa ni kitu muhimu alichokitoa. Hakutupatia mwanawake tu bali roho wake mtakatifu, msamaha na uzima wa milele. Anataka tumwombe chochote tunachokitaka. Wengi wetu tunaweza kuwa katika matatizo. Neno la Mungu linatuambia kwamba anaweza kutupatia tunachohitaji. Ninapotafakari hili ninakumbuka kichwa cha habari cha wimbo wa zamani, "subiri msaada unakuja".

Mstari 17: *"Na kama tu watoto basi tu warithi– warithi wa Mungu warithio pamoja na Kristo; naam; tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye."* Kwa maneno mengine Paulo anaweka wazi tofauti kwamba kwa kuwa ni watoto wa Mungu kwa hiyo ni warithi. Kwa sisi kuelewa kile anachosema tunatakiwa tuwaelewe wasikilizaji wake: Warumi. Sheria ya Warumi na sheria ya wayahudi zilikuwa ni mifumo miwili tofauti. Kwa mfano, katika mila za kiyahudi kijana mkubwa alipokea mara mbili ya urithi wa familia lakini katika tamaduni za warumi kila mtu katika familia hata wale waliofanywa wana walipokea Urithi sawa sawa.

Tunafahamuje kwamba sisi ni wana wa Mungu? Hebu turudi kidogo mstari wa 16 16: *"Roho mwenyewe hushudia pamoja na roho zetu kwamba sisi ni wana wa Mungu."* Tunapofanyika Wakristo tunapata haki sawa kama tulivyokuwa katika mila za Warumi. Moja ya faida yenye nguvu kabisa ambayo tumepewa ni Roho Mtakatifu. Pauo anatuonesha jinsi gani Roho wa Mungu atatenda kazi ndani yetu katika Wagalatia 4:5-6: "Wakati ulipotimia, Mungu alimtmma mwanawake, aiyezaiwa na mwanamke chini ya sheria ili kwamba tupate haki zote za Mwana. Kwa sababu mmekuwa wana Mungu akamtuma Roho wa mwanawake katika ioyo yetu. Roho aliaye Aba, yaani Baba.'"

Sasa turudi mstari wa 17b: *"naam tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye."* **Kuna gharama za kulipa ili uwe Mkristo**. Paulo anazungumza juu ya mateso yake. Katika karne ya kwanza walikabiliana na changamoto za uchumi, mateso ya kijamii na hata kifo kwa kuwa Mkristo. Ni mateso gani tunakabiliana nayo kama Wakristo hapa Marekani? Kama tunavyofahamu tuko katika presha ya kutaka kufanana na ulimwengu. Tunapotaka kumfuata Kristo kabisa tunakutana na misukosuko kutoka duniani. Lakini hebu tuangalie sehemu ya mwisho ya mstari wa 17b: "ili tuoate na kutukuzwa pamoja naye." Roho mtakatifu ni arabuni ya utukufu wetu. Je Mungu anaweza kutukuzwa bila mateso? **Hakuna utukufu bila mateso**. Kila jambo linalopelekea tuteseke leo Mungu anataka alitumie kwa ajili ya utukufu wake kupitia sisi kama waumini. Wengi wetu tunaona mateso kuwa si kitu kizuri. Paulo aliona kama ni njia ya kumletea Mungu utukufu. **Ikiwa tutaona mateso kama si ,itu kizuri ni alama ya wazi kwamba tumejiangalia wenyewe na si Mungu.** Mungu atatumia matukio na mamabo mbalimbali ili kutukomaza. Kuhesabiwa haki ni mwanzo wa wokovu na utukufu ni utimilifu wa wokovu.

Kabla ya anguko la Adamu alikuwa hana dhambi. Aliuona utukfu wa Mungu kwa sababu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Lakini Adamu aliposhindwa alipoteza utukufu na akawa ni kiumbe mwenye dhambi. Warumi 3:23 inatuambia "Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." **Tukitulia na kuwaza tunaona kwamba wengi wetu tunajichukulia utukufu nje na Mungu.** Hii ni swala la kujitahidi mwenyewe kitu ambacho utaishia katika kuchanganyikiwa na kukata tama. Lengo langu ni kwamba kusudi la wokovu ni kusamehe na kuwasafisha watu dhambi zao na kuwarejesha katika utukufu wa Mungu. Utukufu tunaoupata kupitia dhabihu ya kristo ni mkubwa mno kuliko hata alioupata Adamu kabla hajatenda dhambi.

Swala la mbinguni ni kubwa mno kuliko la hapa duniani. Kama tutapokea urithi tutapokea na promosheni. Yohana 17:17 inasema **kwamba tutapokea utukufu sawa na wa Kristo na kufanyika wamoja naye.** Kwa sababu ya imani na wokovu tnaurithi wa pamoja na Kristo. Tito 3:7 inasema "tumehesabiwa haki kwa neema yake [ili kwamba] ili tufanywe warithi kulingana na tumaini la uzima wa milele." Hapa ndiyo kuna jambo la maana: Ikiwa wewe na mimi kama wakristo hatuingii katika kuja mara ya pili kwa Kristo na tunaishi katika mapenzi yake ujue tumefungwa katika mambo ya ulimwengu. Kabla hatujamtumikia Yesu tunatakiwa kuwekwa huru toka katika vitu vya ulimwengu. Mpaka tutakapojitambua kama raia wa mbinguni ("lakini wenyeji wetu uko mbinguni na tunamsubiri mwokozi huko Bwana yesu Kristo." Wafilipi 3:20), tumaini na tegemeo la kushiriki katika utukufu wa Mungu itufanye tuishi kwa ajili ya kristo. Changamoto yetu wote ni kujua kile Roho wa Mngu ametuthibitishia kuwa ni utukufu na kwamba inachohitajika sana ni Kristo kuishi ndani yetu na siyo sisi kujitahidi kufika mbinguni.

SURA YA 32

MAISHA YAJAYO

Warumi 8:18-25

"Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu."- Warumi 8:18

Tumeelezwa katika sura zilizopita kwamba wakristo wote wa kweli wamepokea "Roho ya kufanywa wana." Wakristo wote. Siyo washirika wa dhehebu Fulani. Siyo wale waliozamishwa au kunyunyiziwa. Siyo wale walioweka tamko la kutamani. Bali ni wale walio WaKristo w Kweli moyoni wamefanywa wana katika nyumba ya Mungu. Wanafanyika wana wa Mungu kwa njia ya Kristo mwana. Wanapokea maisha ya kiungu na kiroho kutoka kwa Mungu kwa jia ya Kristo, na maisha yale yanaonesha chanzo. Sisi ambao ni wakristo wa kweli kila siku tunakuwa kama Kristo katika mienendo yetu, katika familia zetu, katika makanisa na hata katika utu wetu wa ndani. Sura hii inaeleza mambo ya mwili na jinsi utakavyoisha:

1) Mwili bado ni chanzo cha udhaifu.

2) Mwili ni dhaifu kwa sababu ni kiti cha dhambi.

3) Mwili hauko kwa ajili ya mambo mema.

4) Mwili uko katika sheria ya dhambi na kifo.

5) Mwili si wa milele kama Baba alivyouvuvia pumzi ya uzima.

6) Mwili ni umebaki kuwa ni vifungo nab ado haujafanywa kuwa mwana.

Mstari tunaouangalia leo katika ulinganifu na ujumbe wa Paulo unatazama sana katika mabadiliko ya mwili. Mistari hii inaonesha mahusiano ya roho iliyohuishwa kama taji na kilele cha kazi ya ukombozi na kutangaza kwamba hadi mabadiliko yatakapotokea, Wakristo wanatazamia kurudi kwa mara ya pili. Katika maneno hayo ya Kiroho: "Nitasubiri hadi mabadiliko yangu yatakapotokea."

Tujuwe kwamba maisha ya baadae ya mwili yanahitajika ili kutupatia maelezo na uimara wa wazo la kuharibika. Injili imekazia sana katika mambo yajayo na kuaminisha na kwa kunguvu kwa sababu ya mkazo wake wa tangazo la ufufuko na maisha ya baadae ya mwili. Injili inafundisha kwamba kutakuwa na ufufuko na kwamba tutakuwa na sehemu katika ufalme wa Mungu. Uthibitisho wa kutokuharibika katika Injili umetolewa katika maswala ya kihistoria ya kufufuka kwa Yesu Kristo na kupaa kwake mbinguni. Ni wazo hili kwamba Injili inapata nguvu na kubadilisha wazo la kutoharibika kuwa ni imani thabiti ambayo tayari tunayo katika uthibitisho wa historia.

Mawazo ya yajayo ya maisha ya baadae yanatimiza shauku za moyo. Moja ya sababu inayotufanya tusinyae katika wazo la kifo ni kutokuwa tayari kuachana na marafiki wetu wa zamani – miili yetu. Mawazo yote ya yajayo yasiyoonesha maisha ya mwili yanakosesha

mwaliko wa kutokuwepo. Mwili utakaofufuliwa ni mwili wa utukufu. Ni bure. Tunapaswa kutafasiri “ufufuko wa mwili” kwa maelezo ya mitume. Kuna vitu vinapingana katika miili yetu na siku moja tutaishi.

1) Mmoja umetupwa katika uharibifu na mwingine hauharibiki.

2) Mmoja umetupwa bila heshima na mwingine umefufuliwa katika utukufu.

3) Mmoja umetupwa katika udhaifu na mwingine umefufuliwa katika nguvu.

4) Mmoja umetupwa katika mwili wa asili na mwingine umefufuliwa katika mwili wa kiroho.

Tunatakiwa tuangalie katika mawzo ya Paulo katika sura ya 5 ya 2 Wakorintho. Hapa anatumia ulinganifu wa aina mbili kuonesha mwili wa muda mfupi na mwili wa utukufu unaomiliki maisha yajayo.

1) Nyumba ya dunia hii – nyumba ya udongo, inaisha lakini kwa Muda.

2) Nyumba ya Mungu ambayo haijafanywa kwa mikono nani ya milele mbinguni.

Tunafahamu kwamba miili yetu ya sasa haiku kamili. Inamakosa. Mwili wa ukombozi takuwa kamili kwa ajili ya mawasiliano na Mungu wa milele. Huo mwili amabo ni war oho naweza kuwa maana yake kuwa ni wa kinja, unawazika sana, una hekima na unaelewa. Mwili huu wa ukombozi ndani yake hautakuwa na mchanganyo bali utakuwa ni msaada war oho na chanzo cha nguvu kwa wadhaifu.

Mwili wa ukombozi utakuwa ni matokeo ya kukaliwa na Roho wa Kristo. Mkristo katika roho yake hai anakuwa kazaliwa mara ya pili. Mkristo atatamani muda zaidi maana atakuwa katika hali ya roho, nyumba ya m,binguni ya Mungu. Ikiwa roho wqa Mngu aliye mfufua Kristo kutoka wafu anaishi ndani yenu atauharakisha mwili wenu wa uharibifu kwa roho Yule Yule. Mwili wa ufufuko umeahidiwa kwa kila mtu lakini wengine watafufuka kwa ajili ya maisha ya milele, hakuna utukufu hakuna uzuri wala Baraka. Ukweli ni kwamba utafufuliwa. Nataka uishije milele? Njia pekee ya inayopelekea utukufu wa ufufuko ni njia ya imani katika Kristo yesu. Kama tutajiachia kwake:

1) Ataweka roho wake katika roho wetu.

2) Atatuongoza na kututakasa maisha yote.

3) Atatuokoa kwa kukaliwa na roho wa uzima utoka katika sheria ya dhambi na mauti.

Tunapoanza kufikiri juu ya mauti tfuate mfano wa Paulo. Mtu huyu wa Mungu alifurahia kifo. Kifo kwa Paulo haki8kuwa ni adui bali rafiki maana alijua kinamaanisha nini kuwa nyumbani mwa Bwana. Umewahi kufikiri juu ya mauti? Sisi sote siku moja tutakfa lakini katika Kristo tumeahidiwa mwili mpya na makao mapya.

SURA YA 33

ROHO MTAKATIFU HUOMBA

Warumi 8:26-27

"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba ipasavyo lakini roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa."- Warumi 8:26

Sura hii inazungumza jinsi sisi waumini tunavyopata mawasiliano wa kimaombezi kutoka kwa Roho Mtakatiu. Umeshawahi kuwa dhaifu kiasi kwamba hata unakuwa hujui fanye nini? Umewahi kujaribu kuomba lakini unashindwa? Kama wakristo Mungu kaisha tuandalia kitu cha kutusaidia tunapofikia hatua ya kutaka kupoteza matumaini. Unafuu huu huja kwa mfano wa Roho Mtakatifu. Moja ya ahadi ya Mngu ni kwamba atatupatia kitu cha kuweza kutusaidia katika matatizo yetu. Hata kama hatujui nini tuombe Roho Mtakatifu anatuombea na kumfahamisha Mungu nini tunataka. Kama tukiomba kwa mapenzi ya Mungu yafanyike na tumtegemee Mungu kwa ajili ya matokeo anaahidi kuwepo kwa ajili yetu katika mchakato. Mara nyingi kumekuwa na daraja kati ya mategemeo yetu na kile Mungu alichonacho kwa ajili yetu.

Tumejifunza katika misitari ya 19-20, "uumbaji unasubiri kwa ham sana mategemeo ya wana wa Mungu yaweze kufunuliwa." Katika mistari ya 23-25, Paulo anatuambia , "Waumini huhuzunika." Sasa tunaona kwamba Roho Mtakatiu huhuzunika. Mstari wa 26 na 27 unatutaarifu, *"Roho mwenyewe hutuombea kwa jinsi kusikoweza kutamkwa."* Uumbaji huhuzunika. Waumini huhuzunika. Roho Mtakatifu huhuzunika.

Katika mistari hii tunamuona Roho Mtakatifu anaweka sahihi ya "Kushindwa" kwa mwanadamu, dunia, na ulimwengu. Mstari wa 21 unatuambia, "kwa kuwa viumbe navyo vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu hata viingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu." Mstari wa 19 unasema, "kwa maana viumbe vyote vinategemea kwa shauku nyingu kufunuliwa kwa wana wa Mungu." Halafu tnaingia katika mstari wa 26 na 27: *"kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo lakini Roho mwenyewe htuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."*

Sehemu hii inahitimisha mtazamo wetu wa utukufu usioweza kutamkwa, na kuugua kwa Roho Mtakatifu. Sehemu hii ni muhimu sana ni ngumu kwetu kuielewa na hasa faida zake. Ni kutiwa moyo kwa ajabu kwa sbabu inasema kwamba kama waumini tunaojuwa uzito wa "Kushindwa kwetu" tunaougua katika miili hii ya ubinadamu na tunasubiri ukombozi wa miili yetu na nafsi zetu kuokolewa.

Tunasubiri mwili wa ukombozi. Si ndiyo? Tnasubiri kutoka katika miili yetu hii "Ya kushindwa" na kuingia katika utukufu. Paulo anasema kwamba Roho wa Mungu yuko ndani yetu anaugua kwa jambo hilo hilo. Tuko salama kwa makusudi ya mwana. Tuko salama katika maendeleo na nguvu za Roho Mtakatifu na kama yeye anavyotamani tutukuzwe katika yeye. Jkama tunavyougua Roho pia huugua. Tunapookoka ni vizuri kufahamu upande wa Mungu katika nafasi yetu. "Anguko letu" na ubinadamu ni kazi ya Roho Mtakatifu kama ilivyosema.

Je naweza kujitunza na kujiokoa? Hapana. Nani atakayeniokoa? Roho wa Mungu. Hiyo ndiyo kazi yake pekee. Anaomba kwa niaba yetu pamoja na Bwana Yesu Kristo. Roho huingilia udhaifu wetu. Ni neno kubwa hilo. Linamaanisha "udhaifu wetu," yaani "Angukoletu." Si maombi yetu dhaifu lakini hata udhaifu wetu wote matatizo yetu yote kama wanadamu tulio katika mwili, mwili uharibikao, hali hii ya dhambi. Tunawezaje kukaa tumeokoka? Htuwezi, kwa sababbu hata kuomba hatujui. Huo ndio ukweli. Na hata vsielewi kama Wakristo wanaelewa msingi huu wa kweli ya kiroho.

Unaona hili ni tatizo. Tulipojifunza miaka kadhaa juu ya usalama wa milele, tunasema, "sawa umeokoka, umeokoka milele." Na tumekubali kwamba hiyo ni kweli. Lakini kwa namna Fulani tnakuwa tumesahau jambo la maana kwamba tumethibitishiwa kwamba usalama wa milele kwa sababu ya maombi yasiyo koma ya Roho mtakatifu. Hivyo tunapaswa kutoa shukurani kwa Mwana anayetuombea na hata hutuombea shetani anapotaka kutukamata. Pia tunapaswa kushukuru kwamba Roho wa Mngu anatusaidia katika dhaifu wetu. Hatuwezi kuwa tumeokoka hadi pale mwombezi wetu asimame mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Hii ni kweli kuu. Waebrania 7:25, dunaukumbuka huo mstari? "kwa hiyo anauwezo wa kuwaokoa wale wanaomjia Mungu kupitia Yeye kwa maana yuko katika kuwaombea." Inamaanisha nini kuokolewa kabisa? Inamaanisha kuokolewa hadi mwisho. Ina maanisha tang siku ya wokovu hadi siku ya utukufu tunaokoka kabisa. Inawezekananje? "Yeye anaishi akituombea."

Kit kinachotufanya tuendelee kuokoka, mwombezi Kristo kwani kuhani mkuu ni kwa ajili yetu. Hatuna Kristo mbinguni akituombea tu bali tuha Roho Mtakatifu akituombea ndani yetu. Tunakuhani mkuu mwaminifu, ambaye ni Kristo, mbinguni tubnakhani mkuu mwaminifu ambaye ni Kristo, katika miyo yetu, kwani Roho mwenyewe ndiye anayetuombea. Neno linguine lililotumika kaka Kristo ni katika Waebrania, **"Kwa ajili yetu."** Tsingeweza kufika katika utukufu. Tsingeweza kuomba kwani hatujui hata kuomba ili kujilinda katika vita vya kiroho. Kwa hiyo tunamsaada kutoka kwa Mwokozi mbinguni na Roho Mtakatifu duniani. Ni wazi kwamba hatujui kuomba si ndiyo?
Katika 2 Wakorintho 12, Paulo liomba mara tatu ili bwana aonde mwiba katika mwili wake. Mara tatu Bwna alifanya nini? Hakuanya lolote. Hakuondoa mwiba. Na Paulo akaamua kwamba haijalishi yuko katika hali gani lazima atulie. Alijifunza jambo ambalo kila mmoja wetu anapaswa kujifunza. Hatujui kuomba. Hatujui vya kuombea. Kama wanadamu tko dhaifu sana..

Roho matakatifu hutuombea. Inamaanisha nini. Inamaanisha kumwokoa mtu aliye katika hatari na hana jinsi ya kutoka. Na ndiyo maana shetani anatenda kazi kwa jaziba sana kwa wamini na anataka awakamate kwa jaziba wale wanaolitaja jina la Kristo. Shetani anajua kwamba tunatunzwa na nguv za Kristo na nguvu za Roho mtakatifu kwa hiyo anapigana na Roho na Kristo kwa jinsi anavyweza ili kwamba angalau aharibu kazi yao. Sasa tunajua kwamba Kristo hayuko msalabani amefufuka yuko mbinguni na hivyo anaangalia yanayoendelea. Hapana, anatenda kazi ili kuvilinda vitu vyote vikiwemo vitu vya ukombozi na roho wa Mungu hajaisha. Hajaacha kufanya tangu mwisho wa miujiza ya mitume. Anatuombea. Anaitafuta nguvu ya Mngu. Anakuja kutuokoa tunapokuwa hatuna msaada na umeona kuna mkazo katika mstari wa 26, **"Roho mwenyewe."** Ni kazi yake.

Roho mtakatifu anaona na kutambua udhaifu wetu si kwamba tunatenda dhambi tu lakini hatujui hata kuomba ili kujilinda. Na Roho Mtakatifu yuko kwa ajili yetu ndani yetu kwa ajili ya

utukufu. Anataka tuwe katika sura ya Kristo. Na huu ni moyo wa Mngu Baba. Na huu ni moyo wa Mungu Mwana. Na huu ni Moyo wa Mungu Roho. Roho wa Mungu anatenda ndani yetu ili atupatie mapenzi kamili ya Mungu. Roho wa Mungu hutend ili kuleta mazao ya mwisho.

Sasa hebu twende mstari wa 27. Katika sura iliyopita tumekuwa na roho anayetuombea. Msatri wa 27 unasema, *"Na yeye aichunguzaye mioyo aijua Nia ya Roho ilivyo, kwakuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo Mungu."* Nani anachunguza Mioyo? Bwana huonesha mchakato wa mawazo yake 1 Samweli 16:17: "Mwanadamu huangalia kwa nje lakini Bwana huungalia Moyo." Zaburi 139:1-2 inasema, "ee Bwana, umenichunguza na unanijua. Unanijua ninapokaa na ninapokuwa nimeamka, unayatabua mawazo yangu." Matendo 1:24 inatuambia, "Bwana anaujua moyo wa kila mtu." Na Warumi 8:27a inasema, "Yeye aichunguzaye mioyo anajuwa Nia ya Roho." Huyo ni Mungu. Hilo pia ni jina la Mungu, mchunguza Mioyo. Anajua nia ya Roho. Roho anatuombea na Mungu katika utukufu wake anasikia. Na halafu hivi, "Kwa sababu roho huwaombea watatifu sawa na mapenzi ya Mungu" (Mstari. 27b). Haujui mapenzi ya Mungu Yeye anajuwa. Unaweza usijue jinsi ya kuomba. Yeye anajuwa. Unajuwa nini maana ya kuomba "katika Roho"? inamaanisha kuomba kulingana na mapenzi ya Mungu. Mungu anajuwa Roho anaomba nini "kwa sababu anaomba sawasawa na amapenzi ya Mungu."

Kwa hiyo Roho huomba sawasawa na mapenzi ya Mungu, mwana anaomba sawa sawa na mapenzi ya Mungu na Mungu anasikia na kuelewa maombi yao na anajibu. Kwa huduma yao ya maombi tunalinndwa. Kwa hiyo ikiwa watu watakuja na kusema, "Sawa ninaamini naweza kupoteza wokovu wako," huyo anakuwa amepiga kazi yaMwokozi na Roho. Hilo siyo jambo dogo katika mabishano ya makanisa. Hiyo ni kuuliza nguvu ya Mwana wa Mungu na Roho wa Mungu.

Mungu anamsikia Roho. Roho anaomba kulingana na mapenzi ya Mngu. Nzuri sana. Utaanza kutumia vitendea kazi vyako vilivyo katika boksi la vifaa? Pokea hazina ya maana tulyo nayo– Roho Mtakatifu

SURA YA 34

MUNGU ANATENDA KAZI WAPI?

Warumi 8:28-30

"Nasi twajuwa ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema yaani wale walioitwa kwa kusudi lake." -Warumi 8:28

Sura hii imebeba ahadi kubwa tunayoipata katika Biblia. Ni ahadi inayotufanya tupumzike. Ni ahadi ambayo Mungu huwapatia watoto wake. Msatri wa 28*: "Nasi twajuwa ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema yaani wale walioitwa kwa kusudi lake."* Nataka tuuvunje vunje mstari huu ili tuone kile Paulo anachokiwasilisha katika kanisa la Rumi.

1) **"Nasi twajuwa."** Paulo anaanza kwa uwazi kwamba Neno la Mungu ni kweli. Kusema kwamba "Unajuwa" kitu Fulani inamaanisha unauhakika. Paulo anasema kwamba usalama wa milele umedhihirishwa kwetu na Mungu ili kwamba sisi waumini tuwe na uhakika na tumbembe Mungu katika neno lake. Hapa kna swali: Unajuwa kabisa? Unajuwa kwa uhakika kwamba wokovu wako uko salama? Paulo alikuwa na uelewa wa kimungu jinsi gani kazi ya Mungu ya ukombozi. Alijuwa kwamba kwasababu ya uaminifu wa Mungu wokovu wake uko salama.

2) **"katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao."** Ngoja nikuulize swali: Ikiwa banki yaCitiGroup itakuhakikishia mkopo wa dola milioni $ 10 inamaanisha nini katika ulimwengu wa kiuchumi? Ina maanisha kwamba imelipwa? Hapana – tumeona mambo haya katika makampuni makubwa duniani . Je kuna uhakikisho wa asilimia 100% katika swala la kifedha duniani? Hapana! Lakini vipi nikikwambia kwamba Mungu anaenda kukupatia mkopo? Utafikiri nini? Ndiyo, ikiwa Mungu ndiye mtoaji unauhakika na pesa. Kwa nini? Kwasbabu hajashindwa kutimiza ahadi. **Mungu hutenda.** Tunakuja kwake kwa imani tukitamba udhaifu wetu. Hatuwezi kujirekebisha wenyewe. Mungu anaweza kuturekebisha. Anafanya nini? Mambo **"yote"** . Nini maana ya vitu "Vyote."?; inamaanisha hakuna utaalamu, hakina mipaka, hakuna kukataliwa, na hakuna masharti. Ngoja niseme kwamba ahadi hii niyamasharti, hata hivyo. Ahadi inahusika na sisi katika kumpenda Mungu. Biblia inatuambia kwamba tunaweza kumtamba mtu anampenda Mungu kwa utii wake kwake. Tu huwa hasemi kwa maneno tu. Upendo ni tendo siyo maneno tu. Kwa hiyo upendo wetun umehakikishwa kupitia maisha yetu na si kwa kile tunachokisema.

3) **"Siyo urefu wala kina, siyo kitu kingine kile kinaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."** (Warumi 8:39) Tazama Mungu hasemi anawazuia watoto wake wasiguse vitu vinavyoweza kuwadhuru. Anasema kwamba anazo nguvu za kuchukua mambo ya kufisha, mabaya, na kuogopesha na kuyatumia kwa ajili ya utukufu wake na kwa ajili ya faida yetu. Hebu tuangalie 2 Wakorintho 7-10. Tunapoteseka, Mungu anatumia kwa ajili ya faida yetu. Kwa hiyo **"katika yote Mungu hutenda mema kwa wale wampendao,"** Kazi ni utendaji wa Mungu, siyo sisi. Unaona, Nguvu ya Mungu na mapenzi ya Mungu ni makubwa kwa kila kitu tunachoweza kukiwaza. Unaamini katika nguvu za Mungu? Unaamini

kwamba Mungu hutenda katika mambo yote kwa ajili ya Mema? Inamaanisha nini hasa? Inamanisha kwamba mUngu anauwezo wa kuchukua hata laana iliyo juu yako kwa njia ya upendo na kweli ili kwamba aweze kutukuzwa. Wema wa Mungu na uaminifu hutenda kwa ajili ya mema kwa watu wake. Neno la Mungu ni kwa ajili ya mema yetu. Yakobo 1:2-3 inasema, "Hesabuni kuwa ni furaha, ndugu zangu mnapoangukia katika majaribu." 1 Petro 1:7 inasema, "haya yametokea ili imani yenu – iwe ya thamni kuliko hata dhahabu iliyo safishwa kwa moto – ili uhakikishwe." 2 Wakoritnho 12:9-10 inasema, "Ndiyo maana kwa ajili ya Kristo ninafurahi katika dhaifu na hata magumu, katika mateso na hata katika magumu. Kwa sababu ninapokuwa dhaifu ndipo nina nguvu." Nguvu inakuja kwa sababu ya kujishusha na nguvu inapatikana kwa sababu ya kustahimili magumu katika maisha. **Matatizo mengi tunayokuwa nayo ndipo tunazidi kujifunza kumtegemea Mungu na tunapomtegemea Mngu ndipo tunapata nguvu ya kweli.**

Unaona, ugumu na mateso yanaweza kutufundisha zaidi jinsi tlivyo zaidi ya kitu kingine katika ulimwengu. Shida za maisha zinatufundisha masmo ya thamani ambayo hatuwezi kujifunza popote pale. Mateso yanapelekea tuwe na unyenyekevu na kuwa na tabia ya kweli. Kuna tofauti kati ya unyenyekevu wa uongo na unyenyekevu wa kweli. Mtu wa kweli aliyejinyenyekeza ni mtu aliye wazi na anahuruma kwa ajili ya wengine bila kujali wakoje.

Mwaka mmoja wakati wa krismasi, niliona kitu cha kufurahisha wakati kundi letu la kujifunza Biblia lilikuwa likipiga kengele kwa ajili ya jeshi la wokovu mbele ya chumba cha kupumzikia kwenye dukala Jackson, Tenesee. Niliona kwamba mara zote watu maskini walikuwa wnatoa sana kuliko hata wali matajiri. Nikajiuliza swali; kwa nini mtu maskini anatoa pesa kwa mtu ambaye hata hajawahi kukutana naye? Kwa nini wanatoa hali hawana kitu kabisa. Kwa nini walio na pesa hawatoi na wanadharau tu. Jawabu likawa kwamba mtu maskini huwa natamba taabu zilivyo na mtu tajiri hawezi labda awe aliwahi kuwa maskini. Kadri mtu anavyozidi kupata ndivyo huyu mtu anavyozidi kuvitegemea. Ni vigumu kuwa tajiri halafu uwe umemwishia Bwana kwa kina. Niliomba siku moja usiku, "Mungu asante kwa ajili ya maumivu yangu kwani naona umenibadilisha. Ninapokuwa sina nguvu ndivyo ninavyozidi kukutegemea."

Maumivu yanatupelekea tujiagalie tena kwa karibu na kwa watu wengi majivuno ni tatizo. Wanaume, Mungu anatuambia kwamba mamabo yote haya yanafanyika kwa wema kwa wale wampendao. Hata mtu unayedhani kuwa anahuruma hapa duniani Mungu anaweza kumtumia kwa ajili ya mema. Mathayo 12:30 inasema, "Yeye asiyekusanya name huyo hayuko pamoja nami." Upendo halisi kwa Mngu ni kuunganikana naye na kuwa na shauku ya kumfahamu. Upendo halisi unaonekana katika maish ya kila mtu kila siku kwa kutegemea nguvu za Mungu anakuwa makini na mtiifu kwa mapenzi yake, anatamani kumpendeza Mungu, anawapenda watu wake na anchukia maovu. Ninakupa changamoto leo uyatoe maisha yako katika kumfuata na kumtumainia. Utamtumainia hata kama haujisikii?

CHAPTER 35

KUCHAGULIWA TANGU ASILI

Warumi 8:29-30

"maana wale aliowajua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. Na wale aliowachagua tangu asili hao akawaita na wale aliowaita hao akawahesabia haki na hao aliowahesabia haki hao akawatukuza."
- Warumi 8:29

Sura hii inahusika na kuchaguliwa kwanza. Hili ni jambo ambalo wantheologia wamekuwa wakijadili miaka hadi miaka. Wengine wanaamini kwamba Mungu kuna wat aliowachagua ili wapokee zawadi yake ya wokovu. Wanatazama Waefeso 1:11 inayosema, "na ndani yake sisi tulifanywa warithi huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye mwenyewe ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake mwenyewe." Wengine wasema kwamba Mungu aliwajwa wale watakaomkubali na ameshaweka alama kwao (wamechaguliwa tangu mwanzo). Neno "kuchaguliwa tangu asili" linamanisha "Kutambuliwa kabla ya misingi ya dunia". Hii ni namna nyingine ya kusema kwamba alama ya ukombozi wa Mungu ni utendaji wa Mungu, na siyo sisi. Kwa sababu ya upnedo wake usio na kikomo Mngu ametufanya kuwa watoto wake. Hatustahili kufanywa watoto lakini kwa ajinsi ya upendo wake kwetu ametuneemesha na kutufanya tuwe katika familia yake. Neema ya Mungu ni hiari wake, ni upendeleo wa wokovu anaoutoa kwa wale wanaookolewa kwa kuweka imani yao kwake. Wokovu hautabikiwi na wala hatustahili. Hakuna akili au juhudi za kimaadili zinaweza kutupatia neema ya Mungu kwasbabu intoka pekee kwa Mungu na rehema zake na upendo. Bila neema ya Mungu hakuna mtu anayeweza kuokolewa. Kupokea wokovu lazima tutambue na kushukuru kwamba hatwezi kujiokoa bali Mungu ndiye anaweza kutuokoa na njia pekee ya kupokea wokovu wake ni kwa njia ya imani katika Kristo. Hiki ndicho ninachokifahamu kuwa ni kweli:

1) Kusudi la Mungu kwa ajili ya watu wake siyo kwamba lilikuja baadae bali lilikuwepo na kristo kabla ya hata misingi ya dunia.

2) Mungu alimtuma mwana wake Yesu kristo kwa ajili ya watu wote na siyo kwa baadhi ya watu.

3) Mngu anafamu vitu vyote, yeye anamamlaka. Hakuna wakati kwa Mungu. Miaka maelfu kwa Mungu ni kama sekunde kwa hiyo kumwona katika namna mbalimbali hatuwezi kujua uwepo wake. Nguvu yake haina kikomo; kwa hiyo anauwezo wa kujuwa na kufanya mambo yote kulingana na neno lake. Hata hivyo japo anafahamu mambo yote haimaanishi kwamba ndiyo azuie pendo wake usio na masharti au apunguze mateso ya dhambi ya watu wote. Dhambi ya mwanadamu imebatilishwa kwa wale wanaoweka imani kwake. Kristo amekuaj kuwaweka "wote" huru kutoka katika vifungo vya dhambi. Hatuwezi kuingilia nafasi ya Mungu. Katika mtazamo wangu Mngu aliwachagua tangu asili wale watakaokwenda mbinguni na wale wataokwenda jehanamu haiwakilishi kweli ya maandiko. Kama mtu ata twaa nafasi hii tujue sisi ni madhabahu ya Mngu na anatuongoza. Kwa upande mwingine mtu anayetwaa nafasi ambayo mwingine anaweza kuifanya hiyo haitakuwa ni maandiko.

Maamuzi ya mwanadamu haimaanishi kwamba amekuwa mkubwa kwa Mungu. Nafasi ziko katika mitazamo ya falsafa za mwanadamu na zinaleta mkanganyiko kwa waumini.

4) Mungu anatumi roho Mtakatifu kuwaleta watu wote kwa Kwake. Roho anakazi muhimu. Wengine wanasema uhiari wa mwanadamu nimhimu kuliko mamlaka ya Mungu; Huwa sisemi mtazamo huu . wengine wanaamini kwamba mamlaka ya Mungu inamanisha mwanadamu hana uamuzi. Huwa sizungumzii hili pia. Nafasi yetu ni kuipokea zawadi ya bure ya wokovu kwa imani au kuikataa. Mngu halazimishi uoendo wake kwetu. Anaturuhusu tufanye maamuzi. Tunaweza kuamini na kuweka imani kwake au kukataa. Ikiwa atatulazimisha kumoenda basi upendo wake utaklwa wa masharti.

5) Maamuzi ya mwanadamu ni ya pili katika mamlaka ya Mungu. Kwakuwa Roho wa Mungu anatusihi kuelekea wokovu ni uamuzi wa mwanadamu kukubali au kukataa. Mamabo haya yote yatabaki kuwa ni siri hadi tutakapokuatana na Bwana. Ksema kwamba mwanadamu anaweza kuwa na majibu yote siyo kweli. Najua kwasbabu nimekuwa mtu wa jinsi hiyo. Kile ninachokijua ni kwamba ni hiki: Uopendo wa Mungu ni wa milele. Hekima yake na nguvu zake ni kuu. Tyunapomkubali kama Bwana atatuongoza na kutuhifadhi hadi siku tutakayosimama katika uwepo wake. Upendo wa Mungu ni kwa "Wote" Mwana wa Mngu amekuja kuwaweka watu "wote" huru na kwa sabahu hatuwezi kuelewa nguvu zake wala kuzijua tunapaswa kumwamini na tuelewe kuwa ahadi zake ni kweli.

Mstari wa 29: *"Maana wale aliowajua tangu asili aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa mwana wake ili yeyeb awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."* Sehemu ya kugeuzwa inaitwa "Utakaso" ikimaanisha ":Kuwa kama Kristo" au "Kutangazwa kuwa mtakatifu" tunapoikubali kweli ya msamaha kwa jia ya kristo maka dhabihu ya mauti tunalikubali neno la Mungu kama kweli na kutusafisha na tunatakaswa kutoka katika dhambi zetu (Yohana 17:17).

Msatri wa 30: *"na wale aliowacagua tangu asili hao akawaita na wale aliowaita hao akawahesabia haki na wale aliowahesabia haki hao akawatukuza."* Paulo anaorozesha hatua za kupata ufahamu katika mchakato wa muumini. Zifuatazo ni mawazo ya msingi paulo anayaeleza kwa Warumi kueleza wokovu katika Kristo:

1) **Kuchaguliwa:** (Warumi 9:10-13) Uchguzi wa Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au hatima. Kwa mfano, Mungu alichagua Isareli. Mungu aliamua watu wote waje kwake lakini anatambua si wote watakubali zawadi yake ya wokovu.

2) **Kuchagua Tangu asili:** (Warumi 8:29) Je Mungu anajua nani ataokoka? Ndiyo lakini kujua kwake hakuwezi kuingilia maamuzi yetu ya kumkubali kwa Imani.

3) **Kuhesabiwa haki:** (Warumi 4:25) Tendo la Mungu la kututangaza "hatuna hatia" kwa ajili dhambi zetu.

4) **mateso:** (Warumi 3:25) Uondolewaji wa adhabu ya Mungu juu ya dhambi kwa njia ya dhabihu kamili ya mwana wake Yesu Kristo.

5) **Ukombozi:** (Warumi 8:23) Ukombozi ni gharama iliyolipwa kwa ajili ya uhuru. Yesu aliwakomboa wale waliomkubali kwa imani kwa njia ya kifo chake msalabani.

6) **Utakaso: (**Warumi 5:2) Kuwa kama Kristo kwa njia ya ya Roho Mtakatifu. Kuondoa na kujaza Kristo utupu ulio katika maisha yetu kwani ni mchakato wa Utakaso.

7) **Utukufu: (**Warumi 8:18) Hii ni hali halisi ya muumini baada ya kifo tnapokuwa kama Kristo (1 Yohana 3:2).

SURA YA 36

MBADALA WA UPATANISHO WETU

Warumi 8:31-38

"Yeye asiyemwachilia mwana wake mwenyewe bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?"- Romans 8:32

Paulo anahitimisha sura ya 8 ya warumi na kile wanazuoni wengi wanaita **"Wimbo wa Usala."** Paulo anauliza swali kali linalolingana na nyakati hizo. Swali ku lilikwa **"Mtu anaweza kpiteza wokovu wake?"**

Msatri wa 31: *"Basi tuseme nini juu ya hayo?"* Hapa Paulo anaeleza mafundiho ya upatanisho kwa niaba yetu. Hata hivyo lengo la pointi hii linaendanan na usalama wa upatanisho wa Kristo. Hebu tusimame hapa kidogo na tlivunje vunje hili somo. Hivi badala ya Inamaanisha nini? Inamaanisha kitu kinawekwa kwa niaba ya kitu Fulani. Mungu alimweka mwana wake katika nafasi yetu kwa upatanisho wa dhambi zetu. Upatanisho inamaanisha nini? Kwa sababu mtu hawezi kuwa haki kwa ajili yake mwenyewe Mngu kwa neema yake akafanya ukombozi kwa njia ya dhabihu ya mwana wake Yesu Kristo. "Kupatanisha" Inamaana ni "kunganisha au kurekebisha na kuweka sawa kosa." Kwa kila kosa kuna hukumu. Kosa letu ni dhambi. Kristo akatupatanisha dhambi zetu na kifo chake msalabani. Akabadilisha maisha yake na yetu. Akachukua nafasi yetu; Kwa hiyo, akawa ni upatanisho kwa niaba yetu.

Mtu anapomkumbatia Kristo katika imani ya toba, Kristo, ambaye hana dhambi, mwana wa Mungu kamili, anatosherza dhambi zetu na anatuweka katika amani ya milele. Hili ni jambo la muhimu kulielewa kwa sababu tunapaswa kuelewa kwamb Kristo amefanya kazi kwa ajili yetu msalabani. Kwa maneno mengine kazi ya upatanisho ya Yesu kristo ni msingi wa uhakika wetu – uhakika wa wokovu wetu. Tnapokuwa tumeokolewa milele sasa tunakuwa huru kumwangalia Kristo na wema wake na kuachana na mambo yetu. Tunakuwa na uhakika wa kumtumikia Mungu kwa ujasiri kwani hakuna kitu kinaweza kututenga na upendo wa Mungu. Tunapofahamu wokovu wetu tunaanza kufahamu amani inayoimarisha imani yetu katika Kristo. Mungu alitupatia Mwana wakekama ushuhuda wa pendo Lake Kwetu. Yesu hajalipa deni la dhambi yetu tu lakni pia kwa ajili ya dhambi za dnia nzima. 1 Yohana 2:1-2 inasema, "watoto wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi na kama mtu akitenda dhambi tunaye mwombezi kwa baba Yesu Kristo mwenye haki. Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu wala si kwa dhambi zetu tu bali na kwa dhambi za ulimwengu wote."

Msatri wa 31b: *"Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye juu yetu?"* Tafasiri ya kiyunani inaasema, **"Kwa sababu Mungu yuko nasi."** Ikiwa mtu anaweza kutuibia wokovu atakuwa ni mkubwa kuliko Mungu. Mungu ni mtoaji wa wokovu na ndiye anayeulinda. Paulo anataka kujua kama kuna mwenye nguv zaidi ya Mungu? Daudi alikuwa na ujasiri katika Bwana. Katika Zaburi 27:1 anasema, "Bwana ni Nuru yangu na wokovu wangu –nimwogope Nani?" Yesu alikuwa dhambihu yako na mimi msalabani. Kuna makusudi mawili ya mngu yasiyobadilika– Ahadi yake na wosia wa kuiheshimu ahadi. Mungu hatafuti imani timilifu lakini anataka tuwe na imani thabiti isiyokanwa inayolalia kwa Kristo.